ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais

20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 05 Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, katika kikao chako cha Baraza la Wawakilishi cha tarehe 29 Mei, 2017, Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Afya na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi. Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, wizara hiyo imeleta majibu kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, wakati likijibiwa swali Nam. 101, lilouzwa la nyongeza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyetaka kujua wizara imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya Kitengo cha Saratani katika bajeti ya mwaka wa Fedha 2017/2018. Mhe. Spika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Kitengo cha Saratani kwa mwaka 2017/2018 ni jumla ya Shilingi za Tanzania Billioni Moja (1,000,000,000/-).

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani ya hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka 2017/2018. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano naomba kuweka hati mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, leo tutakuwa tunahitimisha hoja ya Wizara ya Afya, sasa wachangiaji nilionao watakuwa wawili tu. Nitamwita kwanza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye atafuatiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Afya na baadae mtoa hoja atakuja kutoa majumuisho. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwa mtu wa mwanzo asubuhi hii kuendelea kuchangia hoja hii muhimu kwa taifa letu. Mheshimiwa kwanza nitoe pongezi maalum kwa Mhe. Waziri wa Afya, Naibu Waziri na watendaji wote katika kipindi kifupi kutokana na mabadiliko makubwa yaliyojitokeza katika sekta ya huduma za afya, hii inaonesha wazi uwezo mkubwa wa Waziri na Naibu Waziri katika kutekeleza majukumu yao, tuwaombee Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo huo ili waendelee kukamilisha kazi kubwa iliyo mbele yao ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameeleza kwa kina.

Aidha Mhe. Spika, niwapongeze sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa namna walivyochangia hoja hii, kwa namna walivyoonesha hisia na imani kubwa kwao kwa wananchi wetu ili tuweke utaratibu ulio bora zaidi katika kuimarisha huduma za afya. Kwa hivyo, kwa niaba ya serikali napenda niwapongeze sana wajumbe hawa kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutoa maelezo mazuri na naamini Mhe. Waziri wa Afya atajitahidi kuzijibu hoja zao kwa kina sana, maana na yeye ni mahiri, ni muelewa katika kipindi kifupi kabisa ameweza kufanya vizuri katika wizara hii.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba serikali imesikia sana kilio cha Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa jumla kuhusu matatizo yanayojitokeza katika sekta ya afya. Nataka niwahakikishie kwamba dhamira ya serikali ni kutoa huduma bora za afya na huduma nyengine muhimu katika nchi yetu. Inaelewa matatizo mengi ambayo mmeyasema na inafanya kazi katika kuyatafutia ufumbuzi, na tayari kuna maelekezo wameshapewa Wizara ya Afya kupitia kwa Mhe. Waziri ili azidi kujipanga vizuri yeye na safu yake katika kuyapatia ufumbuzi mambo mengi ambayo waheshimiwa wameyasema hapa. Kwa ufupi suala la huduma za afya sio kwa kwetu tu dunia nzima ina mtihani katika kutoa huduma bora

katika sekta hii, hususan katika mazingira ambayo nchi kama yetu masikini inayobeba jukumu kubwa la kutoa huduma hizi bila ya malipo lazima tuchukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa imani kubwa kwa wananchi wake katika kubeba mzigo mzito wa kutoa huduma hizi za afya bila ya malipo. Wananchi wanachangia pale panapokuwa na uwezo wa kuchangia, lakini kwa zaidi ya asilimia 95 serikali inachangia huduma hizi.

Mhe. Spika, nataka nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwanza kwa imani yake kubwa katika sekta hii lakini kwa uelewa mkubwa alionao katika sekta hii. Yeye ni bingwa katika fani hii anaijua, anaielewa, anaisimamia kwa karibu ili yatokee mabadiliko makubwa. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu naomba tuungane kwa pamoja katika kuyaelewa matatizo ya msingi, lakini katika kuivumilia serikali wakati inatekeleza wajibu huo. Naamini kabisa kabisa kwamba uongozi wa wizara una imani kubwa ya kuyapatia ufumbuzi matatizo hayo ikisaidiwa kwa asilimia 100 na serikali. Kwa msingi huo basi, niwaombe sana Waheshimiwa najua yako mengi mliyoyasema muendelee kutupa muda ili mumpe nafasi Mhe. Waziri aweze kutekeleza vyema haya mengi ambayo mmeyasema.

Mhe. Spika, nataka niseme moja ambalo pia mmelizungumza kwa kina sana hapa, suala la kwa nini wataalamu wa afya wanapewa uteuzi katika uongozi wa vitengo mbali mbali katika Wizara hii ya Afya. Lazima tuelewe moja katika wizara ambayo inahitaji utaalamu mkubwa ni Wizara hii ya Afya, kwa hivyo kutokana na uelewa mkubwa wa sekta hii kwa Mhe. Rais wetu ndio maana anakuwa makini sana katika uteuzi wa nafasi mbali mbali katika sekta hii, ili ziendane na mahitaji halisi na zipate majibu muafaka. Kwa hivyo, uteuzi huo unaotokea si wa kubahatisha ni uteuzi wa makusudi katika kuimarisha huduma bora za afya, kutokana na mazingira wenyewe na mahitaji yenyewe na niseme hakuna utaratibu maalum au *blueprint* iliyowekwa kwa ajili ya namna gani wanaoendesha sekta ya afya, au namna gani wanatoa huduma za afya. Lakini inategemea mazingira na mahitaji na hali halisi inayojitokeza ndio maana uamuzi ufanywe kwa makusudi katika kuimarisha sekta hiyo na kuondoa matatizo mengi ambayo waheshimiwa mmeyasema.

Mhe. Spika, kwa sababu kazi hii ni ya kitaalamu inahitaji sana wataalamu wateuliwe kusaidia kazi hiyo na uteuzi huo wanaopewa wataalamu hauwi kikwazo wa kutokutekeleza majukumu mengine muhimu yanapohitajika katika taaluma zao, na wengi wanaopewa nafasi hizo licha ya kuchaguliwa Wakurugenzi katika idara mbali mbali bado wanatoa ule utaalamu walionao katika kuwahudumia Watanzania wenzao. Nataka niwapongeze sana wale

madaktari ambao wanajitolea kwa hali na mali katika hali ngumu za maisha na katika mzigo mzito wa wajibu wa kazi zao, bado wanaendelea kutoa huduma kwa wananchi. Nawapongeza sana kwa kazi hiyo kubwa wanayoifanya.

Mhe. Spika, naelewa wapo baadhi ya madaktari kwa makusudi kabisa huwa hawapendi kutekeleza wajibu wao ama wanakuwa na maneno ambayo sio mazuri sana wanapotoa huduma kwa wagonjwa. Nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu Mhe. Spika kwamba madaktari wa namna hiyo hawatokuwa na nafasi tena katika kutoa huduma katika hospitali za serikali na Wizara ya Afya kwa jumla. Hatua kali zitachukulia dhidi ya watu wote wale watakaokuwa wanawasumbua wagonjwa au wananchi wanapotaka kupata huduma za afya. Nataka niwahakikishie kwa hili serikali imeamua na mtaona hatua zitakazochukuliwa kupitia Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, napenda niseme hili suala la uteuzi kwa wataalamu sio jambo geni kwa hapa kwetu, limeanza tokea viongozi wetu wa awamu ya mwanzo Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na viongozi wengine waliofuatia mpaka kufikia awamu hii ya saba ya Dkt. Ali Mohamed Shein. Lakini sio hapa kwetu tu ni utaratibu wa kidunia katika taaluma hii. Kwa hivyo, napenda sana Wajumbe wa Baraza letu tukufu waelewe utaratibu unaotumika ni utaratibu wa kawaida na ni utaratibu ambao nia na dhamira yake ni kutengeneza. Kwa hivyo, nawaombeni sana sana Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kwa kiasi kikubwa kumvumilia Mhe. Waziri na wenzake aweze kufanya wajibu wake. Na tumeona kabisa kabisa na mimi napenda nirudie kumpongeza kazi kubwa anayoifanya, hongera sana Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, vile vile wajumbe walieleza hapa kwa uchungu mkubwa suala la usafi katika hospitali zetu hususan Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja. Nataka niwahakikishie dhamira yao na dhamira ya serikali ni moja, nia ya serikali ni kuhakikisha kwamba hospitali ya Mnazi Mmoja inakuwa safi, na hospitali zengine zote zinakuwa safi. Kwa hivyo, hatua madhubuti zitachukuliwa kupitia Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba hospitali zetu ni safi, na kujenga mazingira mazuri sote kuweka mazingira yetu katika hali ya usafi, kwa sababu usafi wenyewe ni afya. Kwa hivyo, hatua mbali mbali zitachukuliwa za vifaa na kinidhamu kuhakikisha kuwa usafi unapewa kipaumbele katika Hospitali yetu Kuu ya Mnazi Mmoja na hospitali nyengine zote, lakini na nchi kwa jumla tumeona jitihada za serikali zinazochukua katika kuhakikisha usafi unakuwepo nchini.

Kwa hivyo, hatua kwa hatua sote kwa pamoja kutokana na jambo lenyewe na ukubwa wake tushirikiane tuhakikishe kwamba tunajenga mazingira mazuri ya

usafi katika hospitali zetu na katika nchi yetu. Naamini kwenye mashirikiano tunaweza kufanya kazi vizuri, na wale ambao watapewa nafasi ya kusimamia jambo hili katika hospitali zetu na wakazembea kufanya wajibu huo hatua kali dhidi yao zitachukuliwa ikiwemo pamoja na kusimamishwa kazi. Kwa hivyo, nataka niwahakikishie Baraza letu tukufu kwamba serikali imejipanga kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha itaimarisha usafi katika hospitali zetu kuu na hospitali nyengine zote.

Aidha, kwenye suala la kutoa huduma kwa muda wa saa zote katika Hospitali yetu Kuu ya Mnazi Mmoja na zile hospitali kuu nyengine. Ni uamuzi wa serikali tayari serikali imefanya maamuzi hayo na Wizara ya Afya itayasimamia ili kuhakikisha kwa saa 24 huduma zinatolewa katika hospitali zetu ili wananchi wazipate huduma hizo kwa wakati wote na hasa pale zinapotokea huduma za dharura, maradhi ya ghafla, ajali na mambo mengine yanapotokea ili shughuli ziweze kufanyika. Kwa hivyo, serikali itahakikisha wakati wote madaktari wa zamu wanakuwepo sehemu za vitengo vya vipimo vinakuwa wazi ikiwemo vipimo vya Maabara, *x-ray* na vyengine ili kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa saa 24.

Nia na dhamira ya serikali ni kuona huduma hizi zinapatikana kwa watu wote kwa wakati ili kuokoa maisha ya watu wetu. Ni jambo lisilofichika kwamba dhamira hii njema imeanzwa tokea kinaundwa Chama cha Afro Shirazi, moja katika sera yake kuu na ya msingi ni kutoa huduma za afya kwa watu wetu bila ya malipo na lilikuwa limetekelezwa hilo baada ya Mapinduzi Matukufu ya 1964 na kiongozi wetu jamadari wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na viongozi wengine, waliofuatia walilisimamia kwa uadilifu mkubwa sana. Ni hali halisi ya uchumi wetu ndio baadhi ya mambo yanakosekana lakini nia na dhamira ya serikali ni kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana kwa upana wake.

Mhe. Spika, lipo tatizo la nidhamu, wapo baadhi ya wafanyakazi na watendaji katika sekta hii ya afya huwa hawawajibiki ipasavyo, na wapo wengine wanaochanganya siasa katika masuala ya kazi. Nataka tuseme bayana kabisa kwamba mtendaji yeyote hususan katika sekta hizi za afya, sekta ambazo wananchi wanazihitaji sana wapate huduma bora na kwa wakati. Mtu yeyote atakayefanya kwa makusudi kabisa ubadhirifu au kuharibu au kuzembea kwa sababu ya dhamira zake za kisiasa nataka niseme wazi mtu huyo hatokuwa na nafasi tena ya kutoa huduma katika hospitali zetu na serikali itafanya uchunguzi wa kina kutafiti, wale wote ambao wanafanya shughuli zao kwa kutokutekeleza wajibu wao ipasavyo na kwa sababu tu wa milango yao ya siasa kwa makusudi wanaharibu kutoa huduma hizo.

Sasa wakati wa kuwavumilia watu wa aina hiyo umekwisha na hatua kali zitachukuliwa zikiwemo za kinidhamu na kisheria kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata huduma bora za afya na wale baadhi ya madaktari na wahudumu ambao wanakuwa hawana maneno mazuri kwa wananchi na kwa wagonjwa wanaofika kupata matibabu vile vile hao wote watashughulikiwa maelekezo hayo Waziri wa Afya anayo na naamini kwa uwezo wake wa kazi na umahiri wake atayatekeleza kivitendo ili kutatua matatizo yote Waheshimiwa ambayo mmeyaonesha wakati mkichangia hoja hii.

Nilikuwa nawaomba sana tumpe nafasi Mhe. Waziri na watendaji wake ili waendelee kutoa huduma bora, waendelee kuyarekebisha makosa yanayojityokeza wasawazishe yale ambayo yote yamekuwa vikwazo katika kutoa huduma hizi. Nia na dhamira ni moja mliyoyaeleza nyinyi ndio ambayo serikali inayafahamu ndio ambayo maelekezo yametoka na ndio ambayo Wizara ya Afya na watendaji na madaktari na wahudumu wako tayari kuyashughulikia.

Nataka nirudie tena kuwapongeza sana madaktari wetu na wahudumu wetu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya wanaofanya wajibu wao kwa kujitolea kwa umakini wa kutoa huduma bora kwa wananchi. Zipo sifa nyingi za watu wa aina hiyo zinazotolewa na wananchi. Kwa hivyo, wanaofanya vizuri lazima tuwapongeze tuwashukuru na kuwatakia kheri na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu katika Mwezi huu mtukufu wa Ramadhan wazidi kuendelea na kazi hiyo, lakini Mwenyezi Mungu awape kheri na mafanikio makubwa katika maisha yao.

Baada ya maelezo yangu hayo Mhe. Spika, naomba niunge mkono kwa asilimia mia moja sekta hii ili Mhe. Waziri apate nafasi ya kwenda kuwatumikia wananchi na niwaombe Wajumbe wenzangu tuipitsihe bajeti hii bila ya buti nyingi, bila ya vikwazo, bila ya maneno mengi ili kumpa nafasi Mhe. Waziri wa afya akatekeleze wajibu wake.

Mhe. Spika, nashukuru sana. Ahsante. (*Makofi*)

Utaratibu

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu kifungu 63, lakini nataka niende katika kifungu 93(2) sijui nikisome au vipi.

Mhe. Spika: Ndio kisome.

Mhe. Machano Othman Said: Nisome eenh! Mhe. Spika, kifungu namba 93(2) kinasema Baraza halitaridhia hoja yoyote yenye madhumuni ya kutoa fedha ila iwe imezingatia katika kamati ya Baraza zima na kama hoja yoyote itatolewa katika Baraza kutaka malipo ya fedha na gharama yoyote kutoka katika mapato ya serikali isipokuwa gharama zinazotokana na dhamana ya serikali, lakini ambazo zitahijali kukubaliwa na Baraza hoja hiyo itapelekwa moja kwa moja katika Kamati ya Baraza zima inayojulikana kwa jina la Kamati ya Matumizi na kuzingatiwa".

Mhe. Mhe. Spika, Nimesimama kuhusu hoja hii kuwa mwenendo wa majibu naona yanaweza kuelekea na kuitahadharisha kwamba serikali sisi Waheshimiwa Wawakilishi wa *back benchers* kazi yetu kubwa ni kuisaidia serikali kwa kuikosoa .....

Mhe. Spika: Mheshimiwa utulivu kidogo tusikie.

Mhe. Machano Othman Said: Tunapoona panataka kupitishwa Matumizi ya Serikali bahati mbaya mimi juzi sikuwahi kuchangia lakini Waheshimiwa wamesema kwamba serikali zaidi Mhe. Rais wizara hii anaipa fedha kwa kiwango kikubwa sana na Baraza linaridhia. Lakini kuna kadhia katika Hospitali ya Mnazi Mmoja inaonekana kama hayaendi sawa. Sisi tunaiomba serikali hebu hata wao kama kamati wanaona tabu waunde kamati waichunguze Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna nini.

Mheshimiwa mwaka jana tulivumilia kulikuwa na ripoti ya mtoto kaliwa na paka Hospitali ya Mnazi Mmoja tukaambiwa kuwa kutakuwa na jopo la wataalamu litafatilia na kuleta ripoti Barazani, ripoti haikuja wazazi wale wameridhia hivyo hivyo shingo upande lakini mtoto kaliwa na paka hatujui tatizo liko wapi.

Sasa tukisema mambo yote yanakwenda salama tu kwa wizara hii tutapitisha bajeti lakini tutakuwa tunajiumiza wenyewe. Mheshimiwa nilikuwa naomba serikali majibu yao yalingane na hali halisi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Machano Othman Said nadhani serikali imesikia kwa sababu baada ya muda sio mrefu wataanza kutoa majibu watazingatia na utaratibu ambao umeutoa hivi punde. Sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Afya ili aje atoe mchango wake. Mhe. Naibu Waziri hata hapo hapo tu haina matatizo, simama.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Awali ya yote naomba nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujualia kuwepo hapa kujadili na kupanga mipango mikubwa na muhimu kwa wizara zetu ikiwemo Wizara hii ya Afya ambayo ni wizara kubwa kongwe muhimu na muhimili mkuu kwa maisha ya wananchi wote.

Mhe. Spika, kwa fursa hii hii uliyonipa naomba pia nichukuwe nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohd Shein kwa uongozi wake mwema na wenye busara na upendo kwa Wazanzibari wote. Uongozi wake umeandelea kutupa heshima kubwa sisi Wazanzibari kuendela kutambulika popote kwamba Zanzibar ni nchi ya amani na wananchi wake ni wananchi wastaarabu.

Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein afya njema amlinde na ampe wepesi katika uongozi wake na shughuli zake kwa ujumla. Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mfupi sasa naomba nichukue nafasi hii kujibu maswali machache ya Wajumbe ambayo nimepangiwa kuyajibu.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nianze kujibu maswali ambayo takribani wamechangiwa au kuulizwa na Wajumbe wako wengi hususan likiwemo suala kubwa la usafi wa Mnazi Mmoja. Ni kweli kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja imekabiliwa na tatizo la usafi, wizara pamoja na uongozi wa Hospital ya Mnazi Mmoja imeliona na kulipangia mikakati mbali mbali kama vile kuwepo kwa ma-*dustbin* katika sehemu mbali mbali kuweka vipeperushi vya maelekezo kwamba usitupe taka ovyo, dumisha usafi kuweko na vipeperushi kwamba ukitumia choo tafadhali weka maji. Lakini yote hayo mara nyingi huwa hayazingatiwi.

Hata hivyo, uongozi wa wizara umegundua tatizo ambalo linachangia kuzorotesha kwa sekta hii ya usafi katika maeneo ya Mnazi Mmoja kuwa ni haya yafuatayo:-

- Ongezeko la wagonjwa katika hospitali hiyo
- Ongezeko la jamaa wanaotembelea wagonjwa
- Ongezeko la majengo na huduma
- Uhaba wa wafanyakazi wa kufanya usafi

- Uhaba wa vitendea kazi na matumizi yasiyo sahihi ya vyoo na maeneo ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, kutokana na changamoto hii uongozi wa Mnazi mmoja unadhamiria kabisa kuajiri kampuni ya usafi na jumla ya kampuni 6 zimeshawasilisha maombi yao.

Mhe. Spika, tumeona tufanye hivi kwa sababu matumaini yoyote ambayo tumeyaona yakiwa yameajiri kampuni hizi za usafi tunaona wamefanikiwa katika suala la usafi. Kwa sababu kampuni zile mara nyingi huwa wanafanya usafi lakini pia wanalinda maeneo yao ya kufanyia usafi, kwa mfano mtu anapoingia chooni basi mtu wa kampuni anakuwa yuko karibu na akitoka tu mtumiaji choo mtu wa kampuni anaingia anasafisha na kutoka.

Lakini pia katika maeneo kama ya Mnazi Mmoja utupaji taka wa ovyo ovyo wao wenyewe huwa wako waangalifu wanaangalia huku na huku na kufanya usafi unaohotajika. Mhe. Spika, tunaahidi Baraza lako hili kwamba suala la uchafu litaishia na sio muda mrefu.

Mhe. Spika, sasa naomba niende kwenye suala ambalo pia limeulizwa na Wajumbe wako wengi lile suala la uchakavu wa majengo ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, ni kweli kwamba majengo yetu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni makongwe na ya muda mrefu na miundo mbinu yake imeshachoka na kuzidiwa na ongezeko la huduma zitolewazo katika majengo hayo. Sekta hii katika awamu tafauti iliweze kufanyiwa matengenezo mbali mbali na baadhi ya maeneo huondoshwa na kuweka miundo mbinu mipya baada ya ile ya zamani. Hata hivyo, jengo linahitaji matengenezo makubwa pamoja na kuweka miundombinu ya kisasa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dr. Ali Mohd Shein imeliona tatizo hilo na kulifuatilia kwa uwezo wake wote ambapo hivi sasa inaendelea na mazungumzo na washirika wetu wa maendeleo wakiwemo *BADEA, Kuwait Fund* na *Saud Fund* kuangalia jinsi ya kushirikiana katika kutekeleza mradi huo wa matengenezo ambayo utagharimu dola takribani milioni thalathini zitahitajika ili kukamilisha matengenezo haya katika Hospitali zetu tatu ikiwemo Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hsopitali ya Mwembeladu na Hospitali ya Mental Kidongo Chekundu. Tutakapokamilisha matengenezo ya Hospitali hizi basi wazara itajipanga ili kuelekeza nguvu za matengenezo katika Hospitali za Pemba.

Mhe. Spika, naingia katika suala ambalo Wajumbe wako wengi pia waliligusia nalo ni upungufu wa wafanyakazi. Mhe. Spika, ni muda mrefu wizara ilikabiliwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi katika maeneo yake mbali mbali. Hata hivyo, tatizo hili limeanza kufunguka kidogo baada ya wizara kuruhusiwa kuajiri wafanyakazi wa kada tafauti. Kuanzia mwezi wa Julai 2016 hadi mwezi wa Juni 2017 wizara imeshaajiri wafanyakazi 104 wa kada mbali mbali na sasa tuna..

Mhe. Spika: Samahani Mheshimiwa Naibu Waziri kidogo.

Waheshimiwa Wajumbe kuanzia Mhe. Naibu Waziri mpaka Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ni sehemu ya majibu ya yale ambayo mlikuwa mmechangia mengi yao ni hayo. Sasa minon'gongo ni mingi nadhani humu kama mnavyojua mna *ECO* mimi pia napaswa kusililiza kwa sababu baadae tutakwenda kwenye vifungu ili nipate msingi wa kile wanachokijibu vile vile.

Sasa mimi sisikii vizuri sujui kama nyinyi mnasikia. Kwa hivyo, msaada mkubwa ni nyinyi kujaribu kuweka hali ya utulivu yaani minongono ipungue ili tuweze kumsikiliza Naibu Waziri na hatimae tuweze kumsiliza Mhe. Waziri kwa majibu yake. Nashukuru sana Waheshimiwa kama mtakuwa na mashirikiano hayo. Tuendelee Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, ni muda mrefu wizara ilikabiliwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi katika maeneo mbali mbali. Hata hivyo, tatizo hili limeanza kufunguka baada ya wizara kuruhusiwa kuajiri wafanyakazi wa kada tafauti. Kuanzia mwezi wa Julai mwaka 2016 hadi mwezi huu tulionao wizara imeshaajiri wafanyakazi 104 wa kada mbali mbali na sasa tunakamilisha mipango wa kuajiri wafanyakazi 325 katika kada tafauti kati ya hao wafanyakazi 100 watawekwa katika nafasi zilizo wazi yaani zile nafasi ambazo wengine walikufa na wengine walistaafu na wafanyakazi 225 wataajiriwa katika nafasi mpya.

Hata hivyo, wizara imepeleka masomoni madaktari bingwa 50 wa fani mbali mbali, kati ya hao madaktari bingwa 13 watarejea katika mwaka huu 2017 na madaktari bingwa 8 watarejea katika mwaka 2018. Kati ya hao wamo wauguzi bingwa yaani *nursing specialist* 10 wa huduma ya mama na mtoto na waunguzi 13 wa fani mbali mbali ambao hao watamaliza masomo yao mwaka 2018 na kuungana na wenzao kutoa huduma bora na kuziba pengo la uhaba uliopo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilichangiwa sana Wajumbe wako ni suala la kuhusu lugha zisizoridhisha kwa wagonjwa. Mhe. Spika, suala hili limelalamikiwa sana na tunakiri kwamba lipo katika hospitali zetu na baadhi ya wafanyakazi ambao hawana maadili ndio ambao wanalishadidia. Wizara imelikemea sana katika hospitali mbali mbali na vituo vyetu maana suala hili haliko katika hospitali ya Mnazi Mmoja tu. Isipokuwa Hospitali ya Mnazi ya Mmoja ni chaka la Hospitali zote yote yanayofanyika pale yanaonekana kwa wepesi zaidi.

Katika miezi sita iliyopita uongozi wa Mnazi Mmoja ulichukuwa hatua ya kupeleka kwenye Kamati ya Maadili wafanyakazi 12 kwa makosa ya nidhamu ya kazi zao na wapo ambao kamati iliwafutia usajili na wengine kupewa onyo kali. Katokana na kujirudia rudia kwa tabia hiyo uongozi wa Hospitali umechukua hatua zifuatazo:-

(1) Kuanzishwa kwa kitengo cha huduma kwa mteja ambacho kitakuwa na sehemu ya huduma ya jamii na sehemu ya uhusiano na jamii na sehemu ya huduma ya kisheria na rufaa za wagonjwa. Kitengo hichi kipo tayari na kimepatiwa wafanyakazi kwa ajili ya kuanza kuimarika.

(2) Kufanya mabadiliko makubwa katika mfumo wa uongozi wa Mnazi Mmoja.

(3) Kuimarisha kamati ya nidhamu ya Hospitali.

(4) Kusimamia uvaaji wa vitambulisho kwa wafanyakazi wote.

Mhe. Spika, naomba kuwahakikishiwa Wajumbe wa Baraza lako kwamba wizara itaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kisheria ili kuhakikisha nidhamu kwa wafanyakazi wetu inarejea.

Mhe. Spika, malalamiko mengine ambayo Wajumbe wako waliyachangia kwa wingi ni lalamiko la walinzi katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, imeshapokea malalamiko hayo kwa muda mrefu na kuyafanyika kazi kuzungumza na walinzi hawa na kuwataka wawe na lugha nzuri kwa wagonjwa na watumiaji wa maeneo ya hospitali husika. Lakini bado tunaendelea kupata malalamiko na ushahidi mkubwa ni juzi katika michango ya Wajumbe wako ni michango mingi ilielekezwa kwa walinzi pia.

Tunalowaahidi Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba walinzi wale tumejaza nao mkataba na mkataba mtu anaweza kuuvunja wakati wowote ambao wanaona

wale wahafati mkataba au wanakiuka malengo ya mkataba. Kwa hiyo, tunaahidi kwamba wakati wowote kuanzia sasa tuko tayari kuvunja mkataba nao kama watakuwa hawatofata maadili na kama wataendelea kuwanyanyasa na kuwasumbua wagonjwa na wananchi wetu. Mhe. Spika, hili tumelipokea tumelifanyia uchunguzi na linakubalika na hatua zitachukuliwa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa sana na Wajumbe wako ni kuhusu banda la kupumzikia wagonjwa na wananchi wanaopeleka wagonjwa wao. Ni kweli kwamba katika bajeti ya mwaka 2016 wizara iliahidi kutafuta mfadhili ya kujenga hilo la kupumzikia katika bustani ilioko mbele ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wizara inaendelea kuchukua hatua za kujiandaa ili kupata jengo lenye ubora na viwango hasa kutokana na idadi kubwa ya watu ambao watalitumia jengo hilo.

Hata hivyo, kwa hatua za awali imeweka sehemu ya kupumzikia jamaa na wagonjwa na muda mfupi tunategemea kujenga vyoo kwa ajili ya matumizi ya wahusika hao. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba niingie kujibu maswali ya mtu mmoja mmoja ambayo nitaanza na suali alilouliza Mhe. Mwantatu Mbaraka Mwakilishi wa Viti Maalumu kusini Unguja.

Mhe. Spika, Mhe. Mwantatu Mbaraka aliuliza wananchi wanaotembelea wagonjwa kukaa nje bila ya kuwepo maeneo maalum pia walinzi wanawasumbua kwa kutowapitisha kwenda kuwaangalia wagonjwa wao. Pia anataka ufafanuzi wa yale mabenchi yaliyojengwa yana madhumuni gani.

Mimi naomba nimjibu Mhe. Mwantatu Mbaraka kwamba hospitali zinazeweza kufanya shughuli zake kwa ufanisi zimejiwekea utaratibu kwa wananchi kuwatembelea wagonjwa hao, utaratibu huu ni kwa hospitali zote duniani muda wa kuwaona wagonjwa kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ni saa 12 asubuhi mpaka saa 1 asubuhi saa 7 mchana mpaka saa 8 mchana na saa 10 jioni mpaka saa 12:00. Wananchi kuwaona wagonjwa nje ya wakati huo ni lazima kuwe na makubaliano kati ya wahudumu na wanao muhudumia mgonjwa na jamaa zao.

Ndani ya hospitali ya Mnazi Mmoja hakuna nafasi ya kujenga banda la wananchi kukaa kusubiri kuwaona wagonjwa wao na pia mazingira ya ndani ya hospitali sio salama kwa wananchi kukaa kwa muda mrefu wakisubiri wakati wa kuwaona wagonjwa wao. Inashauriwa wananchi wafike wakati wa kuwaangalia wagonjwa hao ikisha waondoke wakiwa salama.

Sehemu ya nje ya uzio wa hospitali ziko chini ya mamlaka yetu. Wizara imeanza kujiandaa kujenga vikalio kwa ajili ya jamaa za wagonjwa kupumzikia

na bado inaendelea kuzungumza na wafadhili wengine, ili kuona namna tutakavyoweze kujenga mabanda katika eneo la bustani.

Mhe. Spika, ma-*bench* ya bustani pembeni zimejengwa ili watoto wadogo wagonjwa ambao wamepata kupumzika katika vitanda vya hospitali ya Mnazi Mmoja wapate mahali pa kucheza. Watoto wale wakipata nafuu vitandani ya kuumwa, kawaida ya mtoto anapenda kucheza na ndipo unapomjua kwamba huyu hali yake sasa inaendelea kuwa nzuri. Kwa hivyo, ma- *bench* yale ambayo mnayaona pale nje lengo na madhumuni yake ni kwa ajili ya watoto ambao wako *cot word* wamelazwa, wanapopata nafuu watome nje na wazee wao, watoto wachezecheze pale na wazee wanafarijika na hata madaktari ndio watakapoona mtoto huyu sasa yuko tayari kurudi nyumbani. Sehemu ile Mhe. Spika, haikutengenezwa au haikutayarishwa kwa ajili ya kukaa *relative*.

Mhe. Spika, naomba sasa niende kwenye swali ambalo aliliuliza Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kwamba kwa nini *generator* halikufungwa licha ya kuletwa kwa muda mrefu. Mhe. Spika, ni kweli tangu *generator* lile liletwa huu ni takribani mwezi wa nne, uchelewaji huu wa kulifungua *generator* lile unatokana na kutafuta kampuni maalum ambayo inaaminika kushughulika na *generator* lile. *Generator* ukiliangalia ni *generator* kubwa lenye thamani kubwa, sio vizuri kutafuta tu kampuni au kukurupuka kuweka kampuni yeyote wakatujengea, lakini likawa jengo halina ubora na matokeo yake baada ya muda mfupi tukaanza kulalamika kwamba *generator* limekosa jengo. Kwa hivyo, kuchelewa huku Mhe. Spika, ni kwamba tunatafuta kampuni ambayo itafanyakazi ile kwa ufanisi zaidi. Katika kipindi hiki kuna kampuni ambazo zimejitokeza na hivi tumo katika kuzungumza nao, ili tuone katika hizi ni kampuni gani ambayo tutaikamata kutumalizia suala lile. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niendelee kwenye suala la Abdalla Maulid Diwani, alisema kwamba chumba cha kulazia maiti *mortuary* ni kibovu na hakiridhishi hakikidhi haja. Mhe. Spika, kwanza nataka nithibitishe kwamba waheshimiwa wenzagu ambao ni wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Spika, kwa kweli ni watafiti sana na wanafanyakazi ya kuangalia sehemu zote kwa manufaa ya wananchi.

Mhe. Spika, ni kweli ni lazima nikiri kwamba hali ya jengo letu haliridhishi ni chakavu na pia ni dogo. Pia kutokana na kuwa hospitali ya Mnazi Mmoja ni hospitali ya kufundisha madaktari na kada nyengine za afya, basi kuna haja ya kukipanua kitengo hicho kwa kukiongezea zana ili wanafunzi wa fani ya udaktari waweze kufundishwa mambo mbali mbali. Wizara inatafuta nafasi ya

kutosha ya kujenga chumba cha kisasa cha kuhifadhia maiti kitakachoweza kukidhi mahitaji kwa maisha yetu ya sasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba sasa niende kwenye swali la Mhe. Suleiman Sarahan Said, anasema je, jengo la macho Mikunguni nafasi haitoshi wizara mnatuambia nini. Jibu la Mhe. Suleiman Sarahan ni kwamba hospitali hiyo kweli ni ndogo na haikidhi haja ya kuweko kwa kitengo cha hospitali ya macho. Hospitali ya Macho ilihamia kule Mikunguni kwa dharura tu. Hivi sasa matayarisho ya ukarabati mkubwa wa hospitali ya macho iliopo Mnazi Mmoja yameshakamilika na ukarabati utaanza wakati wowote kuanzia sasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niende kwenye swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliuliza *AC* za *ICU* kongwe zilikuwa hazifanyikazi na za *ICU* mpya kwa sababu ya kupigwa na radi. Mhe. Spika, hivi sasa *AC* hizo zimekarabatiwa na kununuliwa nyengine mpya, kwa hivyo wizara inajipanga kuweka mfumo wa kujikinga na radi ili isilete madhara katika *AC* hizo.

Mhe. Spika, swali la pili la Mhe Jaku Hashim anasema wodi ya watoto wanaoungua moto yaani *cotword B* haitoshi. Mhe. Spika, napenda nikiri kwamba kweli wodi ya watoto *cotword* ya kuungua moto haitoshi ina vitanda vinne tu na mahitaji yake ni makubwa kwa sababu watoto wanaopata madhara haya ni wengi hususan hasa katika kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhani.

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Spika, Swali langu Hospitali ya Bumbwisudi ilifunguliwa na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Riziki Juma. Lakini mpaka sasa haina dawa ya aina yoyote. Je, ni lini hospital hii itapatiwa dawa ili wananchi wasisumbuke kufuata dawa maeneo ya mbali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kuzaliwa na wamezaliwa hapo hapo kwetu na pia wapo wanaofariki bila ya idara husika kuhusishwa. Hapa tunakosa takwim sahihi pamoja na kuwa tunao Masheha na viongozi katika vijiji. Nashauri na njia nyengine ya kusaidia kitengo hichi.

Naipongeza juhudi za serikali kuhamasisha rushwa isiweze kupata nafasi katika sekta za serikali zikiwemo mahakama zetu. Kwa kweli mabadiliko yameanza kuonekana.

Naunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mungu mwingi wa Rehema kuweza kunipa uwezo wa kuchangia yale niliyonayo.

Mhe. Waziri kwanza naanza na kitengo cha huduma za hospitali za watu binafsi. Mhe. Waziri nakuomba sana kamati yako ya kufatilia wafanye kazi ipasavyo. Mhe. Waziri mimi mwenyewe nimeshuhudia kupewa majibu ya kutisha eti nina maradhi ya moyo nikapewa dawa mkoba mzima. Matokeo yake nikaanza kuzidi maradhi kwa madawa niliyopewa nikaenda Bara kupima sina sukari wala moyo haya ningeendelea kula dawa zile ningepata maradhi mengine.

Nakuomba sana Mheshimiwa ufatilie. Mhe. Spika, Mhe. Waziri awe makini la si hivyo watatumaliza hasa sisi wanyonge.

Mhe. Waziri nataka tena kuchangia Kitengo cha Mama Wajawazito. Mhe. Waziri tunamshukuru Mhe. Waziri wetu wa Serikali ya Mapinduzi kuwajali kina mama. Lakini Mhe. Waziri watendaji wako wanatoza pesa nyingi. Tunakumbuka Mhe. Rais alisema magamba ya kupimia kwa wajawazito ni bure. Sasa kwa nini *clinic* ya Chumbuni mpaka uwe na shilingi elfu moja ndio upate huduma hiyo. Je, Mhe. Waziri wale kinamama wasiokuwa na uwezo wanaenda wapi? Nakuomba sana Mhe. Waziri wasaidiwe sana kinamama wasio kuwa na uwezo.

Nakushukuru sana Mhe. Waziri naomba wanaotaabika kupata huduma hii. Naunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Waziri mimi naanza na Hospitali ya Mnazi Mmoja sehemu ya kina mama. Ile sehemu wanapoekwa kina mama ambao wamejifungua kwa kweli imekuwa ndogo utakuta kitanda watu watatu na mpaka chini kwenye magodoro mmejaa.

Mhe. Waziri naiomba serikali ile sehemu ya zamani iliokuwa inatumika kwa kina mama ifanyiwe matengenezo ili baadhi ya kina mama wanaojifungua wakae sehemu ili upungue msongamano kule kwenye wodi ya wazazi.

Mhe. Spika, aidha kina mama wanapokwenda kujifungua wanalipa pesa wengine shilingi 5,000/ hadi 7,000 hakuna idadi maalum za vipimo na wakati washajifungua wanatakiwa watoe pesa nyengine kwa ajili ya kupima damu na mama hapewi ruhusa kama hajalipa pesa hizo.

Mhe. Spika, naomba sana wizara yako iangalie vitu vidogo vidogo kama hivyo viwepo kwani wananchi wetu wengi ni wanyonge.

Mhe. Spika, wafanyakazi wa benki ya damu sehemu ya maabara wanafanya kazi mpaka saa mbili usiku lakini cha kusikitisha tokea Januari hawajalipwa *over time* yao.

Mhe. Waziri nitaomba sana unambie watumishi hawa lini watalipwa pesa zao za *over time*. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Hospitali ya Mnazi Mmoja katika lengo kuu la serikali ni kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa na wananchi kuendelea kupata huduma mbali mbali katika vituo vyetu vya Wilaya na Mikoa na pale inapoonekana mgonjwa ipo haja ya kupata huduma kubwa zaidi za kitaalamu ndio tuende katika Hospitali ya Mnazi mmoja. Kwa mantiki hiyo namuomba sana Mhe. Waziri kushirikiana na Makamu wa Pili wa Rais kutuwekea kituo cha Afya katika Baraza la Wawakilishi kiwahudumie Waheshimiwa pamoja na watendaji wote wa Baraza.

Pia nampongeza sana Mhe. Rais kwa juhudi kubwa ya kuhakikisha anasaidia wizara hii ambayo ndiyo inayoimarisha maisha ya wananchi wote wa Zanzibar. Mwenyezi Mungu amjaalie Dr. Ali Mohammed Shein kheri za dunia na akhera.

Naomba niwaombe sana Wajumbe wenzangu kupitia dhiki kubwa inayowapata wagonjwa wetu kukosekana kwa maji katika Hospitali ya Mnazi Mmoja tusamehe posho yetu ya siku moja ikatatue hili.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, naomba kuchangia kwa maandishi Hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya kwa sababu sikupata kumaliza mchango wangu kwa dakika 10 nilizopewa kuchangia moja kwa moja.

Programu: Utawala na Uendeshaji:

Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna maeneo mengi katika idara zako zina wafanyakazi wake maalum wanaostahiki kulipwa posho zao, linalosikitisha kwa muda mrefu sasa hawajalipwa posho zinazostahiki na kupelekea malalamiko na kupunguza kasi ya uwajibikaji.

Natoa shilingi katika fungu la Utawala na Uendeshaji mpaka nipate majibu ya wafanyakazi hao. Kwa nini wizara kupitia Hospitali ya Mnazi Mmoja hawajawapatiwa fedha zao ambazo ni haki yao ya msingi na kisheria. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti nianze kwa Huduma za Kinga Dhidi ya Ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake za kudhibiti ueneaji wa maradhi ya Ukimwi kwa kutoa elimu inayohusiana na mardhi hayo. Kwa kuwa kuna kliniki 12 tu kwa Unguja na Pemba zinazotoa huduma za kinga na tiba kwa wanaoishi na virusi vya Ukimwi, ni vyema wizara ikazidi kufanya jitihada za kuongeza vituo kwa Unguja na Pemba ili huduma za kinga na tiba kwa wanaoishi na virusi vya ukimwi zikaboreka zaidi na hatimae kufanikiwa katika kupambana na udhibiti kwa ueneaji wa virusi vya ukimwi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Huduma za Usimamizi wa Hopsitali Binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuipongeza Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi kwa kusimamia ipasavyo uanzishaji na uendeshaji wa Hopsitali na vituo vya afya binafsi. Pamoja na hayo, kuzikagua na kuzipatia maelekezo hospitali binafsi juu ya utoaji wa huduma za afya kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo.

Ni vyema Wizara ya Afya ikazidisha jitihada ya kuzifanyia ukaguzi hospitali binafsi mara kwa mara ili kulinda ustawi mzuri wa afya kwa wananchi wetu na pale ambapo hospitali binafsi hizo zitapoteza sifa za kuendelea kutoa huduma, ni vyema hospitali hizo zikafungwa bila ya kuoneana haya na wamiliki wa hospitali hizo adhabu na hatua kali zichukuliwe kwa wale ambao wataendesha hospitali hizo bila ya kiwango.

Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Ame Haji Ali: Mhe. Waziri kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali ya Mapinduzi kwa juhudi kubwa zinazizochukuliwa katika kuboresha huduma za afya nchini.

Mhe. Waziri pamoja na juhudi hizi bado zipo changamoto ambazo zinahitaji kusimamiwa kwa ukaribu zaidi:-

- ✓ Uhaba wa Madaktari
- ✓ Uchakavu wa majengo
- ✓ Upatikanaji wa madawa

- ✓ Kuendelea kuwapa darasa wahudumu wetu kutoa lugha nzuri wanapohudumia wagonjwa.

Mhe. Waziri pamoja na hayo kuna maeneo ambayo nahitaji majibu ya wizara.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipofanya ziara Jimbo la Nungwi alijionea uchakavu mkubwa katika baadhi ya vituo. Vituo hivyo ni kituo cha Afya cha Tazari, kituo ambacho paa lake ni bovu kiasi ambacho linasababisha huduma kutofanyika vizuri.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alisema wizara imo mbioni kuomba wafadhili kuja kuliezeka. Je, jambo hili limefikia wapi.

Tulipotembelea kituo cha Kidoti pia tulijionea ubovu katika kituo hicho pia Mhe. Naibu Waziri alituahidi zipo juhudi za kupatiwa mfadhili kituo hicho. Je, jambo hili lipo au laa.

Jengine Mhe. Spika, naomba kuongezewa madaktari katika vituo vya Tazari Kidoti. Jengine Mhe. Waziri naomba pia wizara ilizingatie jengo la nyumba ya daktari iliopo Tazari nyumba ambayo kwa sasa inahitaji kuezekwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naendelea kuipongeza wizara kwa kazi kubwa inayofanya katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mwisho Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nungwi naunga mkono hoja hii. Ahsante.

Mhe. Yussuf Hassan Idd: Mhe. Spika, kwanza niwapongeze Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji na wafanyakazi wa wizara hii kwa kazi ngumu wanayoifanya ya kuweka afya zetu vizuri.

Pili niipongeze wazara kwa kuanza huduma ya utibabu wa figo hapa nyumbani katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Tunaiomba wizara huduma hii iwe endelevu ili wale wote wanaotaka huduma hii basi waipate na matokeo ya ufanisi kwa mgonjwa wa mwanzo ili wananchi wetu wapate taarifa kamili.

Naipongeza wizara kwa kuifanyia marekebisho nyumba ya madaktari katika kituo cha Fuoni pamoja na kufanya utanuzi wa kituo hicho, kituo kwa sasa kimezidiwa sana hasa kwa huduma nzuri wanazozitoa kwa wananchi.

Naiomba wizara iwapatie mafuta kila mwezi kwa ajili ya huduma ya *ambulance* pamoja na kuwapatia vifulio vya kutilia dawa badala ya magezeti wanayotumia hivi sasa. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri wa Muungano Mhe. Luhanga Mpina alifanya ziara katika kituo hicho. Je, wizara imechukuwa hatua gani hadi sasa katika kutekeleza ahadi hiyo.

Wizara ina mpango gani wa kudhibiti ongezeko la wagonjwa na maradhi yasiyoambukiza ambapo kila mwezi kuna ongezeko la wagonjwa wapya.

Naiomba wizara itoe takwimu ya maradhi ya ukimwi kwa sasa, tatizo hili lipo kwa asilimia ngapi kwa sababu naona ile hewe hewe imepungua kama tatizo hili halipo.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante.

Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Waziri wa Afya nashauri tufanye bidii za haraka tujenge banda la kukaa watu wenye wagonjwa na wanaosubiri muda wa kutizama wagonjwa. Wale wafanyakazi wa kambi za maradhi ya kipindupindu tuhakikishe tunawalipa posho zao vizuri bila kuchelewa ili tuwape moyo wafanyakazi wa bidii.

Tuongeze elimu ya usafi na kuchimba vyoo kwenye maeneo yanayopata maradhi ya kipindupindu. Ahsante.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara yake. Mhe. Naibu Spika, nitazungumzia huduma za Afya ukurasa wa 15-16 za afya ya Uzazi na Mtoto.

Mhe. Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mhe. Waziri ametueleza kuwa kuna jumla ya wazazi 20.893 walijifungua katika Hospitali na vituo vya Afya kwa njia ya kawaida na njia ya upasuaji na vifo vilivyotokea na wazazi 27 na hakuna takwimu ya watoto wachanga (vifo).

Ukiangalia idadi ya wajawazito waliojifungua na idadi ya watoto waliozaliwa hai ni tafauti.

Mhe. Naibu Spika, naomba mchanganuo ufuatao.

- Nataka kufahamu idadi halisi ya vifo vya watoto wachanga 2016-2017.

- Nataka mchanganuoa wa idadi ya wajawazito waliojifungua na idadi ya watoto waliozaliwa hai.

Mhe. Naibu Spika, Ahsante sana naunga mkono hoja asilimia 95 na 5 mpaka nitakapopata ufafanuzi.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Spika, kwanza awali ya yote napenda nichukuwe nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wetu mpendwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake mahiri katika kuiongoza Zanzibar, na kuwa mstari wa mbele kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020, ambayo inatekelezwa vyema. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, umri mrefu na ampe nguvu ya kuwa na busara na hekima.

Mhe. Spika, binafsi napongeza juhudi zinazofanywa na wizara hii chini ya uongozi wa Waziri, Naibu waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Mkurugenzi Mkuu, Afisa Mdhamini Pemba, pamoja na wakuu wa Taasisi zote ndani ya wizara hii. Kwa juhudi zao ambazo zinaleta matumaini ya kuweza kutekeleza ilani ya CCM 2015-2020. Timu hii inaonesha uzalendo wa dhati kwa kustahamili changamoto mbali mbali na kuzipatia ufumbuzi wa changamoto hizo kwa vile Mkoa wa Mjini Magharibi una idadi kubwa ya wakaazi kwa mujibu wa sensa ya 2012 Mkoa huu una dadi ya 46% ya idadi ya watu wa Zanzibar.

Wizara ya Afya iangalie ongezeko la watu hilo na kuona vituo vya afya vya Mkoa huu hususan wilaya za Maghaaribi A na B vitaelemewa na wagonjwa. Hivyo, ijiweke tayari kuwa dawa pamoja na wafanyakazi katika vituo hivyo.

Mhe. Spika, suala la Hospitali Binafsi naiomba serikali waliangalie suala hili na sheria hii ya Hospitali Binafsi iangaliwe upya. Kwani Hospitali hizi zote wafanyakazi wake pamoja na wadaktari wake wengi kati yao ni wafanyakazi wa kutoka hospitali zetu za serikali.

Kuhusu utendaji kazi katika hospitali zetu Unguja na Pemba wizara ifanye kazi ya kuangalia tabia, uzalendo na imani za baadhi ya wafanyakazi. Inaonekana hawana uzalendo au hata pengine wanachanganya kazi na siasa na ndio maana baadhi yao wanakua na lugha za kuudhi kwa wananchi wanaokwenda kupata huduma katika hospitali zetu na kupelekea lawama kwa wafanyakazi ambao wana tabia njema pamoja na kupatikana lawama kwa wizara yenyewe pamoja na serikali kwa jumla. Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hotuba hii asilimia mia. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kuchukuwa nafasi hii kukupongeza wewe na wafanyakazi wako wote.

Pili nawatakia kila la kheri katika bajeti yenu hii pamoja kwamba kwa mtizamo mtakuwa hamna shida ila nazidi kuwaombea Mungu azidi kuwapa njia nyepesi.

Tatu Mheshimiwa mimi nilikuwa naomba zile nafasi ambazo ziko wazi za matroni hasa Pemba ambazo watu wake wameshafariki zamani na bado ziko wazi Mheshimiwa tungeomba waajiriwe hasa ukizingatia hawa wameshatangulia mbele ya haki.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe. Waziri Micheweni ni moja ya Hospitali ya kutoa huduma kwa jamii. Lakini leo katika sehemu ya *theatre* haijamalizika ili kuondoa matatizo ya wajawazito ambao wamefika pale kwa kujifungua. Mhe. Waziri ni lini *theatre* ile itamalizika na kiasi gani cha pesa kinachohitajika kumaliza tatizo hilo.

Mhe. Spika, waziri naipongeza sekta ya afya kwa kujenga majengo ya kituo ili kuondosha msongamano wa kutoa huduma katika hospitali ya Micheweni Mhe. Waziri katika Shehia ya Sizini kuna kituo cha afya ni mda mrefu sasa halijamalizika ni lini sasa kituo kile kitamalizika na kutoa huduma. Pia kwa kupitia bajeti hii wafanyakazi au madaktari wangapi tutapatiwa wilaya ya Micheweni.

Mhe. Waziri Rais wa Zanzibar Dr Ali Mohd Shein alitoa agizo kama mpite kwenye Vituo vya kuuzia dawa pamoja na maduka la chakula ambapo wananchi wanauza dawa ili kuondosha bei zisizo nzuri. Lakini pia kucheki dawa zilizopitiwa na muda ni maduka mangapi mmefanya na *pharmacy* ngapi mmezigundua kutokukidhi haja hiyo.

Mhe. Spika, nimeona kuwa wafanyabiashara wa Nyama wamepatiwa elimu kuhusu uchinjaji na uhifadhi wa nyama ili mlaji asiathirike. Mhe. Waziri vipi kuhusu wauzaji wa samaki lakini hata bandarini maeneo hayo ni machafu hasa. Lini wizara itatoa kauli juu ya afya ya wauzaji wa samaki.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba kutoa mchango wangu wa maandishi kwa Waziri wa Afya. Nikianza na kumshukuru *Allah* aliyetuumba.

Aidha kwa naiba ya wananchi wa Jimbo la Amani wenye imani endelevu ya dhati kwangu katika kuwasilisha na kuchangia maoni yao. Awali ya yote katika mchango huu naunga mkono hoja ya hotuba hii ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa asilimia 100%.

Mhe. Naibu Spika, nawapongeza sana na kumuunga mkono ndani ya moyo wangu Mhe. Rais Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein kwa jitihada zake anazozichukuwa katika kuhakikisha wananchi wake wote wanapata huduma bora za afya hapa nchini.

Aidha naunga mkono jitihada zake za kuimairisha kukuza na kuongeza miundombinu na rasilimali katika sekta ya afya. Nazipongeza sana juhudi za serikali zinazosimamiwa na Mhe. waziri wa Afya Mhe. Mahamoud Thabit Kombo katika kuhakikisha huduma ya afya zinatolewa kwa ubora na zinapatikana kwa urahisi bila ya usumbufu kwa wagonjwa na wajenga afya.

Mhe. Spika, miongoni mwa wizara kuu tatu maana katika nchi yoyote ile ikiwemo yetu basi ni wizara hii. Wizara hivi sasa imejipatia madaktari kituo cha afya cha Sebleni na kukiidhinisha kutoa huduma kwa masaa 24 kwa mama zetu waja wazito ambao kwa sasa tayari wameanza kupata huduma hizo hapo kwenye jimbo langu la Amani.

Nashukuru sana kwa mashirikiano ya dhati kwa chama changu cha CCM kupitia Mhe. Mbunge Mussa Hassan Mussa, mimi Mwakilishi, Madiwani na Uongozi wa Wilaya na Jimbo kwa jumla kwa kufanikisha michango yao na kuchangia kwa kiasi kikubwa kusaidia serikali kufanikisha hilo katika ujenzi wa kituo hicho cha wazazi na bodi yake.

Mhe. Naibu Spika, kuwepo kwa huduma za madawa za mama wajawazito wa Jimbo la Amani ni chachu ya kuungwa mkono bajeti hii. Kwa mara nyengine kwa niaba ya uongozi wa Jimbo la Amani Mhe. Mbunge Madiwani na Mwakilishi wataendeleza kurahisisha mahitaji ya wananchi katika kuwapatia afya bora ili wakabili shughuli zao za ile siku ya kujiletea pato lao na kujenga vyema uchumi wa nchi hii.

Tunaomba bajeti hii ipitishwe bila ya pingamizi ili tuungane na jamii kutekeleza matakwa ya kuwapatia huduma wanazozitarajia. Ahsante naunga mkono hoja.

Mhe. Dr. Makame Ali Ussi: Mhe. Naibu Spika, huduma ya afya ya mazingira ina jukumu la kukinga jamii isipate maradhi yanayoweza kutokea kwenye mazingira.

Naipongeza wizara kwa bidii inayochukuwa kushughulikia suala la maji safi na salama, kutoa elimu ya afya kuwakagua wanaotoa huduma za vyakula na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuchagua mazingira kwa kuchoma taka, hususan kwenye hospitali yetu bado linaendelea, hivyo kusababisha kero na malalamiko kwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hospitali hizo. Wengine huchoma taka hizo usiku ili wasipate malalamiko. Uchomaji huu wa taka za hospitali mbali na harufu mbaya ni hatari kwa maisha ya wananchi. Moshi wenye sumu na majivu wanaweza kuzalisha magonjwa ya ajabu ambayo yanaweza kuwa si rahisi kuyatibu.

Kwa mantiki hii nashauri sana utaratibu wa uendeshaji kwa jumla ikiwemo huo wa uchomaji wa taka ushughulikiwe ipasavyo ili kuepuka janga la maradhi linaloweza kutokea kutokana na uchomaji huo. Mfano Hospitali ya Al-Rahma, baada ya kuona wananchi wanalalamika sana wameamua kwa makusudi kuchoma taka hizo usiku na juu ya ghorofa ya hospitali hii. Utaratibu huu ni mbaya zaidi kwani wananchi wengi wanaokaa mwenye maeneo hayo wakiwa wamepumzika na hivyo kusababisha harufu mbaya, moshi na majibu ni kuwaathiri zaidi.

Ni vizuri watafute maeneo ya kuchoma takataka zao mbali na maeneo ya makaazi. Hasa uchomaji wa karatasi usiruhusiwe kwani majivu hupeperuka na kuchafua mazingira yote ya karibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Nashukuru sana kwa uwasilishaji wako na ninakupongeza kwa hotuba yako.

Naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi kuwa naunga mkono hotuba maelezo na bajeti yako iliyopendelezwa na kuombwa kwa asilimia mia.

Pili maoni yangu suala la maji na ZAWA linatugusa sote pamoja na sekta ya afya. Naomba hili pamoja na mradi wa 92 za India usimamie wewe mwenyewe.

Naomba kuunga mkono.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Spika, naomba ipatiwe gari hospitali ya Vitongoji kwa vile gari lilioko kwa sasa ni bovu tena kati ya gari mbili mpya zilizoletwa Pemba moja iletwe Hospitali vya Vitongoji. Mhe. Waziri nakuomba kukifanyia matengenezo Kituo cha Afya cha Ole, kwa sasa kinahitaji kuezekwa chote kinavuja mapaa yake ni mabovu sana. Mhe. Waziri nakuomba kujenga Kituo kipya cha Afya cha Uwandani Vitongoji, kiliopo sasa hakifai kuwa Kituo cha Afya ni kama nyumba ya mtu binafsi. Mhe.

Jengine Mhe. Spika, Waziri nakuomba sana kusimamia nidhamu ni mbaya sana wauguzi wa Hospitali hiyo asilimia 80 maeneo yao ni machafu kwa wagonjwa hutoa maneno machafu hasa wanapotambua kuwa mgonjwa ni mfuasi wa chama Tawala huyu hutolewa maneno hata kama hana kosa.

Mhe. Spika, mwisho naunga mkono hoja.

Mhe. Maryam Thani Juma: Mhe. Spika, kwanza naipongeza wizara hii ya afya kwa jitihada zao wanazozionesha kupitia kwa Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Dr Ali Mohd Shein.

Mhe. Spika, waziri kwenye kitabu chake cha bajeti nashukuru sana ameeleza upanuzi wa vituo vya kutoa huduma za uzazi na watoto wachanga, katika vituo hivyo sita kikiwemo kitu changu cha Junguni na uwekaji wa vitendea kazi ikiwa ni sehemu ya kuzalisha viwanda na jiko la kutakasa vifaa.

Naomba unieleze je zana hizo tayari vishawekwa katika hospitali hiyo ya Junguni? Na kwa kuwa hospitali hii ya Junguni ina wafanyakazi kidogo na kati ya hao wafanyakazi wawili ni wa siku nyingi wamechoka na wanahitaji kupumzika kwa kazi nyingi. Je, wizara ina mpango gani wa kuwapumzisha hawa na kuwaajiri wengine wa hospitali kongwe na hichi cha huduma ya uzazi na watoto wachanga?

Niende kwenye Hospitali ya Wete, Hospitali hii haina *x-ray* watu wanahangaika kwenda Micheweni, hili ni tatizo kwa hospitali kubwa ile.

Je, ni sababu gani hata *x-ray* ya Wete kuwa haipo na kuwepo Micheweni na kama ipo ni sababu gani hata isitumike na kufanya watu waende Micheweni?

Naomba sana Mhe. Waziri uone matatizo ya Hospitali zetu za vijijini kama Hospitali ya Ukunjwi, Fundo na Junguni matatizo ni mengi kwa hospitali hizi uje uzikague. Naomba sana mwisho naunga mkono hotuba hii asilimia 100 ukinijibu haya niliyoyauliza.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, kuhusu *x-ray* ya Hospitali ni mbovu naomba kujua nini tatizo. Lakini hata msomaji wa *x-ray* ni wawili tu kulikoni kuwe na muda au siku za kusoma *x-ray*, wakati matibabu yanahitajika kila siku.

Tatizo la maji katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni tatizo kulikoni wakati visima na *pump* zipo huoni kuwa hili ni janga linaloundwa kwa makusudi kwa kutiwa ubaya baina ya wananchi na serikali yao. Ipo *B/C* ya homa ya Ini ni tatizo kubwa kwani hata wananchi wanakosa elimu ya maradhi haya kwani ni maradhi thakili kuliko *AIDS* hata Malaria kwa tunavyojua. Naomba unieleweshe kwa tatizo hili.

Kuhusu kipimo *ECO* vipi hata hichi ni shida, *liquid profile* na vinginevyo haiwezekani kwa hospitali ya Mnazi Mmoja iwe tatizo kiasi waende hospitali za nje.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Waziri naomba nikupongeze kwa dhati pamoja na watendaji wako kwa kazi nzuri ambazo mmezifanya.

Nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuweka biashara huru na pia nikupongeze wewe kwa kuteua Bodi ya Madawa na Vipodozi.

Kuna baadhi ya bidhaa ambazo wanaingiza wafanyabiashara wetu hasa mafuta ya kupikia ya geleni na vidoo, mafuta haya yanahitaji uchunguzi wa kina kutokana na matatizo yanayojitokeza kwa wananchi wetu na kuwaepusha na maradhi yasiyo na lazima kwani inasemekana yanaua kwa ufatiliaji wa wananchi wetu.

Mhe. Waziri pia naomba nikupongeze kwa jitihada zako kwa Hospitali ya Mbweni lakini kuna tatizo la wananchi kupoteza maisha kutokana na kutokuwepo *theatre* na tayari imeshayaanzisha. Naomba uendelee na jitihada ya kumalizia ili tuwasaidie wananchi wetu.

Mhe. Spika, Elimu ya Afya ni huduma muhimu sana kwa wakaazi wetu. Lakini inaonekana kuna baadhi ya wakaazi wetu kuwepo kwa ukiukwaji wa sheria kwa unyanyasaji na uchelewaji wa kufika kazini kwa wakati na kupelekea kinamama na watoto kupata tabu. Hivyo tuendelee kuwapa elimu wafanyakazi wetu ili tuondoe malalamiko yanayojitokeza.

Naunga mkono hoja asilimia 100%.

Mhe. Mohammed Mgaza Jecha: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kuipongeza wizara ya Afya kwa juhudi zao kuimarisha afya kwa nchi yetu hasa hospitali zetu zote hasa Hospitali ya Mkoani watu wengi wanakwenda hapo na kupiga picha wakisema wako Afrika ya Kusini. Kwa vile hospitali ilivyo nzuri. Sasa kuna malalamiko ya wananchi kuhusu madaktari wako mbali na Hospitali ya Mkaoni wanakaa Chake Chake na wanatumia gari aina ya basi.

Je, basi likiharibika madaktari hawafiki kazini huoni ni hasara kwa serikali kwa nini hawakai Mkoani wakati nyumba za kukodi zipo.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Mhe. Spika, kutokana na idadi kubwa ya wazazi waliojifungua kwa upasuaji, wizara kupitia uongozi wa Hospitali hasa Mnazi Mmoja iandae mikakati maalum ya kuchunguza akina mama wajawazito tangu mimba zikiwa changa na kwa ushirikiano ya madaktari bingwa ili kupata uhakika wa tatizo. Lakini pia maendeleo ya mzazi ujue jinsi ya ukuaji ili kuweza kupunguza tatizo, wananchi wanaamini kwamba kuna mimba hazihitaji upasuaji lakini Mnazi Mmoja tatizo dogo utapasuliwa tu.

Mhe. Spika, pia kuwapatia mafunzo waliopo au kubadili kampuni ya ulinzi ya Mnazi Mmoja kwani wanakuwa ni wanyanyasaji namba moja kwa wananachi, masikitiko ni mengi mno kutokana na mwenendo wa utendaji wao. Lakini pia kuzingatia matatizo yao yanayowakabili, ipo haja suala hili liangaliwe ili kupunguza ama kuondoka kabisa hali hii.

Kuhakikisha madaktari hususan katika sekta ya uzazi madaktari kuchukuliwa hatua wanapofanya ubadhirifu, kwani wanawatusi kuwapiga na hata kuwaambia maneno machafu wazazi wanaokwenda kufata huduma kumekuwa na malalamiko mengi dhidi yao. Lakini pia kuna tabia ya wanaume ambao si wahusika kuruhusiwa kuingia eneo lile ambapo wanawake wengi huwa maungo wazi kutokana na hali zao hii ukizingatia hulka na silka za Wazanzibari.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, napenda kuipongeza wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha kuwa huduma bora za tiba zinapatikana kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Pongezi kwa wizara kwa kuanzisha huduma za "usafishaji wa figo", hii itawasaidia sana Wazanzibari hasa wa kipato cha chini kuweza tiba sahihi kwa wakati bila ya kutumia gharama nyingi kuifata huduma hii Dar es Salaam au nje ya nchi.

Naiomba wizara izidi kuimarisha huduma zinazotolewa katika hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja ili wananchi wetu wasisumbuke. Lengo la kuanzishwa rufaa liweze kufikiwa ili liweze kufanikia vizuri idadi ya wataalamu katika kada tafauti iongezwe kama waliopo nchini kwetu hawatoshi tusione tabu kuazima hata kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara. Sambamba na hilo tuwashajihishe na wengine kusomea fani hizo.

Tunaipongeza Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kuweka kipaumbele kutoa mikopo kwa wale wote wanasomea kozi za *medicine.* Hili likitumiwa vizuri wataalamu wengi wataweza kupatikana. Tunaiomba Wizara ya Afya kuwabana vijana hawa wote watakapomaliza masomo yao lazima warudi kufanyakazi kwenye hospitali za Zanzibar.

Tunaiomba Wizara kusimamia wale wote madaktari waliohamishwa kwenda kuendelea na kazi Abdalla Mzee Hospital Pemba na kugoma kwenda kuwashughulikia ipasavyo ili tatizo la uhaba wa madaktari liweze kudhibitiwa vizuri.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu itaendelea kumairisha ushirikiano wa wizara ya Afya katika kutoa elimu ya afya maskulini. Pia kukisimamia Chuo cha Afya Mbweni kuendelea kushirikiana kuhakikisha kuwa Chuo cha Afya kikiwa chini wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kinatoa elimu bora kama kilivyokuwa kabla ya kuunganishwa kutoka Wizara ya Afya.

Naunga mkono asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Said Soud Said (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri sana kwa jitihada kubwa kwa uamuzi wake wa kujitolea wewe mwenyewe katika kusimamia shughuli zote za wizara.

Ingawa zipo changamoto mbali mbali ambazo zinaikabili wizara hii kama vile wafanyakazi wazembe wafanyakazi ambao si waaminifu watu ambao si wa kweli kwa sera ya nchi yetu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Waziri maradhi ya Ukimwi yanaonekana kupungua kwa kasi kubwa kwa kuwepo kliniki Unguja na Pemba zinazotoa kinga na tiba za maradhi haya thakili na kuanzishwa kupatiwa dawa za *ARV*.

Kuhusu ugonjwa wa homa ya ini. Maradhi haya kwa sasa yamekuwa yapo na naomba serikali itilie mkazo sana kuhusu ugonjwa huu ambao ni mbaya kama kipindupindu sambamba na ugonjwa wa *typhod* ambayo pia unaweza kuenea kwa kasi kubwa sana.

Kuhusu Malaria naomba serikali iendelee na mpango wa kupiga dawa. Lakini pia iendelee na utaratibu wa kupiga dawa majumbani.

Naiomba serikali imalize haraka jengo la upasuaji kwanza Cottage Hospitali ya Micheweni.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukupongeza kuwasilisha hotuba kwa uwazi na ujasiri.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya ni uti wa mgongo kwa huduma za afya ya jamii na inakumbana na maswali nyeti yanayogusa maisha ya binaadamu. Napenda nichukuwe nafasi ya kushawishi Wajumbe kuipitisha bajeti ili kazi ziendelee.

Aidha licha ya changamoto ya mazingira ya utendaji wa kazi ikiwa watawezeshwa naamini watakidhi haja ya wananchi. Watendaji wanahitaji *insuarence traning* za mara kwa mara.

Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee na Vijana wanawake na Watoto haiwezi kufanya kazi pasipo ushirikiano wa kutosha.

Nawashukuru kwa ukaribu wao na kila tunapowahitaji.

Naomba kuunga mkono bajeti yote waliopewa ili watekeleze majukumu yao hasa wanapokusaidia kujitegemea kirufaa.

Naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kufanya kazi zao za kuimarisha afya nchini. Pia niipongeze hotuba nzuri iliyosomwa na Mhe. Waziri kwa ufasaha na kitaalamu.

Nampongeza sana Mheshimiwa katika ziara ya kamati tulitembelea hospitali ya Wete ambapo miongoni mwa changamoto tulizozikuta pamoja na hospitali nyengine kuwa na upungufu. Lakini hospitali hii imezidi kwani tumekuta vitanda vya watoto ambao hawajatimiza umri (watoto njiti) kuna vifaa lakini hakuna madaktari. Hivyo vifaa vile vimekaa tu pale.

Mhe. Mwenyekiti, waziri nashauri wakati wa kugawa madaktari hospitali ya Wete uliangalie kwa jicho la huruma. Mhe. Mwenyekiti, uk wa 47 kifungu cha 110.

Nampongeza Mhe. Waziri na serikiali kwa jumla kwa kuona umuhimu wa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Abdalla Mzee kwa kutenga fedha sh. 1,000,000,000 kwa ajili ya kugharamia baadhi ya gharama za ujenzi wa nyumba hizo. Ni jambo la faraja sana isipokuwa mimi nashauri fedha hizo zikiingizwa tu basi maandalizi yaanze huku tukiendelea na mazungumzo na serikali ya Jamhuri ya watu wa China.

Jengine Mhe. Waziri naomba utapotoa majumuisho yako ueleze zile sababu zilizosababisha madaktari wetu kukaa Chake Chake na kuja Mkoani kwani kuna baadhi ya wananchi wanaona wizara inaharibu mafuta. Lakini kumbe sio nia ya wizara bali ni matatizo yaliyojitokeza kwa wenye nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu uchangiaji damu salama. Kwanza napongeza kitengo hichi na wale wote waliojitokeza kuchangia damu. Mhe. Mwenyekiti, kwa mara hii inaonekana hatukufikia malengo tuliyokusudia. Lakini bado nashauri waendelee kuhamasisha wananchi hasa vijijini suala zima la uchangiaji damu kwani ni muhimu sana kwa binaadamu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri una dakika tano.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante. Hospitali ina uhaba wa nafasi ya kuongeza majengo. Hata hivyo, wizara inafanya tathmini ili kujua njia sahihi ya kupata nafasi ya kuongeza vitanda kwa ajili ya watoto wanaoungua. Kwa hivyo, wizara tunajipanga ili kupata sehemu nyengine na tukishafanya

marekebisho kwenye wodi kongwe ya wazazi, basi tutaona haja pengine ya kuwahamishia watoto hawa katika sehemu ile.

Mhe. Spika, naona nakaribia kumaliza, lakini kwa sababu nina dakika tano naomba niendelee kwa kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie sisi Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi, pamoja na Kiongozi wetu Mkuu Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, tuendelee kuwa na mshikamano ili kwa pamoja tuweze kupanga na kutekeleza mipango mizuri kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, shukrani za pekee ziende kwa Mhe. Waziri wa Afya Mr. Mahmoud Thabiti Kombo, kwa mashirikiano yake na wafanyakazi anaowaongoza na kwa kuwasilisha vizuri hotuba ya makadirio ya wizara kwa ufanisi mkubwa. Hii inatokana na mashirikiano mazuri aliyonayo baina ya wafanyakazi akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara, Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi wengine wote, wataalamu, Watendaji na wafanyakazi wengine wote na tunawapongeza kwa juhudi zao mbali mbali wanazozionesha na kukusudia kwa dhati kuleta mabadiliko katika kutoa huduma bora zaidi za afya kwa wananchi wote.

Mhe. Spika, mwisho wa salama na sio mwisho kwa umuhimu wake naomba niishukuru familia yangu, hususan mume wangu na mama yangu kwa kunipa mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu yangu. Nawashukuru na nawapongeza sana kwa dhati wananchi wote wa Jimbo langu la Wete, pamoja na wananchi wote Wazanzibari kwa mashirikiano yao. Napenda kuwathibitishia kuwa sisi Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi muliotuchagua na kutuamini, pamoja na wale tuliopata bahati ya uteuzi wa Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein, tuko imara kwa kazi, tunakosoana, tunashauriana na tuna mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu yetu. Presha hii mnayoiona kwa wajumbe katika kupitisha vifungu sio kama hatuelewani, bali ni umahiri wa wajumbe kutaka kuhakikisha kuwa mipango tunayoipanga katika wizara zetu ni imara, inatekelezeka na ili hatimaye mipango hii iwe ni mipango madhubuti ya serikali kwa manufaa ya wananchi wote. Tunawaomba wananchi muendelee kutuamini na kuiamini serikali yenu ya Mapinduzi inayoongozwa na Dk. Ali Mohammed Shein. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri wa Afya ili aje ahitimishe hoja yake. Mhe. Waziri una muda usiozidi saa moja kwa ajili ya hitimisho hilo karibu sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: *Bismillah Rahman Rahiim.* Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe, uongozi wa Baraza la Wawakilishi na wawakilishi wote kwa michango yao mizuri sana na yenye ukweli mkubwa sana ndani yake, yenye kujenga na yenye dhamira ya kutusaidia sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendelea kutoa huduma kwa wananchi, naomba niwashukuru sana kwa jambo hilo na kwa kutimiza wajibu wao na Mwenyezi Mungu atawapa uwezo mkubwa zaidi wa kutimiza wajibu wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nichukuwe fursa hii kwa sababu muda mdogo, michango ni mingi sana na michango ya maandishi ni mingi sana, lakini nitaomba niwataje wale waliochangia ili tuwatambuwe pale ambapo nitakuwa najibu na sikuwataja basi watatambua kwamba tayari nimeshawataja.

Waheshimiwa Wajumbe waliochangia moja kwa moja katika mchango huo wa kuzungumza ndani ya Baraza la Wawakilishi, wa kwanza kabisa ni:

1. Mhe. Viwe Khamis Abdalla ambaye pia alichangia mchango kwa niaba ya kamati na mchango wake mwenyewe binafsi akaunganisha hapo hapo.
2. Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata
3. Mhe. MwantatuMbaraka Khamis
4. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
5. Mhe. Suleiman Sarahan Said
6. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
7. Mhe. Mtumwa Suleiman
8. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
9. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
10. Mhe. Simai Mohammed Said
11. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
12. Mhe. Bahati Khamis Kombo
13. Mhe. Salma Mussa Bilal
14. Mhe. Suleiman Makame Ali
15. Mhe. Khadija Omar Kibano
16. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
17. Mhe. Rashid Makame Shamsi
18. Mhe. Hamza Hassan Juma
19. Mhe. Miraji Khamis Mussa Kwaza
20. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, namshukuru sana kwa kauli yake nzito aliyoitoa ya serikali. Maana yeye ni

msemaji mkuu wa serikali na hatua zile alizozisema hapa zitachukuliwa na serikali, hilo ni agizo na zitachukuliwa mara moja.

21. Pia naomba nimtambuwe Mhe. Machano Othman Said ambaye alisimama mwisho na kuchangia na kueleza kanuni, lakini pia ni mchango alitoa hapo hapo kwa Wizara ya Afya alitumia njia ile ya kanuni, kwa hivyo naomba nimtambuwe kwa hilo.

Mhe. Spika, waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Maryam Thani Juma
2. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
3. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
4. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Khamis Juma Mwalimu
7. Mhe. Ame Haji Ali
8. Mhe. Rashid Ali Juma
9. Mhe. Asha Abdalla Mussa
10. Mhe. Juma Ali Khatib
11. Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
12. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
13. Mhe. Ali Khamis Bakar
14. Mhe. Omar Seif Abeid
15. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
16. Mhe. Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum
17. Mhe. Hamida Abdalla Issa
18. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
19. Mhe. Makame Ali Ussi
20. Mhe. Ussi Yahya Haji
21. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
22. Mhe. Mussa Ali Mussa
23. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
24. Mhe. Makame Said Juma
25. Mhe. Nassor Salim Ali Al Jazira
26. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
27. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
28. Mhe. Miraji Khamis Mussa na
29. Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa

Mhe. Abdalla Maulid Diwani nimemtaja katika waliochangia moja kwa moja.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba hawa wote jumla yao ni 54 na wako wengi wangine ambao wametaka kuchangia, lakini haikuwezekana na wengine wamekuwa wakininong'oneza mambo kadhaa wa kadhaa na yote nawaahidi tumeyapokea, ushauri wenu tumeupokea, maombi yenu tumeyapokea na tunakwenda kuyashughulikia mara moja. Kauli ya serikali imeshatolewa na kauli yetu sisi wizara tunasema tunakwenda kuyashughulikia mara moja.

Mhe. Spika, naomba jambo moja tu niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi. Kuna wawakilishi wa aina mbili kwa uzoefu wetu sisi Wizara ya Afya. Mwakilishi atakuwa na jambo lakini atakusubiri mpaka wakati wa bajeti ndio aje nalo jambo lake. Lakini kuna wale wawakilishi ambao kila siku wanatupigia simu wanatuambia kuna tatizo hili tunaendelea kulitatua na kuna tatizo hili tunaenda kulitatua. Sasa yule anaisubiri mpaka bajeti anakuwa anawanyima wale wananchi jambo ambalo lingeweza kutatuliwa mapema zaidi, tusubiri tena mpaka Julai ama Juni kwenda kutatuliwa lile jambo.

Mhe. Spika, kuna mambo kadhaa ambayo nitayataja kumbe yalikuwa chini ya utatuzi tumeweza kuyatatua ndani ya siku mbili, lakini taarifa zile tulikuwa hatuna. Kituo kiko huko baadhi ya dawa kinakosa, mwakilishi anasema kwa kupitia bajeti. Juzi amesema jana zile dawa zimeshapelekwa. Lakini je angesema kipindi kile kile bwana Mheshimiwa eeh! sisi ni wamoja, mwisho wa siku sisi sote tunajenga nyumba hii moja na mwisho wa siku sisi sote tunawatumikia wananchi waliotuleta humu sote kwa pamoja. Mimi pia nimechaguliwa na wananchi kuja humu, sina sasa hivi na mimi pa kuzungumza ila humu humu ndani ya serikali, lakini na mimi pengine ningeweza kuwasemea pia wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki.

Kwa hivyo, naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi, tukiwa na jambo kama hili ama jambo zito, hasa katika sekta ya afya kwa sababu sekta ya afya ina dhima kubwa sana unagusa maisha ya mwananchi moja kwa moja. Naomba muwe munayaleta musisubiri mpaka wakati wa bajeti.

Mhe. Spika, naanza na Mhe. Hamad Abdalla Rashid Gerei, alizungumza suala la gari Vitongoji. Gari tayari jana limeshapelekwa. Naomba ukitoka hapa ukutane na ndugu Mbarawa yupo pale juu atakuambia na ule mchango unaotaka kuchangia basi yeye ndio utawasiliana naye tayari gari imeshafika Vitongoji. Kwa sababu kulikuwa na gari tatu, Micheweni magari yamewazidi hata mafuta hawana ya magari matatu. Tumetoa moja kule tumeleta Vitongoji

rahisi kabisa, lakini ukisubiri muda wote ule wananchi wa Vitongoji wanaathirika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tuwe na utaratibu wa kwamba ukiwa na jambo lolote. Mimi nashukuru kuna wajumbe kama saba hivi wao daima simu mpaka usiku, mheshimiwa eeh! nenda Hospitali ya Mnazi Mmoja. Namshukuru sana Mhe. Bi Panya Ali Abdalla. Mhe. Bi Panya maji yakiwa hayatoki Hospitali ya Mnazi Mmoja mimi najua kabla hata baadhi ya wafanyakazi wa Mnazi Mmoja, namshukuru sana Mhe. Bi Panya Ali. Kwa sababu anakaa maeneo yale sana yeye anacheza, sio maeneo mazuri ya kuwepo sana na mimi namuombea heri Inshaalla na wagonjwa wake wote wapate nafuu, lakini anakuwepo sana maeneo yale kwa hivyo matatizo mengi anakutana nayo. Kwa hivyo, mimi nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi mkiwa na jambo lolote sisi tuko kwa ajili ya kufanya kazi, pamoja tunajenga nyumba ya pamoja, mlilete mapema tusisubiriane mpaka bajeti, kwa sababu ukisubiri mpaka bajeti unakuwa kama unamtega mtu, wakati nia yetu na dhamira yetu kuu ni kuwahudumia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba niende kwenye mchango wa mwisho kabisa, nianze mwisho nije mwanzo. Mhe. Machano Othman Saidi alisimama akataja kanuni na akazungumza, na alichokizungumza yeye pia kimezungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, kimezungumzwa na Mhe. Hassan Hafidh Diaspora, kimezungumzwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani na baadhi ya waheshimiwa wengine.

Mhe. Spika, mimi naomba kuhusu huu uchunguzi kuhusu Kamati Teule, sisi uchaguzi wetu ulifanyika Machi, tulichanguliwa mwezi wa Machi 2016 tulichelewa, mwezi wa Oktoba uliahirishwa ukafanyika Machi. Bajeti yangu mimi niliyoisoma ya mwanzo kabisa ilikuwa mwaka jana mwezi wa Juni, kipindi kilikuwa kifupi sana baina ya uchaguzi na kusoma bajeti. Lakini la pili huyu Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja Dk. Ali Salim kachaguliwa mwezi wa Augusti na Mhe. Rais katangazwa. Katangazwa yeye na Dk. Abdulwakil Idrissa Abdulwakil kama Mwenyekiti wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kupitia sheria mpya iliyopitishwa na Baraza hili tukufu. Maana mwezi Machi tumechaguliwa kipindi kile cha Baraza ndio tulipopitisha sheria ile namba 3 ya Mnazi Mmoja. Baada ya hapo Mhe. Spika, haraka haraka, tena ilikuja chini ya hati ya dharura ya sheria, ikasainiwa ile sheria Mhe. Rais akamteuwa Dk. Ali Salim kuwa Mkurugenzi na Mwenyekiti Dk. Abdulwakil Idrissa Abdulwakili mnamo mwezi wa Augusti, mpaka Augusti hii ya kesho kutwa wao watakuwa wametimia mwaka mmoja, leo tunawaundia Kamati teule ya kwenda kuwachunguza hawa Mkurugenzi na Bodi hata mwaka

mmoja hawakukaa ofisini kwao *is this fare* kweli, si tutawapangua katika kazi waliyopanga, wamepanga mipango mizuri wamepanga mwelekeo mzuri, wamepanga *strategic plan* ya miaka yao mitano kuelekea mbele leo sisi tunataka kwenda kuwafanyia uchunguzi tutawapangua, na tukiipangua Mnazi mmoja tumejipangua sote humu ndani pamoja na mimi na familia yangu. Kwa sababu pale ndio kimbilio letu sote mimi nakuombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi wote mliochangia kwenye hii hoja ya kamati teule, nakuombeni tuwape muda. Bodi hii imekaa vikao viwili tu mpaka sasa hivi tokea Mwenyekiti ameteuliwa wamekaa vikao viwili na wao pia bodi wanampa muda yule Mkurugenzi yale anayopitisha kwenye bodi yaweze kufanyika.

Kuna baadhi ya wajumbe wa bodi wengine wameomba wasiwepo kwa sababu wameona jambo lile ni zito waliomba wenyewe kujiuzulu baada ya kuchaguliwa, kwa sababu wameona lile jambo ni zito mno si jepesi. Kwa hivyo juzi nimemteua mjumbe mwengine mpya kumbadilisha yule ambae ameshindwa yeye mwenyewe, kwa hivyo mimi naomba sana tuwape muda katika bajeti ijayo angalau tutaweza kuwapima Mwenyekiti uliyeteuliwa na Mhe. Rais, wewe Mkurugenzi uliyeteuliwa na Mhe. Rais, wajumbe wa bodi waliochaguliwa na Mhe. Waziri kutokana na ile sheria mmefanya nini nakuombeni sana, hilo ni ombi maalum naomba tusende kuwachunguza sasa hivi, ila nitakuombeni jambo moja Waheshimiwa. Nitaomba sana tufanye kazi na kamati yetu ya Baraza la Wawakilishi Kamati ya Ustawi wa Jamii, nakuombeni Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii Mhe. Spika, pia kupitia kwako kipo kile kifungu kinachosema kwamba Kamati inaweza ikafanya kazi fulani tusaidiane nao, tushirikiane nao wao kutupa yale yote yaliyokuwepo ili tukae kamati na bodi ya Mnazi Mmoja niitishe kikao twende *step by Step* Mnazi Mmoja na wao wawafanyie *Presentation* kamati ili wajue mipango yote na baada ya hapo mtaweza kuja kutuhukumu sote kwa pamoja pamoja na sisi Wizara nakuombeni sana.

Mhe. Spika, yako mengi lakini nitajitahidi nakwenda kwenye mchango wa Mhe. Hamza Hassan Juma, yeye amezungumzia PH0102 naomba tukiangalia ukurasa wa 28 vifaa tiba hivi vyote vimeorodheshwa, katika mchango huu pia kuna mchango Mhe. Jaku Hashim Ayoub alichangia eneo hili, naomba kusema kwamba *Break Down* yake ipo tukiangalia ukurasa wa 93 zote zimejumuishwa humo na kwa sababu ya muda nitakupa *Breck Down* yake *Itemize Break Down* yote pamoja na kile kifungu cha H02 Hospitali ya Mnazi Mmoja. Ukienda kwenye kitabu katika baadhi ya viambatanisho pale H026 mpaka 15 utakuta. Kuhusu kamati teule nimeshaeleza.

Mhe. Hamza Hassan Juma alisema turejeshe sheria Mnazi Mmoja alisema alinisokota kweli kweli Mhe. Hamza wakati wa *retention* na nakubali mimi yote aliyosema nakubali, lakini bado naomba muda tena ikibidi turejeshe basi mwakani tutarejesha sheria hii tuacheni kwanza wafanye, hii niseme kuna Mhe. Mwakilishi amenisahihisha nafikiri alikuwa Mhe. Jaku Hashim kwamba hospitali huru inajitegemea, tunaelekea huko kwenye kujitegemea kwa kiingereza ni *Semi Autonomic* kwa kiswahili hakuna kati na kati lakini ni *Semi Autonomic* lakini kuelekea wapi *Autonomic* nakuombeni sana sheria hii tutairudisha pale tutakapoona tumekwama lakini tunaomba muda zaidi.

Lile suala alisema Mhe. Hamza mvua imenyesha maji yakajaa tayari limeshatatuliwa hivi sasa tumeshirikiana na watu wa Manispaa tumeshalitatua hilo, kwanza nikubali kwamba katika Wizara ambao tunapewa kipaumbele kimojawapo na Mhe. Rais ni sisi Wizara ya Afya hilo nalikubali na ndio maana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais amesimama leo ametoa kauli nzito kwa sababu ya vipaumbele vile vile tunavyopewa pamoja na wenzetu wa elimu, elimu pia haikuwachwa nyuma hata kidogo hata katika ugawaji wa bajeti wa mwanzo sisi wawili tulikuwa, halafu wengine wote wamefuata kwa hivyo na sisi tutaonesha umuhimu huo huo.

Mhe. Spika, naomba niende kwenye mchango wa Mhe. Miraji Khamis Mussa, Chinjio la Kisakasaka tumelifunga sasa hivi mpaka watimize baadhi ya masharti, Serikali kwa Serikali yule pale Mhe. Hamad Rashid tumelifungia sisi na hatulifungui mpaka yale masharti watimize kwa sababu nia na lengo ni kumlinda mlaji ambae ni mwananchi wetu, mlaji yule akipata matatizo anakwenda wapi kule kule Mnazi mnaita Mnazi wenyewe yakishindikana kote wanakuja Mnazi. Kwa hivyo Mheshimiwa naomba mpaka watimize masharti kuna baadhi ya machinjio pia nayo yalifungwa wakatimiza masharti nayo tumeweka sawa.

Mhe. Spika,mmetakiwa kauli kuhusu *EBOLA* Mhe. Ummi Mwalimu keshatamka kule ametamka kauli nzuri sana na bahati nzuri mimi nilikuwa nae juzi tumekaa pamoja tumelizungumzia hili, lakini na mimi naomba nitamke sasa kuna maradhi yanaitwa *Incubation Period* maradhi ambayo yanakaa katika mwili kwa muda fulani mfano Malaria, kuanzia mbu akikutafuna mpaka ukaipata ile Malaria ikaja juu ni siku saba *Incubation Period* Mhe. Gerei atakueleza zaidi yeye ni mtaalam. Lakini maradhi ya *IBOLA* ukiyapata huwezi kufika kutoka Kongo au huko kwengine mpaka Zanzibar huwezi hata siku moja kufika. Kwa sababu *Incubation Period* yake ni saa 12, ndani ya saa 12 unaanza *bleeding* ya ndani kwa ndani huko Kongo kuvuka kufika mipaka ya Tanzania basi si rahisi sikwambii huku Zanzibar, ila tahadhari zote tunaendelea

kuichukua katika vituo vyetu mbali mbali na hivi karibuni mtaona tunarudisha tena zile *Screen* zilizokuwa zikikaa bandarini pamoja na *Air Port* kama za kupima *Temperature* kwa hivyo hilo naomba tuondoshe hofu hakuna *IBOLA* Zanzibar wala hatuna hali ya hatari ya *EBOLA* na *WHO* pia wametwambia *EBELA Free zone* kabisa. Kwa sababu mtu hawezi kusafiri huko akafika hapa na *EBOLA* yake akawahi atamalizika huko huko njiani kabla.

Mhe. Spika, kuna vyombo vingi ambavyo vinahusika katika kutoa taarifa hizi na kimoja wapo ni Shirika la Afya Duniani, kwa hivyo hadi sasa hata kwenye kipindupindu hatujawekwa bado katika *list* ya Dunia kwa sababu kipindupindu chetu kiko eneo dogo, Chumbuni, Daraja Bovu, Kinuni, Mtopepo kinacheza pale pale sasa hivi kwa hivyo hatujawekwa katika orodha ya nchi hatari kwa kipindupindu mpaka sasa hivi na tumeweza kukidhibiti na tunaendelea kukidhibiti vizuri sana.

Mhe. Rashid Makame Shamsi ameuliza yeye kubadilisha mashuka pia hospitali kunahitajika wahisani na wafadhili, hakuhitajiki na tutaendelea kuifanya kazi hiyo. Tunachokikosa sisi kikubwa kabisa ambao Uongozi wa Mnazi Mmoja leo upo hapa, leo bahati nzuri uongozi wa Mnazi Mmoja mzima upo hapa na bodi yao pia nimeialika leo wapo juu hapo, nataka haya mengine mliyosema nyinyi wasikie *inshaallah* buti zisiwepo, lakini zikiwepo buti nataka na wao wasikie sio asikie Waziri na Naibu Waziri tu na wao. Kinachokosekana ni usimamizi wa juu hamsimamii wa chini ,wa chini hamsimamii wa chini wachini hamsimamii ya chini yake. Sasa mimi nakuahidini Mimi Naibu Waziri, Katibu Mkuu wangu yupo pale, Naibu Katibu Mkuu wangu yupo, Wakurugenzi wote, Mkurugenzi Mkuu namuona pale Dkt. Jamala Adam Taib yuko, Mkurugenzi wa Mnazi Mmoja kakaa pembeni yake kama hamumjui Dkt. Ali Salum hawa nitawaomba wote sasa tushuke chini tushuke mpaka ngazi ya *Orderly* kama leo Wawakilishi wanakuja picha zote nimeziona mimi zile video zote kila kitu, pachafu maji yaliyopojaa, maji yanavuja, paa linaning'inia hivi yote tushuke chini tukishuka chini mengi yatawezekana. Kwa hivyo tunakuahidini sote Wakurugeni mimi nitawaondosha Ofisini kwao sasa hivi wasikae Ofisini, wakae muda mchache ofisini washuke chini zaidi isifike mpaka mtu anafika hapati huduma.

Kuhusu Ugatuzi Mheshimiwa imo kwenye bajeti tumeandika lakini naomba nilitolee ufafanuzi mzuri kabisa, Mhe. Haji Omar Kheir yeye tunampelekea katika ugatuzi vituo vyetu 140 vyote vitakuwa kwake, wafanyakazi takriban 1,300 watahama Wizara ya Afya watakuwa kwake, wale Ma- DMO wetu *District Medical Officer* watakuwa kwake, lakini tutashirikiana nae kwa karibu sana kusaidiana na kiungo chetu kikuu kitakuwa ni Afisi ya *ZMO Zonal*

Medical Officer iliyokuwepo pale Lumumba ofisi yake, kile ndio kitakuwa kiungo chetu kikuu kwa kushirikiana nao wnzetu. Tunafanya hivi ugatuzi *Advantage* yake kubwa kwamba kule ngazi ya chini Halmashauri na Manispaa wale wataweza kusimamiwa vizuri zaidi na kuhakikisha huduma zinafika zaidi na wawakilishi naamini watashirikishwa zaidi. Katika ugavi wa dawa safari hii nimeshawaambia watu wa Bohari wapo juu pale wawashirikishe Wawakilishi kwenye vituo vyenu mkenda wakenda kugawa dawa na nyie muwepo ili muone.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh alizungumza kuhusu kile ki-*note* kutolewa kile kilitolewa kwa sababu dawa zile zipo na mimi kama Waziri nilikuwa nina hakika dawa zile zipo kwa nini mwananchi ananyimwa ndio nikamwambia nataka maelezo, kwa nini dawa hii hajapewa akapewa pale pale. Kwa hivyo mara nyengine dawa hii zinakuwepo kwenye vituo vyenu vya majimboni, vituo vyetu sisi Wizara ya Afya lakini vituo vyenu vya Majimboni dawa hizi zinakuwepo. Lakini kwa sababu moja au nyengine anakuwa mgonjwa hapati, kwa hivyo tunataka Waheshimiwa Wawakilishi tuwashirikishe ili wajue na wao kwamba dawa zile zipo, mgonjwa anapokujia unamwambia dawa ipo ikiwa kirungu suala jengine, lakini kama anakujia hasa kwa ajili ya dawa unamwambia dawa hii ipo na mimi nimeona shahidi twende kituoni. Kwa hivyo Waheshimiwa Wawakilishi tunaomba tuwashirikishe sawa na wakati tunafanya masuala hayo ya kugawa dawa.

Mhe. Rashid Makame Shamsi pia alizungumzia ile habari ya *Chemical* Bashirifu ile inayochanganywa ile *Ephedrine* ndio maarufu *Ephedrine Hydrochloride* wenyewe wanaita wataalam kwa hapa Zanzibar sisi hatuna tatzo, lakini wenzetu kweli lipo lipo huko tatizo kidogo kama ulivyosema imekamatwa. Lakini kwa hapa Zanzibar naomba niendelee kuwapongeza sana *Zanzibar Food and Drugs* yaani hii Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi wanafanya kazi nzuri sana na kazi kubwa ya kuweza kudhibiti mpaka Uwanja wa Ndege, chochote kinachoingia hata ikiwa *quantity* ndogo basi wao wanadhibiti, kwa huko naomba tuondoshe hofu.

Kurejesha huduma za afya maskulini hizi tunaendelea mpaka sasa hivi ni koo, pua, sikio na macho huduma nne hatujaweza kufanya zote bado na yote ni kutokana na uhaba wa wafanyakazi, lakini hizi huduma nne tutaendelea nazo ripoti imo ndani ya kitabu na tutaendelea kutoa semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu bado elimu inahitajika, jana mmefaidika mmeambiwa mambo mengi sana kuna walioiuliza masuala mengi sana kuhusiana na ile homa ya ini. Kw hivyo tutaendelea kufanya hivyo naomba tushirikiane zaidi.

Mashirikiano na Waziri wa Elimu pamoja na Sekta ya Elimu tunaendelea bahati nzuri yeye ndio Kaimu Waziri wa Afya nikiwa sipo mimi ndio kaimu wa Wizara ya Elimu akiwe yeye hayupo, kwa hivyo hakuna mashirikiano zaidi ya hayo nashukuru sana. Mhe. Spika, tunamshukuru sana Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa kutuunga mkono kwa asilimia mia moja tayari yeye ameshatuunga mkono.

Mhe. Spika, sasa naomba niende kwa Mheshimiwa Salma Mussa Bilali katika mchango ambao umenigusa sana naoni mchango wake mojawapo. Amezungumza Mhe. Salma Mussa Bilali hizi lugha nzuri lugha njema hatufundishi kwenye shule zetu hizi za afya, Chuo cha Afya Mbweni kina *Subject* nzima kuhusu maadili, lugha na jinsi ya kumuenzi na kumtunza mgonjwa kuna *Subject* nzima pale ukenda kutembelea Chuo cha Afya na naambiwa watoto wanaotoka pale wanakuwa wazuri nimeambiwa hilo, wakishaingia Mnazi na wao wanakuwa wanaambukizwa. Kwa hivyo kwa hilo tutaendelea kulifanyia kazi kuanzia chuoni huku tunalifanyia kazi vizuri na sasa hivi Chuo kiko Wizara ya Elimu *SUZA* tumeshawakabidhi lakini tunaendelea kushirikiana nao karibu sana na bodi husika inayosimamia lugha hii ipo pale juu. Dkt. Amina Abdulkadir Mwenyekiti wa bodi yupo pale juu yeye ndiye anayesimamia hasa masuala haya na tumemualika apate kusikia yote.

Pia amezungumzia kuhusu takwimu, amezungumza Mhe. Naibu Waziri, taarifa rasmi ya tafiti zinazofanywa Wizara ya Afya tuwe tunazitoa tumeshaanzisha kijarida chetu kwa hivyo tafiti hizo na matokeo yake ya tafiti tutatoa, na safari hii tunataka kufanyia utafiti kipindupindu tukwambieni kwa nini kipundupindu kinarejea Zanzibar kila mwaka baada ya mvua tu tunakwenda kwenye kipindupindu imekuwa ni kawaida sababu zake kuu.

Idadi ya wazazi wanaozaa kwa upasuaji imezidi wananiambia wataalam jana nimekaa nao tena watalaalam wananambia njia pekee iliyokuwa sio hatarishi ni upasuaji na kinamama wengi wanaokuja pale wanakuwa aidha na *problem* ya *pressure*, ama kisukari cha mimba, kisukari cha uja uzito kuna kisukari chake, pregnacy diabetic ama damu kuwa ndogo, sasa yakishakuja mambo yote yale kwa pamoja na pressure na nini hata nguvu za kusukuma anakuwa hanazo. Kwa hivyo Daktari anafanya uamuzi kwamba *the safe first medhod* njia pekee ya kumzalisha salama yule ni kwenda kwenye upasuaji, ndio maana umeongezeka. Kwa hivyo tujaribuni kwa pamoja tuhangaike Afya ya Mjamzito anapokuja hospitali iwe nzuri na njia moja ya afya ya mjamzito kuwa nzuri anapokuja Hospitali wakati wa kujifungua ni kuanza mapema kwenda *clinic*

miezi mitatu, minne, mapema kabisa ili unachunguzwa mapema unaonekana mapema. Kwa hivyo hilo nalo naomba nilieleze hivyo.

Hospitali zipi zinazotumika kwa bima ya afya kwa upande wetu Wizara ya Afya mpaka hivi Sasa hospitali yetu ya Mnazi Mmoja inatumika kwa Bima ya Afya hii NHIF kadi yako ukenda pale, lakini tunatarajia hivi karibuni kutanua huduma zetu ili hospitali nyengine mpaka za Wilaya yaani Makunduchi, Kivunge, na zile za Pemba kule Wete, Chake, Abdalla Mzee, Vitongoji bado Mheshimiwa na Micheweni hayo yote tunataka kuyafanya kwa kuunganisha waweze kuwapokea wale *Member* wa bima ya afya lakini wakati huo huo tumeshatiliwa fedha nimeona katika bajeti kuanzisha mfuko wa Bima ya Afya yetu wenyewe, mchakato tunaendelea nao na ile sheria yetu itakuja hapa hapa Barazani, naamini katika kikao kijacho tutaweza kuwasilisha ile sheria, tunakwenda nayo mbio ili weze kupita taratibu zote halafu tuweze kuwasilisha bima yetu wenyewe ya afya. Anasema tunachelewa wee tunakwenda kulipa kwenye bima nyengine tunasubiri bima ya Zanzibar naomba tuendelee huko itakapokuja yetu tutaingia huku kwetu.

Hospitali ya Abdalla Mzee ni ya Mkoa sasa lakini bado tunatakiwa tuziangalie hospitali nyengine bajeti tumeweka ya kutosha, hili nawajibu pamoja na wale waheshimiwa waliochangia paa la Chake Chake, pale safari hii alilazwa Mhe. Waziri wa Elimu alipokuwa anaumwa pale pana VIP nimeiona mwenyewe nikasema daa, mtu yoyote mwengine akiumwa Pemba wakati huku anafanya kazi zake Pemba atalazwa pale. Kwa hivyo tumetenga kama milioni 300 kwa ajili ya hospitali ya Chake Chake na nawaomba Waheshimiwa waondoshe hofu zitatumika ipasvyo kufanya ukarabati uliokusudiwa.

Mhe. Salma Mussa Bilali pia alisema hatujui chochochote yeye na Mhe. Sima hatujui chochote kuhusu Binguni bado hatujui chochote Binguni safari hii tumeitengea Milioni 300 nayo mtaona kidogo lakini hizo Milioni 300 Shilingi ni kwa ajili ya *feasibility study* kutengeneza *Master Plan* ya eneo lile pamoja na kujenga ukuta wa uzio tunaanza na hatua hiyo, lakini wakati huo huo mazungumza tunaendelea kuyafanya kwa sababu miongoni mwa ahadi mbili zilizobakia za Dkt. Ali Mohammed Shein mkiangalia ilani ya Chama cha Mapinduzi miongoni mwa ahadi mbili zilizobakia katika sekta ya afya ni bima ya Afya, na Hospitali ya Binguni nyengize zote 12 zile zote ameshamaliza kabakisha 2. Kavunja rekodi maana ndani ya mwaka mmoja kamaliza zote yeye kabakisha mbili tu. Kwa hivyo naomba kusema kwamba ile ni ahadi Dkt. Ali Mohammed Shein yeye ni muungwana alitoa ahadi hiyo ya Binguni wakati anakwenda kuomba ridhaa kwa wananchi na naamimi ataimaliza kabla ya mwaka 2020 na sisi Wasaidizi wake tupo tunamsaidia tunakwenda mbio

tumeshaanza mazungumzo .Kwa hivyo sasa hivi *feasibility study* inakamilika *master plan* ya eneo lile na uzio naomba hilo tuondoshe hofu na fedha tumetengewa kwa ajili ya hospitali hiyo.

Mhe. Spika, nataka kuongeza *Speed* kidogo kuhusu Jenereta Mhe. Naibu Waziri ameeleza *quotation* zimeshafika na wiki hii atapewa mtu tenda ya kuanza kujenga ile kazi mara moja, tumeshuka chini imebidi tushuke chini lazima tuseme ukweli, Mhe. Abdalla Maulid Diwani nakukubalia ni kweli unajua ukiwa umefunga inabidi uwe mkweli zaidi, ndio maana Mwezi wa Ramadhani unaambiwa mwezi wa barka, neema, rehma mafungu yale yote, kwa hivyo mwezi huu inabidi uwe mkweli mara mbili zaidi, mimi nakubali ni kweli huwezi kufahamisha miezi mitatu kijenereta kimoja tu, haiwezekani ni kweli tumeshuka chini ndani ya kipindi kifupi cha siku kumi hizi utaona kazi inaendelea na inafanywa pale.

Tulikwenda mbio kutafuta jenereta kwa sababu palikuwa panatokea vifo *maternity* na *theater* umeme ukizimwa leo jenereta lishapatikana vipi tusionane nakukubalia Mheshimiwa nakukubalia na hili utaliona ndani ya kipindi kifupi na wewe mwenyewe utakuwa shuhuda maana nitakupigia simu wewe na Mhe. Hassan Khamis Hafidh mje pale muweze kuangalia. Najua nyie ni wadau wetu wazuri sana.

Maji, kisima na huduma za maji Mnazi Mmoja hili la Mhe. Bi. Panya pia na Waheshimiwa wengi wamechagia hili, Mnazi Mmoja kuna *reserve tank* ya lita1,000,000 pale, Mnazi Mmoja hivi sasa tunapata lita 30,000 elfu mpaka 50,000 elfu baadhi ya wakati kwa sababu maji yamepungua chini ya ardhi, tumeshakaa na watu wa ZAWA kisiwa chetu kimoja kiko Victoria Garden pale kwenye ZAKUKURU ya kwetu, pale kisima chetu kimoja kiko pale. Paipu ya pili ni *main line* ya Serikali. Hivi sasa tunakaa tunatafuta mbinu ya kuwa na kisima cha tatu kisichokuwa na chumvi kwa sababu eneo lote la Mnazi nyie mnaita, Mnazi basi ni eneo la chumvi kwa hiyo pale huwezi kupata kisima, inabidi tukitowe maeneo labda huko kwa Mhe. Dimwa au kwa Mhe. Nassor Salim Ali tuvute *line* ya kwetu wenyewe ije Mnazi Mmoja iweze ku-*supply*.

Demand ya Mnazi Mmoja ni lita 2,500,000 kwa siku, *reserve* tunayo *demand* kuengezeka kwa vitanda, sasa hivi tuna vitanda 800 ni lita 2,500,000 kisima wala *source* ya ZAWA hazifiki lita 2,500,000 siku ndio maana tuna *shortage*, tunakwenda mbio sasa hivi kuna timu tumeleta wataalamu wa maji ambao wako pale wanafanya *monitoring* pamoja na zile pampu zote itabidi tuzibadilishe kwa sababu zishakuwa ndogo zimezidiwa, kila huko waheshimiwa majimboni mkiendelea kuzaa zaidi maji yanatumika zaidi kule.

Tulikuwa sisi kwa siku tunapokea zamani watoto 38 mpaka 40 kwa siku sasa hivi tunagonga 100 mmeona kwenye kitabu nimeandika humu tunakaribia 100 kwa hivyo na maji yanaongezeka kwa hivyo tupunguze na huko kidogo. *(Makofi)*

Anasema ukifika kwenye huduma za maabara mara nyengine unambiwa nenda Alrahma siku hizi kuna pahala panaitwa *lancet* nenda hapa nenda pale, mnyonge atapata wapi hizi elfu 90,000? Ni kweli Mheshimiwa, tatizo letu kubwa pamoja na wale walioulizia hususu dawa na vitendanishi. Tatizo letu kubwa ilikuwa ile *mechanism* ya *procurement* sasa hivi tumeshatoa mtaalamu kwa masuala haya vitendanishi tumempeleka Bohari mmoja tumemtoa huku tumempeleka Bohari, ili awe ananua yeye kilea anachokitaka ifike kwa wakati, na ninakuhakikisheni tumeshaanza programu hiyo, sasa hivi ni kama mwezi wa sita tokea tumeanza tunaona tunakwenda vizuri. *Test* nyingi ukiacha chache zinaweza kufanyika katika *laboratory* zetu kuu, lakini katika eneo hilo mimi mwenyewe nakuahidini kwamba nitashuka na nitaendelea kuweka mkazo zaidi ili vifaa hivi vifike kwa wakati. Tukiishiwa pale ndio matatizo yanayopotokezea na nyinyi ndio mnakuwa watu wa mwanzo kujua matatizo yale, kwa sababu mko karibu sana na wananchi, kwa hivyo hilo tutaendelea kuliongezea pale.

Mhe. Spika, umesema wataalamu tunao lakini tunawaweka sipo tunajitahidi kuwaweka ndipo, na hivi karibuni tutafanya mabadiliko makubwa mtayaona, mabadiliko makubwa yanakuja. Mmemsikia Mhe. Mohammed Aboud amesimama hapa amezungumza asubuhi mabadiliko makubwa, sitafuni maneno yanakuja, kwa hivyo mtayaona. Miongoni mwa mabadiliko haya fedha pia, mnasema fedha nyingi zinatolewa katika Bajeti lakini yale matokeo madogo miongoni mwa mabadiliko hayo ni kwenda kuangalia hayo, fedha nyingi zinakwenda wapi, kwa nini matokeo yake madogo. Naomba tupewe muda tuyafanyie kazi sisi wenyewe pale tutakapokwama tutakaa na Kamati tutazungumza lakini naamini hatutokwama kwa hivyo na nyinyi naamini hiyo Kamati Teule itakuwa haipo hii.*(Makofi)*

Mhe. Spika, nakwenda kwa Mhe. Hassan Khamis Hafidh uchafu umekithiri katumia neno hilo naomba niseme kweli, nikatae kwa nini kwani mimi siuoni, kwani Mhe. Mohammedd Aboud aliposimama hapa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kasemaje, mengi mlosema yote ni kweli, uchafu umekithiri. Mheshimiwa mimi naomba niwaahidi kwamba hivi karibuni tutachukua Kampuni ya kusafisha hakuna njia nyengine. Tutachukua Kampuni ya Kusafisha mnaona Baraza letu linan'gara hapa, maana yake hapa niliposimama mimi panan'gara, tutachukua kampuni ya kusafisha hilo halina

mjadala. Tukichukua Kampuni ile ya kusafisha watashughulika kote pamoja na huko *Mental* kwenye majani nyoka walikozidi kote pamoja tutamalizia. *(Makofi)*

Amesema pia Mhe. Hassan Khamis Hafidh hakuna watu wanaosemwa kama nyinyi watu wa Sekta ya Afya na hakuna pahala panaposemwa vibaya kama Mnazi Mmoja, inshaallah mwakani kidogo mambo yatakuwa tofauti tumuombe Mwenyezi Mungu. Ni kweli najua tunasemwa, mimi ni kweli najua tunasokotwa yote nakubali tunasokotwa sana, lakini Mwenyezi Mungu atatujaalia kwa nia yake njema kiongozi wetu Dkt. Ali Mohamed Shein suala la *priority* tunayopewa kwenye Bajeti kwa nia zetu safi sisi sote kwa pamoja, tukiwa tunashirikiana kama hivi tumeonesha mashirikiano makubwa naamini tutasemwa kidogo, sisemi hatutosemwa kabisa aa tutasemwa kidogo mwakani naamini tutasemwa kidogo. (*Makofi)*

Mhe. Spika, tatizo nini *management*, *supervision*, watu, Rais anachukua jitihada kubwa sana yote hayo ni matatizo *management* tatizo, *supervision* tatizo, watu tatizo upungufu wa watu tatizo yote hayo ni matatizo, lakini yote tutayakusanya katika mfuko mmoja safari hii tuyatatue. Nimeshaeleza kuhusu Kampuni hiyo ya usafi kwa hivyo yote hayo yataweza kufanywa humu.

Mhe. Simai Mohammed Said pia alitaka kujua kuhusu takataka Mnazi Mmoja, Serikali imeshatoa agizo rasmi ya kununua *special incinerator* ya kuteketeza taka zote naomba mtupe muda ndani ya kipindi kifupi tutafanya *under emergency purchase incinerator* ambayo itaweza kuteketeza zile taka hatarishi za Mnazi Mmoja. Namshukuru sana kiongozi wangu Mhe. Rais kwa kunisaidia katika hilo na kusema kwamba hili jambo lifanyike mara moja namshukuru sana.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid naomba nikupongeze umezungumza kitaalamu sana maana uliyozungumza mengi ni ya kitaalamu tumeyapokea, ya ushauri kuyafanyia *orientation* ma-*oderly* na manesi na kada nyengine mbali mbali tutaendelea kufanya naomba nikwambie kwamba tumewachukua *orderly* 14 tumefanya *experiment orderly* 14 kwenda kusoma, masuala ya uuguzi wamefanikiwa wawili walikosa lakini wengine wamefanikiwa. Naomba kusema kwamba wauguzi siku hizi wameshaanza ku-*qualify*katika hizo *specific professional* kama vile *psychology*, *ICU* yaani *Intensive Care Nursing* wako wanaosoma ukiangalia kitabu utaona pia na tunashukuru sana Shirika la UNFPA ambao wanatusaidia. Tuna watano ambao hivi karibuni tumewasomesha *dialysis* manesi kada yako hiyo ambayo wamesoma *dialysis* wako waliosoma ICU, wako waliosoma *anesthetic assistants* wote hao wako

masomoni na tutaendelea kuzingatia ushauri uliotupa wa kusomesha kada maalum, asiwe *general nurse*, sasa hivi ende kwenye *specialization* kwa sababu tutawahitaji na watatusaidia sana pale pahala ambapo pana upungufu wa madaktari.

Cottage ya hospitali ya Vitogoji ina *nurses* watatu tu, naomba nenda tena kaangalie sasa hivi wako wangapi halafu nijibu. Ndio yale niliyosema kuna ya papo hapo, tusisubiri kwenye bajeti kuna yale ya papo hapo, unamwambia Mhe. Rashid nataka taarab kesho anakuletea kikundi cha taarab kesho huna haja ya kusubiri. Kwa hivyo naomba uangalie halafu urejee kwangu tena. Uchakavu wa majengo tayari nimekwambia milioni 300 zimetengwa paa linavuja tayari fedha hizo zimetengwa, kuhusu *ambulance* yako tayari imeshafika hospitali kwako naomba wende ukaangalie na uzungumze na ndugu Mhe. Mbarawa.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar amezungumza *film* za *X-Ray* kweli wakati mwengine hutokea uhaba yote sio kwa sababu ya fedha lakini katika ile *process* ya uagiziaji kuna Kampuni chache ambazo zina-*supplly film* za *X-Ray*, lakini sasa hivi tunataka kuachana na masuala ya *film* kwenda *digital* moja kwa moja. Kwa wale wanaokwenda kutembelea hospitali nyengine wanaona siku hizi unapewa CD ama DVD moja kwa moja, hupewi tena ile *film* ukaondoka nalo bahasha lako kubwa aa unapewa DVD tu, mwili mzima. Mapigo ya moyo mambo ya damu, mambo ya *brain scan*, kila kitu inakuwa kwenye CD unawekewa DVD unatia mwenyewe unatazama moyo wako unavyopiga, kila chemba unaiona kwenye DVD, tunataka kuelekea huko kwa sababu tumeshapata mitambo ya *digital* tunataka kuelekea huko. Tunataka kuachana na mambo ya *film* na kutia zile dawa za kuchanganya.

Kuna suala nadhani Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Simai Mohammed Said wamezungumza la *mortuary*, alisema maiti ya mzungu imeondoshwa pale imepelekwa Bububu hospitali ya Jeshi ni kweli, kwa sababu tulipata kidogo taathira, kuna maiti pale imeathirika sisi wizara tunapata taathira na anajewajibika ni Waziri. Tulipata taathira hiyo namshukuru sana Ndugu Mjaka kasema Mheshimiwa maiti hii ina wenyewe uko, naomba tuiondoshe haraka sana kweli tuliiondosha, kwa hivyo naomba niahidi Baraza lako Tukufu Mhe. Spika *mortuary* mpya tutaitengeneza. Itakuwa kama ya Jeshini Bububu kwa wale waliofika Jeshini, tunashirikiana nao sana hawa hospitali ya KMKM na Bububu Jeshini tunashirikiana nao sana tunawashukuru na wao pia, itakuwa mpya kama ile iliyokuwapo Bububu. *(Makofi)*

Pale tutaiondosha kwa sababu pale pashakuwa katikati mno, mtu anakwenda kufanyiwa *neuro* anakwenda kufanyia *neuro* uti wa mgogo ama operesheni wa kichwa kule anapita *mortuary* anaona ile hofu yake inaongezeka akenda kule. Kwa hivyo nataka tuiondoshe pale *mortuary* iondoke pale kabisa tuiweke kwengine. Kwa hivyo hilo mtupe muda tutalishughulikia suala la *mortuary*, nashukuru ahsante sana kwa wale walionikumbusha.

Mhe. Zulfa pia alizungumza *cityscan* ya Abdalla ya Mzee inahitaji hivi vifaa vya *film* na kadhalika ni kweli anasema bure, tumeweka bajeti ukurasa 63 ya huduma za tiba ya bajeti hiyo sehemu yake inakwenda kule, kwa wananchi wanatoka Unguja kwenda Pemba kwa ajili ya sityscan ni kweli, Mhe. Rais wakati anafungua hospitali ya Abdalla Mzee alisema hiyo katika Hotuba yake watu watatoka Mombasa watakuja hapa kutibiwa alisema na nyinyi mashahidi maana wengi mlihudhuria siku ile, tayari Mungu ameshaonesha haya watu wanatoka sehemu mbali mbali wanakwenda kwa ajili ya kupata huduma hizo. Hospitali ya Abdalla Mzee. Ukiangalia kifungu kile cha Mhe. Hamza Hassan Juma H01020107 mimi nimekiita kifungu cha Mhe. Hamza makusudi kwa sababu najua ataniuliza baadae H01020107 tumekihifadhi tayari na mtiririko wake wote, upo hicho ndio kifungu chako. Tayari Mhe. Zulfa katika kifungu hichi ya Mhe. Hamza hichi tulichokipa jina kinafedha hizo.

Tuchukue madaktari kutoka Tanzania Bara tumeshaanza hiyo tukitangaza daktari kama hapa hajapatikana Unguja, tunapeleka yale matangazo Tanzania Bara nawashukuru sana Mhe. Ummi Mwalimu, Waziri wa Afya wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, namshukuru sana Katibu Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Wizara ya Afya Dkt. Mpoki, ninamshukuru sana Prof. Mohammed Bakari Kambi ambaye ni Mganga Mkuu, tunashirikiana katika kwenye eneo hilo na ametwambia atatupa mashirikiano zaidi, kwa sababu sisi tuna mashine kubwa sana ya MRI ya kisasa wataalamu wake hawapo, hapa Unguja hawapo. Huko Tanzania Bara wako wane tu lakini wamesema watatupa mashirikiano kumleta mtaalamu wao mmoja kuja kuwapa mafunzo watoto wetu hapa na tunachukua watoto wabichi. Sasa hivi tushachukua wasichana wabichi wadogo kabisa, tumechukua wabichi kwa sababu tunataka wakae muda mrefu hatutaki tena kuchukua mtu ambaye amebakisha miaka mitano au kumi sisi tutumie uwezo wetu na fedha zetu kum-*train* halafu baada ya muda anaondoka.

Hawa watoto miaka 26-27 piteni pale mtawaona, wako wasichana wadogo wawili pale., Kampuni ya usafi nishaieleza. Katika kutoa nafasi za ajira hatufanyi ubaguzi, katika nafasi za ajira hatuulizi huyu anatoka wapi huyu anatoka wapi, hatuulizi huyu wa wapi huyu wa wapi, tunatoa wote kutokana na

sifa zilizotangazwa. Kwa hivyo naomba hilo muondoshe hofu Waheshimiwa Wawakilishi hatuna ubaguzi wa aina yoyote katika ajira.

Mhe. Suleiman Sarahan Said alizungumza kuhusu maziwa kunyonyesha, madaktari walikuwa wananitania wananambia siku hizi maziwa haya wananyonya wengi, kwa hivyo tunaendelea kusisitiza mtoto asi-*share* anyonye mtoto tu alozaliwa ndani ya miezi sita asi-*share* na mwengine. Kuhusu chumvi, chumvi kutiwa madini yoto na kadhalika. Tayari tunaendelea kudhibiti na ZFDP kusaidiwa tunaendelea kudhibiti ziingie chumvi joto, madaktari kuwafikiria kwa upande wa usafiri kwa wale wanaokaa mbali sana maeneo ya mbali tayari kuna *minibus* tumeshanunua kule Pemba zinafanya kazi, tutaendelea kuwafikiria zaidi hasa wale wanaojitolea, kuna kituo kimoja nilikwenda hivi karibuni Ndagoni, kuna Afisa Tabibu kwa Mhe. Suleiman yupo tulikwenda pale kituoni yule kijana aliyekuwepo pale yule muuguzi, amejitolea anatoka mbali kweli kweli amejitolea mwenyewe kuja kituo kile, kwa kweli tulimpongeza na mimi nilimuahidi nitafanya kila mbinu kumtafutia japo kitu kidogo kwa mpango maalum aweze kwenda na kurudi. Kwa hivyo hilo nalo tunalichukua na tutalifanyia kazi.

Kuhusu watoto njiti tayari Kitengo cha Kaharuki kichafunguliwa kiko pale Mwembeladu mkipata nafasi Waheshimiwa Wawakilishi tutaandaa Semina maalum ya kitengo cha Wazazi mambo ya *eclampsia* haya na wanaume tunaomba mje kwa wingi sana siku hiyo, watafanya mpaka kuonesha vipi mtoto anavyozaliwa. Mimi nishafanyiwa tayari semina hiyo, kwa hivyo wote tutawaleta pamoja na wakati wa semina hiyo tutaeleza masuala ya kangaruu wale watoto njiti, wanatugharimu kiasi gani Serikali tutawaeleza siku hiyo. Kwa sababu wale wanahitaji gharama zaidi kwa sababu *care* yao inakuwa kubwa zaidi, kwa sababu wanakuwa wamezaliwa kabla ya muda wao. Kwa hivyo na Kitengo hicho kipo tayari kutaendelea kukifanyia kazi kwa pamoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alizungumzia sana Sheria Nam. 3 ya Mnazi Mmoja naomba nikubaliane naye yote aliyoyazungumza pale, alisema kwamba hospitali inajitegemea lakini *semi autonamous* kwa Kiswahili mtanisailia wataalamu wa Kiswahili *semi autonamous* ni neno kujitegemea hivyo hivyo au inajitegemea kiasi tuseme, *semi autonamous* inayojitegemea kiasi nakubaliana naye. Majengo mapya ICU ipo, dawa hakuna ndani hakuna kinachoendelea, Mheshimiwa naomba kusema dawa zipo lakini masuala ya AC tunayafanyia kazi tunamshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tunamshukuru Bi. Asha Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wametusaidia sana mchango wao ni mkubwa sana katika eneo hili la ICU naomba niendelee kutoa shukurani zangu

dhati kwao wao pamoja na mama yetu mpendwa Mama Mwanamwema Shein ambao wamekuwa wakitusaidia sana eneo hili. *(Makofi)*

Tuwe na moyo wao wakati mwengine tunasema sana lakini tuwe na moyo wao wakija wanasema machache lakini wanafanya makubwa, wakija pale anasalimia na kuzungumza machache lakini anayoyaacha pale ni makubwa, tunabakia sisi kuwakumbuka na kuwaenzi na kuwaombea dua kila siku, tuwe na moyo kama huo *stretcher* zipo, zile gari zenye matairi yaani *stretcher trolley* zipo, vifaa vile vyote *gauze* alivyovitaja, viwembe *theater blades*, zote zipo *cannula urinary bags*, zote zipo, Dkt. Zaharan yupo pale ametuthibitishia na tumekwenda kutazama vyote vipo. Ila wakati mwengine wale wanaojaza fomu hawajazi kwa wakati ndio maana vile vifaa vinachelewa kufika kituoni.

Generator nimeshalijibu tayari, kuhusu banda, mimi sipendi likiitwa banda napenda kuita sehemu ya kupumzikia *waiting bay*.Kwa kiingereza wana jina zuri sana lakini kwa kiswahili mnaita banda. Naomba nilitolee tamko rasmi tunaomba muda wa miezi sita Mungu akitujaalia ndani ya miezi sita tutakuwa tumeshaanza pale kazi na pengine tutakuwa tushamaliza, tunaomba mtupe muda msituzuie katika eneo hili naomba mtupe muda tunahangaika sana. Safari hii yako mambo mengi sana mapya tunamshukuru Mhe. Rais wetu mambo mengi sana mapya yapo, mambo yenye gharama kubwa safari hii tuliochukua moja wapo ni ugatuzi una gharama zake, *dialysis* kusafisha mafigo kuna gharama zake, mashine ya DNA iliyopigiwa kelele humu ndani sana na wengine kusema kwamba ipo melini bado hiyo meli haijafika safari hii pesa zake zimo, tuna kazi kubwa ya kuitafuta, kuifanyia kazi, kuitafutia eneo lake na kupata pia wataalamu wake.

Kuna hospitali ya Binguni kuifanyia *master plan* kujenga uzio. Kufungua mfuko wa Bima ya Afya tumepiwa bilioni 2 kazi kubwa, pesa unakuwa nayo lakini kazi kubwa kuanzisha ule mfuko.

Mhe. Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika 10.

Mhe. Waziri wa Afya: Kwa hivyo yote hayo ni mambo makubwa, moja wapo katika hayo mambo makubwa tunachukua na hili la banda. Tunachukua la *mortuary*, tumeshalitaja, tunachukua na *incinerator*, mambo matatu makubwa naomba nikupongezeni Waheshimiwa Wawakilishi yameibuka kutokana na majadiliano yetu. Nakupongezeni sana. Hii ndiyo kazi ambayo Baraza la Wawakilishi inayotakiwa kufanywa na sisi serikali, mnaibua vitu na sisi tumevikubali tunakwenda kuvishughulikia, tunakwenda kuvifanya. Nakuombeni mashirikiano yenu. Mkituzuia tutakuwa hatuwezi kwenda

kuyafanya hayo mengine. Nyinyi mtupe *supporter* kubwa zaidi na kutuwezesha zaidi.

Mhe. Spika, niliulizwa na Mhe. Mwantatu kuhusu *physiotherapy* nina waraka mzima wa *physiotherapy* na yule daktari pale kaja kutufanyia *presentation.* Naomba tufanye semina maalum pia kuhusu *physiotherapy* tutaunganisha na hizi semina zetu nyengine kwa Wajumbe ili muone kitengo kile kinafanya kazi gani. Kitengo kile kinatoa huduma za *clup foot* kwa ile miguu iliyopinda kwa watoto wadogo na mpaka sasa hivi wameshafanya *operation* zaidi ya 500 tokea kianzishwe kitengo kile. Sikuweza kuweka bajeti yake Mheshimiwa sio kama kudharau, sikuweza kuweka bajeti yake kwa sababu kuna vitengo vingi sana ndani ya Mnazimmoja. Ningeweka Bajeti ya kila kitengo mfano, Kisukari, mabusha, tezi dume, saratani, ningeanza kuweka bajeti ya kila kitengo au kila *section* iliyokuwepo Mnazimmoja hichi kitabu kingekuwa ukubwa wake mara mbili zaidi.

Mhe. Spika, naomba unikubalie bajeti yake imeingia katika *over role* ya bajeti ya Mnazimmoja zile bilioni 10 unazoziona na wao watapata, mishahara yao wafanyakazi wote ambao wewe unawajua na wanakuhudumia mishahara yao yote inatokea katika bajeti ya Mnazimmoja ni bajeti ya Serikali. Sitaki kusema kwamba hawapati bajeti kwa sababu mishahara pamoja na huduma zinazotolewa pale zinatokana na bajeti ya serikali, lakini tutaongezea fedha zaidi kwa ajili ya vifaa na ile miguu bandia, nakuahidi hilo tutaongezea zaidi. Wale ndugu zetu wa Uingereza tunaoshirikiana nao pia tutaendelea kuongeza mashirikiano zaidi.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala la chanjo naomba turudi tena katika ukurasa wa 80 na 82 katika vile viambatanisho. Palitokea kasoro kama miezi miwili mpaka mitatu ni kwamba zilichelewa kuwasili zile chanjo naomba nikiri hilo. Alipokwenda akaambiwa hakuna kwa sababu zilichelewa kuwasili na zile nyegine zinakuja katika mfumo maalum *refrigerated*.*S*asa panapotokea tatizo na Mhe. Abdalla Diwani wewe unaelewa mambo ya bandarini katika *refrigeration system* panapotokea matatizo na ikachelewa ndiyo hapo na sisi tunapopata tatizo. Kwa hivyo nikiri kwamba tulichelewa kidogo lakini chanjo zote sasa hivi zipo na zinaendelea kupatikana.

Mhe. Spika, pia lilizungumzwa suala la Tasakhta Hospital, kwa kweli mimi nawapongeza sana Tasakhta Hospital. Naomba nikiri kwamba taarifa hizo *specific* taarifa hizo nilikuwa sina. Ndio maana nikasema Waheshimiwa Wawakilishi wakati mwengine tusisubiri mpaka bajeti tupeane taarifa mapema, ungenipa mapema, ningeweza hata kuwaingiza katika kitabu cha bajeti yangu

nikawashukuru. Mahusiano tuliyokuwa nayo sisi, tuna mkataba nao sasa hivi wa kushirikiana tunawapeleka wagonjwa pale kwenda kutibiwa na sisi tunawalipa kama wengine na wagonjwa mpaka sasa hivi kama 9 wa serikali ambao ilikuwa waende India hatujawapeleka tumewapeleka pale. Wana daktari mzuri sana wa mifupa, wanafanya *operation* nzuri sana ya mifuga, mmoja wapo ni kiongozi wetu sisi ambaye mtu mzima alifanyiwa *operation* pale na *operation* yake ilikwenda vizuri, sitakiwi kutaja jina kutokana na maadili ya uuguzi maana Waziri wa Afya na yeye awe na maadili ya uuguzi. Tunawapongeza sana tutaendelea kushirikiana nao na tunaendelea pia kuwapa moyo kwa sababu kuwepo kwao ni msaada pia kwetu sisi, wanatusaidia. Kwa sababu wale wagonjwa wote wanaokwenda pale huwa wanakuja Mnazimmoja huko Mnazi kungekuwaje, kungezidi zaidi. Kwa hivyo wale waliokuwa wanajiweza wanakwenda kule wanatusaidia kwenye masuala ya *dialysis* tutashirikiana karibu kwa sababu wao wana *experience* wana *dialysis nurse* mzuri zaidi ambaye yupo na sisi wa kwetu wametoka kusoma tutaendelea kushirikiana nao na wao watapata *experience* ya kutosha.

Vitendanishi vya damu, hii kwenye mambo ya damu, namshukuru sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Lazima nikiri lile basi la damu baadhi ya taarifa, sio taarifa zote zinazokuja juu nyengine zinaishia huko. Sasa Mwakilishi anapoleta taarifa hapa na akaibua jambo zito kama lile, mimi nakupongeza sana Mhe. Abdalla Diwani naomba uendelee hivyo hivyo na Mwenyezi Mungu atakujaalia zaidi. Maana lile gari likitoka na wewe mkono wako una baraka zipo pale, kwa hivyo tumeshapata pesa na sasa hivi linashughulikiwa na litatoka hivi karibuni.

Mhe. Spika, maduka ya dawa yana leseni mbili mbali ya Manispaa na ZFDB. ZFDB sheria yao mbali kudhibiti sawa na Chakula na Vipodozi na Manispaa ni ile ya kuwepo pale biashara. Naomba tuendelee nazo hizo leseni kwa sababu ni leseni mbili mbali mbali. Wauzaji wa dawa zisizo rasmi wale watu wa siku ya Ijumaa wanaotandika baada ya Sala ya Ijumaa, wale udhibiti wake upo chini ya tiba asilia na tiba mbadala wataendelea kudhibitiwa. Hivi karibuni vile viringe tisa vimefungiwa tayari na wengi wamekuja pale kuomba, "Mheshimiwa tunaomba tufungulie". Nikawaambia hapana. Timiza masharti ufunguliwe, hizi ni pamoja na zile dawa za sunna, tunapofunga mjue kama tunafanya kazi hiyo.

Kituo cha Umbuji cha Mhe. Mohammedraza Hasanali naomba twende ukurasa wa 91, kituo hicho kimo katika kiambatanisho. Nilichokuwa sijakiweka hapo ni Kituo cha Miwani ambacho kinatakiwa kufanyiwa *repaired* kwa hivyo naomba kiingie.

Mhe. Viwa kituo chako Kiuyu Minungwini naomba uende ukurasa wa 91. Tumefanya kosa pale tumetia Kiuyu nyengine ile tumeisahau. Kiuyu ile itakwenda kwenye milele. Naomba nikiri kwamba kituo cha Kiuyu tulisahau kukitaja lakini kimo na tutakwenda kukutengenezea na usiwe na wasi wasi, nakuomba wewe na pamoja na Mhe. Mwantatu kuna ziara ya pamoja tutaifanya katika kituo hichi na Kiuyu na kitengo hicho cha *physiotherapy.*

Mhe. Spika, kuhusu kuvuja kwa paa la Mnazimmoja Mhe. Naibu Waziri amelishalitolea ufafanuzi. Tumeshaanza sasa hivi *repair* nadhani mmeona mabati yamezunguushwa pale Mnazimmoja *west wing,* mkipita leo tizameni mtaona mabati yemezungushwa. Tumeshaanza *repair* yetu *maternity*.

Mhe. Hamza Hassan Juma tumeshatoa mkataba kwa jengo la macho kwa sababu najua unalalamika sana Kwamtipura. Tumeshatoa mkataba pesa tayari tumeshapata mkandarasi ile *advance* ya awali imeshalipwa, Miranzi, aliyepata mkataba ule na katuahidi atakwenda kwa *speed* kubwa sana. Tumalize kule, kweli madaktari wanne (4) wa macho wanakaa chumba kimoja wanatia huruma kwa kweli. Halafu na wewe mwenyewe huduma zako hupati kutoa. Kwa hivyo naomba sana mtuvumilie tukishamaliza hivi tu huku kina *Doctor* Slim na wenzake watakuja, watahamia huku na nyinyi mtakuwa *free* kule na tutaendelea kushirikiana zaidi. Maana mnatusaidia sana ni lazima niwashukuru sana.

Mhe. Spika, mapato kuwa madogo yametolewa ufafanuzi. Lakini mapato yamekuwa madogo sehemu kubwa kwa sababu huduma nyingi tulizokuwa zamani tunachangisha sasa hivi tunatoa bila ya malipo pamoja na hizi huduma za *film* za *X-Ray* na kadhalika ndiyo maana mapato hayo yamepungua. Kuhusu kituo cha Kiuyu Minungwini nimeshaeleza hapo.

Kuhusu ghorofa ya tatu inavuja. Nimesema kuwa tumeanzia *maternity* tunakwenda kwenye jengo la macho, tukimaliza tunataka kulifanyia paa zima la Mnazimmoja lakini ni lazima tumalize nafasi ya chini kwa sababu wale wa juu tukiwale chini *temporary* tutakuwa hatuna nafasi ya kutosha. Ghorofa ya tatu inatumika sana na tunajaribu sasa hivi kukaa na wataalamu wetu maana lile paa liko juu sana, tulifanyie *repair* nusu twende nusu. Lakini wakati huo huo kuna mkataba mmoja wa *KuwaitFund* tumeshaletewa sasa hivi *draft,* kwa hivyo tupo katika *dilemma,* tuanze sisi wenyewe au tusubiri, maana tukisubiri na wao wanachukua muda mrefu *Kuwait fund,* BADEA pamoja na *Saud fund.*

Naomba niseme kwamba tuachieni tutakaa sisi kama Wizara, fedha zipo aidha tutaanza nusu ya huku wagonjwa wa hawa tuwahamishie huku halafu wengine

tuwa-*shift* huku, kama tunavyofanya *maternity* chini. Mmeona sasa hivi Mnazimmoja kuanzia kati pale tumeifunga nusu kwamba matengenezo pale yameshaanza. Wauguzi wachache, tumeshapata kibali kwa Mnazimmoja Wauguzi 180 tayari kazi ya usaili imeshaanza na tarehe 1 Julai wanatarajiwa kuanza kazi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa hitimmisha bado dakika moja.

Mhe. Waziri wa Afya: Haya nahitimisha sasa, naomba kuwambia Wawakilishi Wawakilishi wote pamoja na wananchi rasmi kuwa tumeanzisha kitengo kipya Hospitali ya Mnazimmoja kutokana na kero hizi katika utendaji wake wa mwanzo kabisa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuchukua hatua ya kero ambazo nyinyi mmezitoa tumenzisha kitengo kipya Hospitali ya Mnazimmoja na naomba nikitamke rasmi Mhe. Spika, mbele yako kitengo hichi kitajulikana kama kitengo cha huduma za jamii. Kitakuwa na wafanyakazi jumla yake sita na kitakuwa pale mbele kabisa ukiingia kwenye ule mlango Mkuu zamani watu walikuwa wakikaa sana upande wa kulia, ama zamani watu wa *computer* walikuwa wakikaa sana pale.

Mhe. Spika: Naomba utoe hoja Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Namalizia Mheshimiwa tu kidogo tu, naomba kidogo, pale kitengo hichi kitafanya kazi, naomba Waheshimiwa sasa watakuwa wanawasiliana na kitengo hicho moja kwa moja na nitawasilisha kwako kwa maandishi namba zao za simu. Mhe. Spika, nakushukuru nawashukuru Waheshimiwa Wawakilishi na nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kunipa *support* yao. Namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Kiongozi wangu, Mkuu wa Serikali katika Baraza la Wawakilishi. Sasa naomba kutoa hoja kutokana na hotuba pamoja na makadirio niliyowasilisha.

Naomba kutoa hoja rasmi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana ....

TAARIFA

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri akifanya majumuisho katika kuwataja waliochangia alitaja jina Mhe.

Mwantanga, tuweke *hansard* sawa katika Baraza hili hakuna Mheshimiwa anayeitwa Mwantanga.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa itarekebishwa kwenye *hansard* wataweka sawa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, wakati nilipochangia nasimama kwa Kanuni ya 63 nilionesha nia ya kutumia Kanuni ya 111 ya kuunda Kamati Teule. "Baraza linaweza kuunda Kamati Teule kwa ajili ya jambo fulani."

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa ya usubuhi ya leo, jambo fulani kwa mujibu wa Kanuni lipo. Jambo fulani lenyewe ni kwamba Serikali ya Zanzibar inajitahidi na tunamshukuru sana Mhe. Rais katika kuishughulikia Mnazimmoja ili iweze kuleta maendeleo. Kwa masikitiko makubwa pamoja na serikali kutoa pesa nyingi ili Mnazimmoja iweze kung'ara lakini huduma Mnazimmoja zinaonyesha kudidimia, wananchi wanalalamika.

Mhe. Spika, tulitegemea majibu Mhe. Waziri amejitahidi kujibu lakini majibu bado hajaturidhisha. Nitatoa mfano, tulitegemea kuambiwa jenereta litaungwa lini, lakini tumeambiwa jenereta hakuna mtaalamu wa kuungwa. Jenereta kubwa nchi hii ni jenereta la Airport na limeungwa na wataalamu wa ZECO. Majenereta kama yale mahoteli yapo matano sita na yameungwa na wataalamu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, tulitegemea kuambiwa vipimo wananchi dhidi ya kwenda kupima Al-Rahma, Kilimani, na hospitali nyengine, lini atafanya vipimo vipimwe Mnazimmoja, majibu hayo yatukuyatapa.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na taadhima kubwa kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar wakwezi na wakulima tunakuomba, tunakuomba Mhe. Spika, mtukufu wa Baraza hili leo tuunde Kamati Teule ili tuweze tukachunguze huduma inayotolewa Mnazimmoja haifanani na pesa zinazotoa serikali.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mheshimiwa ushatoa hoja naomba ukae.

Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri alipokuwa akijibu bahati nzuri sana jambo hili amelipa umuhimu mkubwa kwa sababu ameli-*address* mwanzo ameanza kujibu kabisa suala la Hospitali ya Mnazimmoja na nilikuwa

namsikiliza kwa makini sana. Ameeleza ukweli Waheshimiwa muda ambao tumekaa ndani ya hili Baraza ulikuja Mswada wa dharura hapa wa kuigeuza ile hospitali iwe Hospitali ya Rufaa. Muda hata hautajatosha vizuri tokea tuwape nafasi ile. Sasa hivi kwa *point* yako Mheshimiwa ni kwamba hata hicho tulichokifanya cha kupitisha Mswada hapa kuwa Hospitali kuifanya iwe ya Rufaa kwamba tumefanya makosa.

Sasa unachojaribu kushauri kwamba kushauri labda tuachane na ule utaratibu wa kwenda kwenye Rufaa turudi tena nyuma na hili nalo litahitaji sheria. Mimi sijashawishika Mheshimiwa ila nakuunga mkono kwamba tatizo lipo lakini pia namuunga mkono Mhe. Waziri kwamba tuwape muda waendelee kuliweka sawa hili. (*Makofi*)

Hata serikali ilipoleta kwa dharura, maana yake kwa ule umuhimu wake serikali imeleta Mswada wa Sheria kuigeuza Hospitali ya Mnazimmoja kuwa ya Rufaa sote tupo hapa. Dharura ile uharaka ule ni kwa sababu tatizo lipo. Mheshimiwa mimi kwa nafasi yangu kama Spika nisingependa kuchukua nafasi ya Waziri kuyajibu haya. Lakini ule uzito wake na maombi ya Waziri mwenyewe kwamba tuwachieni serikali tunauwezo wa kuyaweka sawa. Kwa sababu *concern* zetu mmezi-*address* vizuri sana, mengi mliyoyazungumza yako sahihi kabisa wala hayana matatizo na kayakiri wala hajakanunisha hata moja, yote ameyakubali.

Mhe. Hassan Khamis (Diaspora) nakuomba tuiwache serikali tuwape muda zaidi tuwaamini wamefanya haraka kuletwa Mswada wa Sheria. Nisengependa tuendeleze mjadala kwenye hili naomba mkae. Mhe. Hamza Hassan naomba urudi chini na Mhe. Hassan Khamis (Diaspora) naomba hili liishie hapa hili tuwape muda.

Baada ya hapo naomba nichukue nafasi hii sasa kuwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako tukufu limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya. Sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu ili twende tukafanye hiyo kazi. Ahsante Mhe. Spika.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU - H01 WIZARA YA AFYA

Kifungu PH0101 Programu Kuu ya Kinga na Elimu ya Afya
Jumla ya Kifungu 19,950,049,000

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakuona Mhe. Asha na Mhe. Dimwa na Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wakati nilipopeleka mchango wangu kwa maandishi kifungu cha HH01010106 ambacho kinachozungumzia Huduma za Afya za Uzazi na Mama na Mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kujua kwamba kwa sababu katika hotuba yake Mhe. Waziri alitupa ufafanuzi kwamba kuhusiana na vifo vya mama wajawazito pamoja na watoto waliozaliwa hai..

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hicho kifungu unachokizungumza kinazungumzia Huduma za Ufuatiaji wa Maradhi Yasiyoambukiza au vipi.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti kifungu ninachozungumza mimi kiko mwisho hapa chini, chini yake baada ya hili fungu kubwa programu ndogo....

Mhe. Mwenyekiti: Basi ni HH01010116.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ndiyo niliyosema.

Mhe. Mwenyekiti: Umesema 06 haya endelea Mheshimiwa.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti katika hotuba yake Mhe. Waziri alitwambia kwamba jumla ya wajawazito 20,893 ambao wamejifungua lakini watoto waliojifungua hai walikuwa 20,859 lakini katika hotuba yake hakutoa taarifa za vifo vya watoto wachanga nilitaka kujua kwamba katika mwaka 2016/2017 hakuna vifo vya watoto wachanga vilivyotokezea katika kipindi hichi. Lakini nilitaka kujua pia kwamba ukichukua idadi ya waliojifungua 20,893 na watoto waliozaliwa 20,859 ukitoa wanabakia watoto 34 lakini hapa hawakutuelezea hawa watoto 34 jee wamefariki, wameibiwa haijulikani idadi halisi ya watoto hawa wachanga, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri mambo ya *infant mortality*.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika kwanza namshukuru Mheshimiwa kwa ku- *note* hivyo na naomba kidogo tu niseme kwamba bajeti yake pia ipo katika 010101 ukiangalia ni Huduma Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto huku chini utakuta Huduma za Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto lakini utakuta zero lakini bajeti ya kifungu hiki ni hii iko juu 4.785 billion haya sasa katika takwimu Mhe. Naibu Waziri alizungumza hapa mwaka juzi *average ratio* ya vifo ilikuwa vifo 54 katika kila vizazi hai elfu 1000 mwaka jana tulipungua tulifika vifo 45 katika kila vizazi elfu 1000 tunaendelea kupungua *Alhamdulillah* mwaka huu mpaka sasa hivi tuko kwenye vifo 34 katika kila vizazi elfu 1000.

Kwa hiyo tunaendelea kufanya jitihada naomba Mheshimiwa elewe kwamba kuendeleza kupunguza sasa hivyo hizi idadi nyengine siyo inavyotakiwa hawa wanakwenda kila vizazi hai elfu 1000 wana *calculate* ndiyo *statistic* wanavyofanya hao. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuinipa ruhusa tena ni sawa na ndiyo maana nikasema kwamba nilitowa mchango wangu nikataka kujua suala hilo kwa sababu katika hotuba yake na hata katika kitabu chake hiki kikubwa hakuweka takwimu hasa halisi ya hawa watoto walifariki, lakini kwa sasa amesema kwamba 34 kwa sababu nimetaja. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba humu wameorodheshwa watu walifariki yaani mama wajawazito hao wako 27 na huku waliposema vifo vimepungua....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha ulipoandika huo mchango wako wa maandishi au ulipochangia majibu alitakiwa ayatowe sasa sitaki tuitumie *forum* hii sasa kumpa Waziri aanze kujibu hoja zenu kwa sababu hukumsikia kalitaja jambo, tuko kwenye vifungu vya fedha tujielekeze huko zaidi. Kama una jambo la kisera basi ulizungumzie lakini sasa hapa pasiwe pahali pa kuanza mjadala tena mpya hukunijibu hiki Waziri ili Waziri anyanyuke sasa ajibu maana yake muda haukunitosha nafikiri tuko sawa. Tunaendelea Mhe. Dimwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti nakushuru sana

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Doholo hukusimama kwanza kwa hivyo nafasi hiyo hutakuwa nayo Mhe. Dimwa .

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti mimi niko kwenye fungu HH01010106 Huduma za Ufatiliaji wa Maradhi Yasiambukiza, kwenye kitabu hichi kimekuwa na 30,000,000 makisio yake lakini kwenye fedha ya maendeleo hakuna kitu iko zero na kwenye kitabu hiki kidogo Mhe. Waziri ametuandikia mchango wa SMZ ni 96,000,000 lakini wa maendeleo ni 2,865,967,000 sasa nilikuwa nataka kujua kwa nini huku naona kama *confusion* atuweke sawa, lakini hoja nyengine ilikuwa kuna homa ya ini sijui inaingia hapa au vipi sijui naona kwa sababu sijaiona humu. Kwani jana tumesoma pale kwenye semina kuwa mradi ule hata hela humu haukuwekea kwa hivyo nilikuwa nataka ufafanuzi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dimwa waheshimiwa nisingependa Mheshimiwa mmoja achangie halafu nimtolee mfano yaani awe ni mfano wa watu wengine waige hiki ndicho kinachofanyika katika vifungu hiki anachokifanya Dimwa sasa hivi kwa hivyo kinakubalika kiko *valid* na Waziri unatakiwa sasa utowe maelezo tafadhali.

Mhe. Waziri wa Afya: Mheshimiwa nakuomba Mhe. Dimwa arudie ile *code* ya mwanzo sikuipata vizuri *code* ya mwanzo ile ya pili homa ya ina tayari.

Mhe. Mwenyekiti: Code ya mwanzo aliyoitaja ni HH01010106 Huduma za Ufatijiaji wa Maradhi ya Yasiyokuwa ya Kuambukiza, nafikiri sahihi Dimwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Mheshimiwa naomba nimwambie Mhe. Dimwa katika karatasi niliyokuwa nayo mimi hapa ambayo sio inakuwa ya Wizara ya Fedha kwasababu bajeti hii inapangwa katika mfuko wa programu na hizi *code* za Wizara ya Fedha. Sisi kiwizara ndani katika *code* ile ile tunakuwa na *breakdown* yetu kwa hivyo naomba nimsomee kifungu hiki H01010106 Huduma za Ufuatiliaji wa Maradhi Yasiyoyakuambukiza ndani yake ilichopangwa ni milioni 29,100,000 ambayo imegawika sehemu zifuatazo. Utoaji wa Mafunzo ya Vituo vya Afya milioni 14,248,000 kufanya ukaguzi wa afya za kinywa katika skuli za msingi milioni 6,306,000 na utoaji wa elimu ya afya juu ya maradhi yasiyo ya kuambukiza ni milioni 8,546,000 kwa hivyo hayo ndiyo *breakdown* yake nadhani ndiyo aliyokuwa anataka.

Kuhusu homa ya ini Mhe. Spika naomba nikubaliane naye kwamba ile homa ya ini haija- *appear* moja kwa moja katika *Global Fund Breakdown* kwasababu wale tunatumia zaidi *Global Fund* na *Global fund* ni maradhi matatu *Leprosy, TB* na *HIV Aids* sasa kuna *health support* mle mle ndani *component* maradhi yale mengine *Syphilis* mambo ya *Gonorrheal Sexually Transmitted Disease* kwa hivyo na hii *Viral Hepatitis* pia inachukuliwa kama *Sexual Transmitted*

Disease kwa sababu katika *population* ya wenye ukimwi hii inakuwa kidogo iko juu zaidi.

Kwa hivyo hivi majuzi tumefanya kikao na *Global Fund m*jini *Geneva Swiss* na Zanzibar tumewasilisha maombi yetu kwa ajili ya *Viral Hepatitis* na *Alhamdulillah* wametukubalia na wanakuja mwezi wa Julai wao mtaona kwenye TV maana tunachukuwa na kamera zetu tutambe kidogo, wanakuja mwezi wa Julai tutakaa nao pamoja na Mradi ule wa ukimwi mambao *Viral Hepatitis* pamoja na Benki ya Damu hili la Mhe. Abdalla Diwani pia naomba nimjibu kabisa pamoja na Benki ya Damu kuna *Component* ya *Syphilis* kaswende kwa sababu kila damu inayotolewa inapimwa kaswende pia na kule pia wanapima *Viral Hepatitis Component* zote zile tutazingiza humo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti nimemuelewa sana kaka yangu Mhe. Waziri wa Afya katika ile *code* yako moja ambayo ameisema lakini bado niko katika hili hili buku kubwa katika fedha za maendeleo hapa haikupangiwa kitu na wakati huku kuna pesa nyingi zilizopangiwa imekosewa na Wizara ya Fedha au wamekosea nani, kwa sababu haikupangiwa na hapa tupo kwenye kifungu cha matumizi nataka kujua hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. hebu wape *reference* ya kurasa kidogo maana yake.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Nilikwenda katika ukurasa ya H0H0130 katika vitu vya maendeleo na *Project* hii ya HIV, *TB* na *Leprosy* hapa imepangiwa kwenye maendeleo hakuna kitu hapa sasa nataka nijuwe vipi mbona hapa hapana kitu wakati huku kuna pesa nyingi zaidi ya bilioni 2,000,000,000 kwenye kitabu chao.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kuna fedha kama atakwenda kuangalia Mhe. Dimwa najaribu kutafuta kwenye kitabu ambacho zile za *donors* zimewekwa kule ndani kuna *component* ndogo ya fedha hizo, kuna fedha hapo katika hiyo bilioni 7,000,000,000 *component* hiyo ya maendeleo lakini haijakuwa *itemized* kwamba *component* ipi itakwenda.....

Mhe. Mwenyekiti: Mpe ukurasa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ukurasa wa 86 kiambatanisho namba 11 haijasema hamna *breakdown* kiasi gani kitakwenda huko hatika *Non Communicable Disease* lakini kuna *component* ambayo inakwenda kwenye *Non Communicable Disease* moja moja, mfano kikao kijacho tunaleta ile Sheria na

Sera ya Tobacco matumizi ya tumbaku *In Public Place Zanzibar* sasa hiyo inafadhiliwa moja kwa moja na *WHO* katika *component* ya *Non Communicable Disease and CD* ndivyo nilivyomuelewa hivyo Mheshimiwa. Kwa hivyo haiko wazi kiasi gani lakini inakwenda katika hizi *General Component* ya maendeleo hawa *donors*. Ahsante

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti sikusudii kabisa kuzuwiya fungu hili lakini Mhe. Waziri bado haeleweki kabisa na hapa hizi ni pesa nyingi ambazo tunazipitisha hapa. Sasa wasiwasi wangu mkubwa sana hajaweka wazi na hapa ndio kitu kinachoendelea sijui niamini vipi, niamini Mheshimiwa kapitikiwa, niamini au vipi ukweli sijui, tuendelee.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi lakini pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Afya lakini kidogo kabla ya mimi nilikuwa niko kwenye HH01010109 Huduma za Msingi za Matibabu ya Macho.

Mheshimiwa mimi katika kifungu hiki naona pesa iliyotengwa kwa sababu ya hii huduma ya macho milioni 28,000,000 Mheshimiwa kutokana na mahitaji yenyewe kwa sasa naona ni madogo sana ukitilia maanani kwamba sasa hivi huduma za macho wagonjwa wengi sana wanaokwenda hospitali wengi hawajiwezi. Kwa hivyo ningemuomba Waziri wa Afya kwamba kifungu hiki wakiongezee fedha kidogo ili wale wananchi wetu masikini, ambao wanakwenda pale kupimwa macho waweze kupatiwa na miwani kwa sababu mahitaji haya sasa yamekuwa ni makubwa sana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa unapendekeza pesa ziongezwe.

Mhe. Omar Seif Abeid: Pesa zitoke kwenye HH01010105 naona hapa kwenye kinga kwenye Huduma za Kuimarisha Kinga kwa Jamii fedha ziko nyingi tu za kutosha unaona moja katika kinga hii ya macho pia nayo ni kinga, kwa hivyo mimi napendekeza hapo kidogo papunguzwe paongezwe hapa. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti namkubaliwa Mhe. Omar wala halina wasiwasi lakini nataka kumwambia kwamba pesa hizi nyengine anazoziona huku pia nazo zinatumika katika huduma za macho. Mfano Huduma za Kuimairisha Kinga kwa Jamii Mradi huu wa *Trachoma* vikope tunatoa pesa huku, kwa hivyo pesa nyengine bila ya kuonekana hapa lakini inatumika tayari katika huduma za macho. Kama ataangalia ukurusa wa 83 wa

kitabu cha bajeti ataona mwaka jana tulikuwa na bajeti ndogo sana lakini tuliweza kutoa huduma nyingi sana kwa sababu tulishirikiana na wenzetu wale nilowashukuru, *X-Server*, *Site Servers* na *Lions Club International* ambao wote tunashirikiana nao katika miradi hiyo. Kwa hivyo naomba atukubaliye kwamba kifungu hiki twende nacho lakini kitatoka katika kifungu hicho chengine cha 05 alichosema Kuimarisha Kinga kwa Jamii mambo kama vikope na mengine yataingia huko kwenye macho. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mheshimiwa nashukuru sana kwa hilo kwa jibu nililolipata nimeridhika naomba tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku kwanza hukuwepo umeingia sasa hivi nimewataja watu ambao watazungumza hapa wewe hukuwepo kuna mwenzio ambaye amenyanyuka kwa naye kwa utaratibu kama huo wako hivi punde tu naye ni Mhe. Doholo nikamwambia hapana twendeni kwa utaratibu unanyuka pale tutakapotaja halafu nitakutajeni wote, tueendee.

Kifungu PH0101 Kinga na Elimu ya Afya 19,950,049,000

Kifungu PH0102

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza, Mhe. Bi Panya, Mhe. Suleiman Makame Ali, Mhe. Jaku, Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Masoud Abdurahman, Mhe. Mtumwa Peya.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kupata ufafanuzi zaidi ingawa Mhe. Mwenyekiti, sikuridhika kabisa na ile hatua leo uloichukuwa.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kurejea lakini kanuni zetu ukiangalia kanuni ya 111(2) hoja ya Mhe. Hassan ilikuwa...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ilikuwa ile hoja tumeshaifunga jielekeza kwenye vifungu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya ahsante sana lakini hoja ile ilikuwa haitaki kujadiliwa ilikuwa tuulizwe hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, bado narejea hoja yangu ile ile ya kutaka kuunda Kamati Teule ingawa hapa Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa muongozo wako hatuwezi tena kuunda kamati teule lakini tunaendelea kukwambia kwamba hatujaridhika kabisa na utendaji ambao unafanyika katika Hospitali ya Mnazi mmoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza...

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nakuja katika hilo fungu nishajua unakonielekeza, Mhe. Mwenyekiti, maneno yote ya Mhe. Waziri pale inaonesha tatizo ni fedha lakini mimi nikiangalia Mheshimiwa kifungu HH01020107 hapa katika bajeti ya mwaka huu tuliyoipitisha ilikuwa karibu bilioni 8.452 lakini katika bajeti inayokuja hapa tuna bilioni 8.855 sasa hiki kiasi cha fedha ambacho alichokiongeza haionekani kabisa kama pale hayo mabadiliko tunayoyataka nayo alituahidi kama yataweza kutekelezeka.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, pale ndio kimbilio letu sisi wanyonge kwa hivyo mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti Mhe. Waziri atwambie ukweli, amekusudia vipi kuboresha Hospitali ya Mnazi mmoja na hoja yangu zaidi moja anapokwenda pale tunaambiwa mtu hospitali ya rufaa katika kijiji, anakwenda pale damu anaambiwa akachunguzwe kilimani sijui mkojo akachunguzwe kilimani, pale wagonjwa wanakwenda *gloves* hapana tumepitisha mwaka huu mpaka katika kitabu chake Waziri anatuambia ameshaingiziwa karibu bilioni 2,000,000,000 leo mtu pale anaambiwa *gloves* hamna, bendeji hamna, vipimo vyote hamna hospitali za binafsi leo zina vipimo hospitali ya rufaa hamna Mhe. Mwenyekiti, mimi bado sijaridhika na fungu hili na sitolipigia kura.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma kuna maeneo ambayo tunaweza kwenda kutembelea pamoja tukaangalia kilichokuwepo baada ya kumaliza bajeti, na yeye akaeleza ya kwake tukaangalia pamoja na wataalamu wangu wakawepo. Lakini katika kifungu hiki naomba niseme kwamba tumetengewa fedha safari hii hizi 8 billion alizotaja, ambazo kwa mara ya kwanza tumeingiziwa pia fedha za saratani, mbali ya vifaa vyengine. Kuna fedha ya chanjo, kuna dawa muhimu na vifaa tiba hivyo alivyovitaja 4.589 billion, kuna vitendanishi vya maabara na huduma za uchunguzi, mionzi, ikiwemo *MRI, CityScan* na *X-ray* 1.2 billion…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri *point* ya mheshimiwa ni kwamba fedha hii haitoshi, nafikiri ungejielekeza katika huko…

Mhe. Waziri wa Afya: Mheshimiwa naomba fedha hii ndio tuliopata *allocation* tuifanyie kazi hii, na naamini huko mbele tunakokwenda tutajua nini cha kufanya wakati huo tunazungumza na *donors*. Huo ndio uwezo uliokuwepo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba Mhe. Hamza akubaliane kwamba mara hii bajeti ya wizara hii imeongezeka, na imeongezeka kwa asilimia 35.91, na ni bajeti ambayo ya tano tuna karibu mafungu 45, hii ni ya tano kwa kupata fedha nyingi katika mgao wa mwaka 2017/2018. Inawezekana hizo fedha anavyoziona yeye ni kidogo, lakini kwa mujibu wa fedha tuliyonayo basi tumezingatia kweli kweli na ukitizama kwenye bajeti ya wizara imeongezeka kwa asilimia 35, lakini kwa hospitali ya Mnazi Mmoja peke yake kwa zaidi ya asilimia 20 ya bajeti ya mwaka 2016/2017. Kwenye hizi fedha za vifaa na dawa ni bilioni 8, ndani yake dawa peke yake na vifaa bilioni 7, lakini kuna bilioni 1 ya chanjo na kuna nyengine karibu milioni 500 kwa ajili ya shughuli nyengine ambazo tumetenga kwa mafunzo ya madaktari.

Kwani bajeti nzuri, tunakwenda vizuri hali yetu ni vizuri, lakini pia tumekaa juzi tukazungumza na uongozi wa hospitali, tumezungumza pia na bodi kwamba tutakaa pamoja kuangalia mapato ya hospitali ya Mnazi Mmoja na kile ambacho kinapewa kwa sasa hivi tuweze kujua *gap* iko wapi. Kwa hivyo, kiutaratibu wa bajeti mimi ningemuomba sana Mhe. Mwakilishi akubaliane na hiki kilichopangwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, pale pana matatizo mawili, pana tatizo la uingizwaji wa fedha na matumizi ya hizo fedha zenyewe, na sisi kitu tulichokuwa tunataka kwenda kukichunguza matumizi ya hizo fedha zenyewe. Sisi tunapokwenda pale tukaambiwa hiki hakuna, hiki hakuna ukiuliza Wizara ya Fedha unaambiwa pesa walizoomba ndio zile zile walizopewa. Lakini mimi ili kwa sababu huko tumeshatoka sasa mimi naomba Mhe. Waziri aniahidi kitu kimoja. Je, kuanzia lini wananchi wetu wakienda hospitali ya Mnazi Mmoja hawatoambiwa waende Kilimani wakafanye vipimo, wala hawatoambiwa wanunue *glove* na *bandage*?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri *commitment*.

Mhe. Waziri wa Afya: Mimi mheshimiwa nimekuomba hapo awali na namuomba tena Mhe. Hamza Hassan Juma tukimaliza bajeti hii tufanye ziara ya pamoja yeye, bohari pamoja na Mnazi Mmoja tukae na wataalamu wangu ataeleza *concern* zake na wao watamueleza vitu vyote vilivyokuwepo atapata kuthibitisha. Sitaki kusema kwamba watu sasa hivi wanaambiwa moja kwa moja waende huko, wanakwenda pale panapokuwa na mapungufu, hilo nakubali na nilikubali hapa na nakubali tena. Lakini tukimaliza hapa twende pamoja atazame atakwenda *point by point* namkaribisha tutakwenda pamoja ataona kila kilichokuwepo na kilichokuwa hamna pia ataona.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mimi nikutahadharishe tu maana yake *concern* hizi ni za wajumbe wengi, yaani hiyo ahadi unayompa Mhe. Hamza utajikuta unanyanyuka unawapa na wengine ahadi kama hiyo watakuwa ni wengi. Mimi nashauri sana waheshimiwa tujitahidi sana kuiweka sawa. Kumbe *point* ya Mhe. Hamza fedha zinatosha isipokuwa *result* za matumizi ya pesa zile ndio tatizo. Nashukuru sana tunaendelea. Mhe. Hamza vipi?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ilikuwa bado kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Naam! Nilifikiri umeridhika Mheshimiwa, haya tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Unajua Mheshimiwa tatizo hapa ndio tunapitisha bajeti na wananchi wetu wote wanasikiliza. Je, leo tutaambiwa vipi kwa sababu hii ni kauli ya wananchi, mheshimiwa mambo madogo madogo sana kipimo cha mkojo twende tukapime Kilimani? Kipimo cha damu, mimi Mheshimiwa hiyo ziara anayoniambia twende tukafanye, mimi nimeshafanya. Nimekwenda kule *Laboratory* tunaambiwa zile *kit* zinazopelekwa huyo *supplier* aliyeambiwa apeleke hayo madawa anapeleka asilimia 20, *reagent* hakuna. Lakini huku unaambiwa keshapaleka ndio maana tukasema mbona haya matumizi ya fedha zinazotolewa na serikali, fedha nyingi lakini kinachopelekwa pale ni kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri hili…

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, maelezo anayoyasema Mhe. Hamza Hassan Juma ni ya msingi ni kweli wananchi wetu wanapata matatizo pale ambapo wasipopata huduma kutoka hospitali yetu kuu ya Mnazi Mmoja, ndio maana tukasema sasa serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya itasimamia kwa karibu sana kuona mambo haya yanakwenda vizuri. Nataka tulipokee hili lalamiko ili tukae tuone ni kwa namna gani tatizo hili litaondolewa, kama fedha zinafika lazima zitumike vizuri, zisimamiwe vizuri ili kupunguza shida ya wananchi wetu. Tunalolifanya katika eneo hili ni kuweka usimamizi wa karibu ili wananchi wetu waepukane na tatizo ambalo serikali inaweza kulifanya. Fedha za serikali ni za umma zinahitaji kutumika kwa utaratibu mzuri, hivyo tunamuahidi Mhe. Hamza atupe nafasi serikali na Wizara ya Afya tuliangalie kwa umakini zaidi ili fedha zitumike vilivyo ndivyo zisaidie wananchi wetu na tatizo liondoke. Namshukuru sana Mhe. Hamza kwa kueleza kwa kina jambo hili. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri samahani, unajua nadhani walichokihitaji ni *commitment* ya serikali, kwamba kwa sababu fedha hizi zinaonekana kumbe zinatosha katika kununua hivyo vifaa na ku-*supply* maeneo tofauti. Je, wananchi watakapokuwa wanakwenda maana ndio nafikiri ndio lilokuwa la msingi, watakuwa hawaelekezwi sasa kwenda kuchukua vipimo kwengineko ambako wanapaswa kulipa au dawa zitatolewa bure? Yaani nafikiri sijui umenielewa vizuri Mheshimiwa, cha msingi kilichopo lakini sasa inaonekana kuna uoga wa kuji-*commit.*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa nimekuelewa sana, sisi hatua yetu ya kwanza ni kuwashughulikia wale ambao wanaharibu hizi fedha. Hatua ya pili ni kuhakikisha hicho Mhe. Mwenyekiti, ulichokisema kwamba fedha hizi zinatumika ipasavyo ili zikidhi mahitaji na wananchi wapate huduma zao. Kwa hivyo, tunachotaka kwenda kukifanya ni kuhakikisha je thamani ya fedha inatumika vilivyo ndivyo, serikali itachukua hatua hiyo ione ili wananchi wetu wasipate matatizo, nia na dhamira ni kuondoa matatizo. Kwa hivyo, lugha anayosema Mhe. Hamza ndio lugha tuliyonayo lazima tuhakikishe je fedha hizi tukichukua kusema kwamba fedha hizi zitamaliza matatizo yote kwa wakati huo lipo tatizo hapo. Inawezekana Mhe. Hamza anasema fedha hizi zinamaliza matatizo yote, inawezekana kumbe bado zinahitajika zaidi, lakini kwa mara hii bajeti zimetoka hizi. Msimamo wetu ni kwamba tutakwenda kuangalia kwa kina ili kuhakikisha wananchi wetu wasipate bughudha na matatizo ya kupata huduma za afya wanapohitaji kufanyiwa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mimi nadhani serikali ingeji-*commit* hebu undeni *team, very seriously team* halafu mkayachunguza haya halafu mje muya-*report* hapa, kwa sababu tunafika pahali yaani mnatuweka katika wakati mgumu.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa natoa majibu ya ufafanuzi nilisema kwamba Wizara ya Fedha tayari tulishakutana na Wizara ya Afya, na tulikutana na uongozi wa hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na bodi na tayari tumeunda timu ya wataalamu, na timu hii kazi yake na majukumu yake tuliowapa ni kuangalia matumizi yote ya hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini wakati huo huo kutizama na mapato wanayoyapata ndani ya hospitali ya Mnazi Mmoja, ili tuangalie kama kuna *gap* kutokana na mahitaji yao halisi. Kilichopangwa sasa hivi ni bajeti, sasa kama kutakuwepo na mahitaji ya ziada ambayo tunaweza tukaya-*justify* kwa pande zote mbili na katika hilo tutajua kama kuna fedha zinakwenda lakini hazitumiki ipasavyo basi hiyo kamati

itatueleza na itatoa ushauri serikalini. Kwa hivyo, serikali itajua nini la kufanya baada ya kamati hiyo kukamilisha kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza ushazungumza mara tatu nafikiri unaona na hiyo hali halisi ilivyo, naona waziri anakutizama usoni, naam.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Waziri wa Fedha na katika mtu ambaye nina muamini sana, sio mawaziri wengine siwaamini, ninamuamini kweli kweli. Sasa mimi nilikuwa naomba kitu kimoja kwa sababu sisi hukuturuhusu kwenda lakini nitaomba kamati yako ya wenyeviti kabla kukaa na Bajeti Kuu ya Serikali tukae na Mhe. Waziri wa Afya, Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na uongozi wa hospitali ya Mnazi Mmoja tuzungumze kwa kina tuelewane na tufahamiane kabla hatujaja kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Kwa sababu hayo ambayo Mhe. Waziri wa Fedha anayoyasema serikali tunajua nyinyi shughuli zenu ni siku zote, sisi hapa tukishaondoka mpaka miezi mitatu ndio tunakuja tena. Sasa sisi haja yetu kama kuna tatizo la fedha kabla hatujapitisha Bajeti Kuu ya Serikali tuangalie wapi tutaweza kufanya ili tuondokane na mzigo wa watu wetu kuwahangaisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nashukuru sana, mimi mheshimiwa nimekusikia na muongozo wangu ni kwamba bahati mbaya sana hatuna Kamati ya Wenyeviti, kuna Kamati ya Uongozi ndio ambayo inakusanya Wenyeviti wote, lakini bahati nzuri tuna Kamati ya Bajeti nadhani ina siku mbili za kufanya kazi kabla ya kusomwa kwa Bajeti Kuu ya Serikali. Sasa kamati hiyo ndio kazi yake hasa hii, haya ambayo mnayazungumza nafikiri Mwenyekiti bahati nzuri yupo hapa basi kamati yake ndio itapaswa kukaa na serikali kwenda kufanya hizo kazi ambazo unazishauri, na Mwenyekiti wake makini tu Mhe. Mohammed Said Mohammed nadhani itaweza kufanyika. Mimi nakubaliana na wewe mheshimiwa. Tunaendelea.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii lakini kabla ya kuanza nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake kubwa anazozichukua katika kuhakikisha afya njema juu ya wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimuomba Mhe. Waziri aweze kushirikiana na Makamu wa Pili wa Rais kutuwekea suala zima la kituo katika Baraza letu hili, ukizingatia ndani ya Baraza hili waheshimiwa tupo lakini kila mmoja kiafya wenzangu nadhani wanaweza wakakubaliana na mimi, kila mtu ana tatizo lake…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Bi. Panya ungetutajia na kifungu ambacho unakizungumzia…

Mhe. Panya Ali Abdalla: Kifungu kilikuwa HH01020104 ambacho kinasema *upgrading* Mnazi Mmoja, katika hili kwa sababu tumeona hospitali yetu ya Mnazi Mmoja tunataka iwe hospitali ya rufaa ili kuondosha huo msongamano wa kwenda pale na sisi Waheshimiwa Wawakilishi tunaitumia sana hospitali yetu ya Mapinduzi Mpya ambayo tunakwenda kutaka huduma pale tunawakuta wazee wetu wapo wengi kwa ajili ya kupima *pressure*. Sasa tunapokwenda sisi pale kama tunakwenda kuwazonga kwa sababu tunapoonekana waheshimiwa huwa tunapewa ile hadhi ya uheshimiwa ili tuweze kupita haraka haraka, lakini ni kitu ambacho sisi kinatusononesha kuona mzee wako kaja tangu asubuhi yupo hapo na anaumwa halafu wewe upite.

Sasa Baraza nimuombe Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Makamu wa Pili wa Rais tuweze sisi kuekewa kituo chetu hapa kiweze kutuhudumia sisi Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na watendaji wetu hapa ili kupunguza huo msongamano katika hospitali ya Mnazi Mmoja mpaka kwa lile jambo ambalo litakuwa kubwa kabisa ndio tuweze kwenda huko. Lakini kwa haya matibabu madogo madogo tuweze kupatiwa hapa hapa katika Baraza letu la Wawakilishi, hivi sasa hivi tunayo *First Aid* hapo lakini bado huduma zake ni ndogo sana hata ile *bed rest* pia hapana…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tunashukuru usihutubie twende kwenye hoja, tushaisikia ule msingi wake kwa hivyo tumuache waziri kwanza akupe majibu halafu utaongea baadae.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Inayohusu hapo hapo Mnazi Mmoja sijui kama naruhusiwa tena kuipitisha hapa hapa au…

Mhe. Mwenyekiti: Ngoja tumalize hiyo kwanza.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na hoja ya Mhe. Bi. Panya wakati *Budget Session* ikiwa zinaendelea hapa sio *First Aid* tu pale tuna *very senior staff* ambao wanatoa hizi huduma pakitokea lolote lakini wakati huo huo Waheshimiwa Wawakilishi wanakaribishwa kwenda kupima afya zao, kwa sababu wana vifaa vyote wakati wa *budget session*. Wakati hakuna *Budget Session* wale *staff* wanakuwa hawapo hapa kwa sababu kile kituo sio *permanent* kinafunguliwa wakati wa Baraza la Wawakilishi *session*. Kwa hivyo, wazo lake ni zuri na tutajitahidi tuweke vifaa vya ziada ili

Waheshimiwa Wawakilishi wawe wanaweza kupata huduma zaidi ya hiyo huduma ya *Firs Aid*. Ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru lakini nimuombe sana Mhe. Waziri kwa sababu sisi kuhudumiwa hapa ni tayari tumeondosha msongamano kule katika hospitali ya Mnazi Mmoja kuacha wazee wetu waendelee kutibiwa vizuri. Na nimuombe tu pamoja na hiyo *Firs Aid* ambayo katuekea niombe kama kuna uwezekano atuwekee vitanda pale vya mapumziko japo kimoja kwanza kiwepo kwa dharura kwa sababu saa nyengine hapa inaweza kutokezea *emergence* alau akapelekwa mtu hapo kimapumziko kidogo halafu baadae ukafanyika utaratibu mwengine. Kwa hivyo, kwa hili namuomba sana Mhe. Waziri aweze kulijali na kulithamini kwa sababu wenzetu Bungeni tumeona huduma zote zinapatikana pale pale katika Bunge bila ya kumtoa mtu nje anapata huduma pale na anaweza kurudi hapa kazini kwake akaendelea na kazi.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimesikia na nimekubali. Ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kuhusu hospitali ya Ndagoni, kituo cha afya…

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu gani?

Mhe. Suleiman Makame Ali: Nipo kwenye kifungu cha HH01020101.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumza kuhusu kituo cha afya cha Ndagoni, kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa kukubali kwa sababu kile kituo cha afya alikwenda kukifungua yeye. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akinijibu amenambia kwamba kijana yule anayejitolea pale atampatia kijichombo sijui kama ni vespa au pikipiki au *met*. Lakini sasa Mhe. Mwenyekiti, tangu kuanza Mapinduzi ya 1964 sasa hivi Ndagoni watu wanamiliki gari, wanamiliki vespa na vitu vyengine vya usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, Ndagoni hakuendeki kwa hali ya barabara, sasa leo Mhe. Waziri akiniambia kwamba atampa chombo ili kuweza kufika pale ni bora angeniambia ningeridhika zaidi kwamba atajenga nyumba ya daktari pale na

kuniongezea madaktari pale ili kuhakikisha kwamba huduma ile inapatikana kwa kila wakati. Lakini sasa utakapompa yule daktari chombo cha pikipiki mvua imenyesha na Ndagoni hakufikiki atafikaje kwenda kutoa huduma hii.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Suleiman wakati wa risala inasomwa pale siku ya ufunguzi wa kituo kile waliweka wazi kwenye risala na mbele ya Mhe. Mkuu wa Wilaya wa pale kwamba wanahitaji nyumba ya daktari ili yule daktari aliyejitolea asiwe anapata shida ya usafiri na kutokana na hiyo hali ilivyokuwa ya barabara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuombe Mheshimiwa kwamba hilo tuliweke kwa mwakani kwa sababu hawa wenzetu wa Milele na *ORIO* safari hii tushawaomba vya kutosha. Vituo vya kutosha pamoja na nyumba za daktari pia zimo na hili kwa sababu limekuja sasa hivi na ufunguzi umefanyika juzi juzi tu pale Kisiwani Pemba. Kwa hivyo, naomba kwa mwakani tuingize hilo, kwa hiyo habari ya chombo sasa na-*cencell* tutaingiza hiyo nyumba mwakani. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru majibu ya Mhe. Waziri mwakani hauko mbali ni kesho asubuhi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, lakini sasa nataka anipe majibu ya huyu kuongeza daktari pale wacha yule daktari moja atuongezee daktari pale, kwa sababu tayari mwakani nakubali kwa jengo sawa, na mimi nikipata pesa za mfuko wa jimbo naahidi kutoa ili kuanzisha hilo jengo. Lakini sasa nataka suala la daktari atanifanyia utaratibu gani, kwa sababu daktari aliyepo ni mmoja na anakaa mbali.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuombe tena Mhe. Suleiman kwa huduma tunazotoa pale imeonekana daktari yule mmoja anatosheleza na ana wasaidizi wake wawili na wao bahati nzuri hawaumwi sana watu wa eneo lile kwa hiyo *Alhamdulilah* nashukuru.

Kwa hivyo, aliekuweko huyo daktari anatosha, pale tatizo lao kubwa ambalo pia alizungumza katika risala ni ajali zinazotokea baharini za vyombo kupinduka, ndio mara nyingi matatizo ya pale. Lakini huyi daktari aliekuwepo sasa hakuna foleni na mara nyengine anakuwepo pale hata mgonjwa mmoja hapati yaani hapati hata mteja mmoja na ndio tunavyoomba hivyo Mnazi Mmoja wakipungua watu sisi tutafurahi zaidi.

Kwa hivyo, Mheshimiwa kwamba kwa sasa hivi aridhike na mwakani tutaangalia nini tutaweza kufanya.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sijaridhika sana lakini mimi nimwambie kwamba daktari mmoja hatoshi kwenye kituo cha afya chochote kile. Kwa sababu kama alivyosema yeye mwenyewe kwamba daktari yule hakai pale anakaa sehemu mbali Vitongoji. Mhe. Mwenyekiti..

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hilo limeshafahamika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile na yeye pia amenambia mwakani na mwakani nimejibu kwamba mwakani si mbali. Mheshimiwa mimi nasema tuendelee mwakani utafika nikija kumuuliza asijenambia tena mwakani, hapo hatutakubaliana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpe pole Mhe. Waziri vikao jana vilikuwa vingi BLM huko na sasa hivi na shughuli zake na jana usiku akakesha kucha kujibu hoja za Wawakilishi, pole sana Mhe. Waziri na ndio ukubwa huo.

Mimi langu dogo tu ni yale yale ninayorudia elimu yangu mimi ni ndogo nataka kuelimishwa. Tulipitisha sheria hapa unanisikia waziri...

Mhe. Mwenyekiti: Nukuu kifungu kwanza halafu twende.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Tupe hicho kifungu ambacho unachotaka kuzungumzia hapo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu Mhe. Mwenyekiti, SH01020104 Mnazi Mmoja Hospitali nafikiri tuko sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tulipitisha sheria na Mwanasheria Mkuu alikuwa mkali hapa ndio nikasema wakati mwengine maneno mengine binaadamu aweke hakina asije akamaliza kuyatoa yote ni wasia huo. Tulihoji sana Wawakilishi hapa Mnazi Mmoja. Mimi nataka kujua inajitegemea haijitegemei na kama inajitegemea kwa nini ikawekewa pesa hizi 9.8 maana yake huko wananchi wanatusikiliza na wanatufahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Nimeshakufahamu hapo *point* yako iko vizuri tu. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye sheria katika kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub ile sheria inasema ni *semi-autonomous*. Kwa hiyo, *semi-autonomous* ukitafsiri kwa kiswahili inajitegemea na ndio maana bajeti yake wanapata wao moja kwa moja na anaesimamia bajeti hiyo imendikwa chini kwenye kitabu ni Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazi mmoja na 10 bilioni hizo ndio maana sisi tuko kwenye 72 uki-*plus* na hizi 10 *point some thing* inakuwa 83 zinakwenda moja kwa moja Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo inajitegemea kwa kiwango kikubwa sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sikutaja milioni kumi bilioni tisa laki nane thamanini na tano. Nimeuliza tumepitisha sheria na sheria ni msumeno tunahimizwa siku zote. Kwa nini tukapitisha sheria wakati Mnazi Mmoja hapana. Leo tunaziombea pesa hapa Mhe. Mwenyekiti.

Tumepitisha sheria hapa hapa ndani na Mwanasheria Mkuu namkumbuka aliinuka mzima mzima hapa tukamuhoji tunakwenda na Mwenyezi Mungu haya hapa leo tunayaona hatima yake leo. Sheria hii inamuhusu nani? Waheshimiwa walikuwemo akina Mhe. Mohammed Said Mohammed alikuwa mkali kweli kweli Mhe. Mwanasheria Mkuu tukahoji kutoka kuisaidia serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Ngojea akujibu huyo huyo Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Itakuwa vichekesho Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ngoja akujibu yeye Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wakati tulipokuwa tukipitisha ile sheria kwenye *financial provision*. Fedha ambazo zitapewa Mnazi Mmoja ni fedha ambazo zitaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, pamoja na kwamba wao wanajitegemea lakini bado mapato yao yanatoka serikalini. Kwa hivyo, fedha zao ndio hizi ambazo ziko hapa zinaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, wao wanajitegemea lakini bado sio shirika kusema wao wanafanya biashara fedha zao zinatokana na biashara ambazo wanazifanya. Wao bado wanatoa huduma bure lakini kinchotakiwa na wananchi kupitia sheria ile ni kuchangia baadhi ya huduma na ndio maana fedha nyingi zimewekwa kwenye Mnazi Mmoja kwa sababu kiasi kikubwa cha huduma kinachotolewa pale ni

fedha zinazoodhinishwa na Baraza kutoka kwenye bajeti hii ya serikali. Nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwenye hichi kwenye kipengele cha *up grading* ambacho unazungumza hichi kipengele ambacho unakizungumza wewe Mnazi Mmoja wana fungu lao. Yaani bado suala lako liko *valid* lakini bado hatujafika huko iliko hiyo Mnazi Mmoja yenyewe ndio ziliko hizo pesa zenyewe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, niko katika kuhoji mapato na haya ndio mapato yenyewe Mheshimwa na naelewa mimi si mgeni wa hivi Mhe. Mwenyekiti, nimo katika kuhoji mapato, kabla yatujafika huko mbele, safari inaanza hatua moja kwenda mbele. Sheria Mwanasheria Mkuu labda nimsomee hiyo sheria yenyewe pengine kaisahau tuliyopitisha.

Tumepitisha sheria namba 3 ya mwaka 2016 hebu kaitafute sheria Mwanasheria mie elimu yangu ndio ile ile ndogo, tumepitisha sheria hapa tukahoji waachieni wakala kama Muhimbili wakusanye hizi pesa watumie wao wenyewe. Leo tunataka ku-*up grade* hapa na Mhe. Bi Panya Ali Abdalla kuna fungu hapa Mhe. Mohammed Abuod, Mhe. Balozi Seif Ali Idd Mhe. Spika, mwenyewe ndani pesa chungu nzima zinataka kuwa *up grading* nikasema loo! hii ni hatari. Unajua nakumbuka vizuri Mhe. Mwenyekiti, mkanita ndani kule pesa nyingi kumbe ni *typing error* sasa hii tunafanya nini.

Mheshimiwa hii wizara inataka kusaidiwa kwa hali na mali Rais anafanya kazi kubwa sana kama ....

Mhe. Mwenyekiti: Wache serikali wakupe majibu Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Huku tunapitisha sheria na namba 3 iko wazi. Hasa tukitaka kuja kumbana Mheshimiwa itakuja kuwa vichekesho sheria inajieleza wazi Mwanasheria Mkuu alikuwa mkali hapa tukasema iachineni. Sasa leo anakuja kugeuza shilingi upande wa pili aitafute sheria inamuelezaje na *hansard* zipo .

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mheshimiwa anachozungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni pale ambapo baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walihoji kwenye *retention* kama Mnazi Mmoja hivi kwenye fedha ambazo zinakusanywa basi wao waachiwe nadhani na Mhe. Hamza Hassan Juma na yeye alikuja kwenye

percentage akasema basi angalau asilimia 30% waachiwe iwe inazunguka kwenye mfuko wao na sisi tulichowaambia kwamba kiasi kikubwa cha fedha cha kuendeleza Mnazi Mmoja Hospitali bado kinatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kweli serikali.

Kwa hivyo, hakuja haja ya wao ku-*retain* kwenye fedha ambazo wao wanapewa kiasi kikubwa na serikali. Ndio maana tukaomba kwamba waachiwe fedha hizi ziendelee bado kutoka serikalini na ndio tutakubaliana na tukapitisha ile sheria ndio maana hapa tuko kwenye kupitisha hayo mafungu ya fedha hizo. Kama ya fedha hizi pamoja na kwamba Mnazi Mmoja inajitegemea lakini utegemezi wake kwa kiasi kikubwa bado inategemea fedha ambazo zinatoka serikalini wanapokwenda wananchi pale Mhe. Mwenyekiti, huduma ambayo ni sera ya Chama cha Mhe. Mohammed Aboud huduma za wananchi ni bure, kinachotakiwa kufanywa ni kuchangia baadhi ya huduma. Lakini kwa kiasi kikubwa fedha nyingi za kuendesha Mnazi Mmoja Hospitali zinatoka serikalini na ndio maana tunapitisha haya mafungu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hichi kitu kiko wazi wala hakitaki tochi....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tutakuwa tushamaliza umeshaongea mara tatu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa kanuni zinaturuhusu tupige kura basi hapa sheria mmetupa wenyewe hapa kanuni tufike pahali tutumie japo nikawa peke yangu lakini tujenge hoja. Siwezi kustahamili kama hivi...

Mhe. Mwenyekiti: Unataka kupiga kura ya kitu gani Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hii wizara Mhe. Mwenyekiti, inanikosesha usingizi mimi nahangaika mimi kufanya kazi ...

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuitafuta hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub lakini kama ni suala la fedha nilisema wakati ule na kwa dhamira ile ile aliyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwamba serikali inatenga fedha kwa ajili ya Mnazimmoja peke yake. Mwaka jana tulikuwa karibu na bilioni 8.6 lakini kwa mwaka huu 2017/18 zimepangwa bilioni 10.38 ni ongezeko la asilimia karibu 20.62 kwa dhamira hiyo hiyo. Lakini Mnazi Mmoja wanakusanya mapato yao, lakini *on top of that* serikali inatoa milioni mia moja kila mwezi na tulichokubaliana kwamba tufanye uchambuzi wa yale mapato ambayo wakusanya wao wenyewe na kile kinachotoka serikalini

tutizame kama kuna upungufu ili serikali ifanye mazingatio kwa lengo hilo hilo. Lakini suala la kupandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja nalo pia linafanyiwa mkakati maalum kwa maana tunazungumza na washirika wa maendeleo akiwemo *BADEA* na *Kuwait Fund* kwa ajili ya ku-*up grade* hospitali ili iweze kuwa ya rufaa.

Kwa hivyo, jitihada zinafanywa na namuomba Mhe. Mwakilishi akubaliane na jitihada hizo hizo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae ushamaliza. Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa naomba nifahamishwe maana sheria tumepitisha sote.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae, tafadhali *please.*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Huko kote anajizongwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nakuomba ukae, *please* Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kiti kutubena zaidi katika hili maana yake sheria zinakiukwa.

Mimi nasimamia katika kifungu cha SH01...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa unaanza kwa kunituhumu baada ya kwenda hoja, subiri. *Please* tafadhali Mheshimiwa

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mheshimiwa naendelea..

Mhe. Mwenyekiti: Taratibu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Nakwenda katika kifungu cha SH01020102 Huduma ya Utoaji wa Damu Salama.

Mhe. Mwenyekiti: Haya endelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Hapa nimeona kwamba kuna makisio ambayo 2016/17 iko hii hapa. Lakini 2017/18 hakuna wala 2018/19 hakuna. Je tatizo nini ina maana hizi huduma itakuwa imekufa itakuwa haipo tena huduma kwa sababu hizi ndizo changamoto ambazo wakati kule nachangia nilisema hata pesa za kujikimu wale watu hawana.

Je, katika mahesabu haya mimi sijenda skuli nifahamishwe ili niweze kuridhia.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa Mhe. Abdalla Maulid Diwani kuliona hilo na mimi bahati nzuri hapa nilikuwa nimeshaliandikia katika mpangilio mzima pesa zao hawa milioni mia tatu na hamsini zimo katika kifungu cha H01020101 yaani *general* Huduma za Hospitali za Wilaya na Hospitali za Rufaa kwa sababu gani kwa hawa *blood bank* wanapata pesa zao kutoka ile *distribution* inakwenda kwenye hospitali zote, kwa sababu kila hospitali wanaweka *branch* yao na ruzuku nyengine safari hii watapata kutoka ile *Global Fund* katika fedha za *Global Fund* ndio tumewaombea.

Kwa hivyo, *total budget* yao waliopata *allocation* benki ya damu Huduma za utoaji damu salama kwa wagonjwa ni milioni mia tatu hamsini kwa mwaka huu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana unajua ingeandikwa hapa tusingekuwa na nguvu hata za kuhoji. Lakini kwa sababu haijandikwa hapa yeye kanifunga funga tu kwamba atatoa katika kifungu cha S01020101. Lakini bado hivi sasa wamewekewa hizi pesa na changamoto kadhaa namwabiwa siku hadi siku. Kwa sababu mimi na *group* yangu *G1* tunafanya zoezi la kuchangia damu nchi nzima hii nakumbana nayo. Imefika *time* kule hata zile pesa za kuchukua wale madaktari wanaotusaidia tunatoa sisi mfukoni mwetu.

Sasa unambie kwamba kifungu hichi kinakuja kutolewa katika kifungu cha juu yake Huduma za Hospitali za Vijijini na anasema kuna benki kule sio kweli bado. Naomba sana aniridhishe katika maelezo yake vizuri sana ili nifahamu zaidi kwa hii mimi sijafahamu bado. Kwa sababu naona hajanipa majibu yenye kustahiki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kwa nini ziko huku zisiweko hapo anaposema.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, huo ni mfumo wa *coding* wa Wizara ya Fedha sisi tunapopeleka Wizara ya Fedha ndio inapanga hizi *coding*

na hizi *title* vifungu vyote vinapangwa katika hii progamu *base* bajeti. Mimi ninazo karatasi zangu huku ambazo zina-*itemize* zote na benki ya damu Sebleni inasema milioni mia tatu na hamsini kutoka serikalini na fedha zilizobakia zinatoka kwa wafadhili wa maendeleo kupitia Mfuko wa *Global Fund* takribani milioni mia sita kwa ajili za zile *reagent* na *testing na kits* nyengine. Kwa hiyo hii ni utaratibu uliokuwa umepangwa wa kitabu....

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mheshimiwa hivi vitabu vinatoka Wizara ya Fedha na hapa *point* yake haipo kwenye pesa za wafadhili. Nafikiri *point* yake iko kwenye hizi pesa zetu sisi wenyewe hizi za kawaida hizi ambazo zimo kwenye hivi vitabu.

Kwamba kiasi hicho mgekiweka hapa kikaonekana bado yaani mngekipunguza huku mkakiweka hapa bado ile *total* haibadiliki nafikiri ndio *point* yenyewe na ndio hapo sasa mnaifanya Kamati ya Bajeti iwe *active* yaani kwa kuwa wanafanya wao Wizara ya Fedha wasitu-*confuse* basi waweke kwa mujibu wa hivi vitabu, maana yake wasiwe na *code* zao ambazo Baraza hatujui halafu tunakuja kupitisha vifungu kumbe *code* ziko za siri ndio msingi wake. Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Waziri kwanza hizi *code* huwa tunazifanyia marekebisho kila katika kipindi na nyengine tunazifuta kabisa kuna nyengine tunaziongeza kufuatana na mahitaji. Sasa kama kuna *code* ambazo zinafanana ni vizuri ile *code* moja ikapungua kwa mfano kama hapa kuna Huduma za Hospitali za Vijijini Wilayani na Hospitali za Rufaa. Lakini ukija na huku kuna huduma ambayo umei-*single out* huduma moja. Sasa ni vyema zote ukazi-*fuse* katika kifungu kimoja katika *code* moja na hicho ndicho kilichofanyika na kama alivyosema Mhe. Waziri ukitizama bajeti ya 2016/2017 kuna 7.5 lakini hii ime-*double more than* karibu 100% ime-*increase* kwa sababu ya kuingiza hicho kifungu katika *code* hii. Mhe. Mwenyekiti naomba kukaa.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi ningeomba Kamati yangu ya Bajeti hebu lifanyieni kazi na hili ili kuweza kuliweka sawa mtakapokaa na serikali. Mhe. Abdalla Maulid Diwani bado unaendelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana nashukuru sana. Pamoja na maelezo ya Dokta lakini hata kile kifungu nilichokinukuu mimi yeye kaikosema yeye kasema 7.5 ambayo iko chini. Mimi nilizungumza cha juu yake pale kakosea. Umakini kidogo samahani.

Sasa mimi katika hilo ningeomba *commitment* yake Mhe. Waziri kwa sababu wale pale Benki ya Damu wamekaa kama watoto yatima yeye ni shahidi mimi nimeshakuwa nae pale na najua jitihada zako katika taasisi ile, kwa nia safi kabisa silipwi mapenzi yangu tu kwa sababu napenda serikali yangu isilaumiwe katika ile. Tumeweza kuchangia damu mikoa mitatu ya Zanzibar, tumeona changamoto zao inafika *time* hata ile pesa ya kuondokea pale *over time* hamna na hapa kwenye programu yao hakuna kilichoandikwa kwa ajili ya 2017/18. Alisema kwamba itaandikwa huku juu ananithibitishiaje?

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na yale mawazo yako ya Kamati ile ya Bajeti si *mind* kwa sababu ikiwemo hapa *total* itakuja vile vile ndicho hichi kifungu anachokitaja Mhe. Abdalla Maulid Diwani kinachoishia na 102.

Mimi naomba nimuhakikishie kwenye *Global Fund* nimeshiriki kwenye mkutano na nimehakikisha kwamba wao wanajaza zile *component* zao za *reagent* na *test kits* zinazofanyiwa kwa damu wao wenyewe *direct* .

Naomba nimthibitishie tena wakati napitia bajeti hii kamati mbali mbali najua umakini wake, najua umahiri wake, najua jinsi anavyosimamia na hamu yake ya kuchangia damu ambayo inawaokoa watu wengi maisha Zanzibar basi nimehakikisha kwamba zile milioni mia tatu na hamsini kamati ya bajeti ikiamua kuziweka hapa basi sisi tutafurahi zaidi na tutakuwa hatuna tatizo.

Lakini naomba nimuhakikishie kwamba milioni mia tatu hamsini zimetengwa na mie nitalisimamia hilo kuhakikisha kwamba pesa hizi zinafika kitengo kile na yeye anajua mimi miko karibu sana na kitengo kile. Ahsante.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasimamia kifungu SH01020101 Huduma za Hospitali za Vijijini Wilaya pamoja na za Rufaa.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilipokuwa nachangia nilizungumzia suala zima la Hospitali ya Mbuzini na bahati mbaya kama ilivyosahaulika kwenye bajeti na hapa Mhe. Waziri kalisahau. Sasa pale palikuwa na ahadi ya Mhe. Rais kuwa hospitali ile iwe Hospitali ya Wilaya na akaagiza ifanyiwe kazi mara moja.

Lakini sasa hivi tunaingia mwaka wa nne agizo lile la Mhe. Rais halijatekelezwa.

Nilisema kuwa kuna Mhe. Waziri kateuliwa na Rais Katibu Mkuu kateuliwa na Mhe. Rais, lakini na Wakurugenzi wote wameteuliwa na Mhe. Rais. Lakini hapa limetolewa agizo na Mhe. Rais karibu sasa hivi miaka minne yule aliempa agizo Mhe. Waziri wa Afya kwa wakati ule hakutaka kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ungeenda kwenye hoja yako yaani usijenge hoja kwa kutuhutubia.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ndio Mheshimiwa yule aliepewa agizo kwa wakati ule waziri Juma Duni hakutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kulitekeleza agizo la Mhe. Rais. Lakini bahati nzuri kipindi hichi kuna Mhe. Mahamoud Thabit Kombo ambaye yeye anatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa mwaka jana hopsitali ile ilionekana imo katika kitabu. Lakini mwaka huu kaitoa kabisa sasa nataka atuambie au amwambie Mhe. Rais agizo lile alilolitoa Rais atalitekeleza lini au pale Mhe. Rais kenda kudanganya wananchi?

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna jengine nilipeleka kwa maandishi ....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hilo la mwanzo tu kwanza halijakaa sawa. Kwa sababu mimi nalifungunisha na vifungu vya fedha hapa maana yake sijui unakusudia kusemaje. Wewe unataka ahadi maana yake unaturejesha tena kwenye hotuba zile mlizokuwa mkihutubia mmeshajibiwa na waziri unataka tena waziri asimame hapa akupe ahadi.

Mhe. Mjumbe zungumza na mimi, Mhe. Machano mwache huyo kwanza aongee na mimi huku.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kujua tu Mhe. Waziri hiki kituo cha Mbuzini kwa kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais atakitekeleza lini.

Mhe. Mwenyekiti: Bado. Lakini Mhe. Waziri hebu msaidie kidogo labda, bado Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa kutoa hoja yake nzito kwa kweli. Ni kweli ahadi ya Mhe.

Rais, safari hii tulipopata *allocation* ya hospitali za vijiji na wilaya lilikuja hili wakati tunajadiliana bajeti, na *allocation* tunapata kwa fedha maalum. Kweli safari ile tuliweka katika bajeti lakini safari hii hatukuweka, fedha zile ilibidi tuweke kipaumbele na kipaumbele kutimiza ilani hiyo hiyo ya Chama cha Mapinduzi ilikuwa Binguni, kwa sababu imetajwa moja kwa moja kwenye ilani. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe atukubalie fedha hizi tunakwenda Binguni kwa ajili ya *master plan survey* na kujenga ukuta ule wa uzio. Kwa hivyo, naomba atukubalie tunaendelea kuzungumza na wafadhili wetu wa maendeleo, sikuitaja moja kwa moja kwa sababu hakukuwa na *commitment* ya moja kwa moja. Ahadi ya Rais iko pale pale na mimi naendelea kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu lile limetajwa tumeipa kipaumbele, lakini haina maana kwamba hii hatujaipa kipaumbele. Nitaendelea kufuatilia naomba Mhe. Mjumbe atuvumilie, nitaendelea kufuatilia na mara tu nitakapompata mfadhili eneo la mwanzo tutakapoelekea ni kule, kwa sababu safari hii vipaumbele vilikuwa vingi kidogo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Unajua Mhe. Masoud Abrahman msingi wangu mimi ili tusirudi tena kwenye hotuba, angalau ungeuliza kuhusiana na hizi fedha zilizokuwepo hapa kama zinagusa hicho kituo chako ambacho unaulizia ambacho ilikuwa ni ahadi ya Rais. Ingekaa vizuri zaidi kuliko kwamba Rais alisema halafu unamtaka Waziri akupe uhakika. Naam, tuendelee.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana Mhe. Waziri katika kifungu hiki alipata bilioni 7.58 na mwaka huu kapata shilingi bilioni 15.36 ni ongezeko kubwa sana kwa kutekeleza hii ahadi ya Rais anao uwezo huo. Mimi nataka aniahdi ni lini atakwenda kutekeleza ahadi ya Rais Mbuzini.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa unaona ilivyokaa sawa sasa kuliko pale mwanzo. Sasa hivi iko vizuri tu. Mhe. Waziri naomba umjibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa fedha hizi zote tumeshazipangia tayari katika maeneo yale. Mimi namuomba Mhe. Mjumbe anivumilie kama nilivyomuomba, sisi tunakutana na wafadhili kila siku wanakuja wafadhili mbali mbali wa miradi mbali mbali hata hao wa Milele wanakuja kwa ajili ya miradi mipya, *ORIO* tunaendelea kuwasiliana nao sasa hivi, hivi karibuni Mwanasheria Mkuu tunatarajia kusafiri naye tena kwenda kuzungumza na baadhi ya wafadhili kusaini na mkataba ikiwezekana kwa ajili

ya *Mental Hospital* pamoja na huko Binguni kwenyewe, kuna maelekezo yameshatolewa tunakwenda nayo.

Kwa hivyo, naomba sana watatokezea hawa na tutaweza kufanikisha la Mbuzini hatujaliwacha, *study* yake ipo na ramani zake zipo, *feasibility* ipo, pamoja na *costing* zake zote na kitabu kizima cha Mbuzini. Naomba atuvumilie.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa maelekezo yake, lakini mwaka jana Mhe. Waziri aliniambia Milele wanajenga hospitali nne Pemba, wakirudi wanakuja kujenga Mbuzini kwenye Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Milele *allocation* yao ilikuwa kwa ajili ya ku-*repair*, huku Mbuzini tunataka kuweka *District Hospital* hilo ndio agizo la Mhe. Rais, Hospitali ya Wilaya. Binguni Rufaa, kasema wilaya iwekwe kule. Katika yote hayo tunayofanya anayajua yeye Mhe. Rais kwamba hili agizo lake lipo bado na tunaendelea kulisimamia na hivi sasa tutalifanyia kazi.

Kwa hivyo, mimi ninachoomba ni uvumilivu kwa sababu Binguni kule ina *deadline* yake katika *timeframe* ya ilani pia ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe kuvumiliana ndio kawaida. Kwa hivyo, akiendelea kunipa muda tutaendelea kumjulisha tumefikia wapi. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mtumwa Peya. Mhe. Masoud Abrahman mara tatu umeshamaliza basi.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru kwa majibu yake mazuri, lakini atambuwe kama Mhe. Rais anasikiliza hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Masoud Abrahman, umeshamaliza mara tatu imetosha, naomba ukae. Mhe. Mtumwa Peya.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi niko kwenye fungu la PH01020201 kuhusu Huduma za Uchunguzi. Nilipokuwa nikichangia kwa maandishi nilizungumzia masuala ya wafanyakazi wa Kitengo cha Damu Salama hususan wafanyakazi wa maabara wanaochunguza masuala ya damu. Wafanyakazi hawa hawajalipwa mafao yao ya *overtime* kuanzia Januari mpaka hivi sasa. Nimuulize Mhe. Waziri wafanyakazi hawa katika hiki

kifungu kilichotengwa hapa je, na wao watalipwa mafao yao au ni lini watalipwa mafao yao haya ya *overtime*.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kuhusu malipo ya mafao ya wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo awe *clear*, wafanyakazi wepi hao aliokusudia.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Kitengo cha Damu Salama wale wa maabara wanaochunguza damu, wanadai *overtime* zao tokea mwezi Januari hawajalipwa hadi sasa, nilitaka kujua ni lini watalipwa *overtime* zao hizi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hilo nitalisimamia sikuwa na taarifa nalo kwa sababu halikuwemo katika mchangio, lakini nitalisimamia kulifuatilia ili walipwe mara moja kama wanadai fedha zao. Ahsante.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, lilikuwemo kwenye mchangio wangu wa maandishi, labda hukuwahi kulifanyia kazi. Lakini nitaomba Mhe. Mwenyekiti, nitamuomba Mhe. Waziri suala hili aje anijibu kwa haraka tena kwa maandishi nilipate na niweze kujua wananchi hawa ni lini watapatiwa malipo yao.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mchango wake niliupokea wakati niko pale kwenye meza, dakika ya mwisho kabisa.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa. Lakini naomba ulifanyie kazi tafadhali. Tunaendelea Waheshimiwa Wajumbe.

Kifungu PH0102 Huduma ya Tiba 37,096,228,000

Kifungu PH0103

Mhe. Mwenyekiti: Naanza na Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mhe. Hamad Abdalla Rashid, Mhe. Ali Khamis Bakar, Mhe. Omar Seif Abeid na tunamalizia na Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Kwanza nikushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kwenda katika kifungu moja kwa moja cha Utawala na Uendeshaji. Katika kifungu hicho kidogo katika mchango wangu nilichangia suala zima la kadhia ya wafanyakazi wa hospitali ya Mnazi Mmoja ambao, na nimezuwia hili la waziri nalielezea kidogo ili mantiki ipatikane, kidogo tu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kuna viongozi ambapo *level* ya viongozi hawa ni ya wizara, najua Mnazi Mmoja iko mbele, lakini nazungumza *level* ya wizara katika *commitment* ya kuwawajibisha viongozi hawa wa hospitali ya Mnazi Mmoja. Wafanyakazi wanaingia kazini wanaandika majina na wanaondoka kwenda kutumikia hospitali binafsi, ambapo sehemu ya hao viongozi ni hospitali zao, nilisema katika mchango wangu.

Lakini nikushukuru sana Mhe. Waziri katika majibu yako na ulikiri kuwa mlikuwa juu muda mrefu sasa hivi mtashuka chini. Sasa katika hii kushuka chini nataka *commitment* ya wizara, hawa viongozi wa hospitali ya Mnazi Mmoja mkishashuka chini katika utaratibu ambao ulisema mwenyewe, nini *commitment* ya serikali katika kuwawajibisha wote watakao kwenda baada ya huko kushuka chini, huku nyuma nataka tuwache wakifanya takadhia hii.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Miraji Khamis kwa kuliuliza hilo na kunipa fursa ya kutoa ufafanuzi mzuri zaidi. Ufafanuzi wa awali katoa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwamba serikali imeshagundua hilo imeshafanya uchunguzi na ripoti zake zipo kwa watu wetu wahusika. Mimi pia wakati najumuisha pale nilisema hatua husika zitachukuliwa mapema iwezekanavyo na tutafanya mabadiliko makubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe atupe muda tumeshawajua wengi wao, wameshafuatiliwa nyendo zao na hospitali zao zinajulikana huko wanakotibu na wanakowaambia wagonjwa wakati mwengine njoo kule. Sio kwa sababu hakuna dawa Mnazi Mmoja au hakuna vifaa tiba, au hakuna vitendanishi anapeleka biashara wapi hospitalini kwake, tumeshawajua na hatua hizo zitachukuliwa mara moja, kama alivyotamka Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na mimi kutoa hilo tamko.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Kwanza nimshukuru tena Mhe. Waziri na mawaziri wote ambao walichangia kwenye eneo hili, lakini nilikuwa nasoma sehemu moja ile ya katiba ya Zanzibar, kuwa moja ya jukumu la waziri ni kumsaidia na kumshauri Rais katika masuala ya kuendesha serikali. Sasa naomba wajibu wenu huu, mimi hili fungu naliachia la Utendaji na Uendeshaji, mwende katika mantiki mazima ya kumsaidia Rais, msimuonee muhali mtu hatufiki basi.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii. Niende moja kwa moja kwenye fungu dogo HH01030106 Usimamizi wa Rasilimali Watu na Huduma kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilitoa mpaka mfano wa kitaalamu hapa, kuhusu kila mfanyakazi na sehemu yake husika. Namshukuru Mhe. Waziri katika majibu yake ameeleza wazi kwamba wana nia ya kuajiri kampuni ya kusimamia usafi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini nimsaidie tu, mimi najua kazi ya usafi wa hospitali kuna magenge mawili. Moja *special gang* na ndani ya wodi ni *Health Orderly*.

Mhe. Mwenyekiti, inaonekana dhahiri na leo nimefurahi kupata jibu kwamba wahusika wa juu sasa watateremka chini. Inaonekana dhahiri kwamba usafi wa hospitali unapotea kwa sababu ma-*orderly* tunawapa kazi ambazo sio zao, ndio pale niliposema tunataka *appropriate person at appropriate place.* Ma-*orderly* wetu sasa hivi ukenda hospitali, *orderly* anaachiwa kazi ya kutandika kitanda nasema sio yake, *orderly* anapewa kazi ya kugawa chakula nasema mimi sio kazi yake, *orderly* anapewa kazi ya kugawa chakula nasema mimi sio kazi yake, *orderly* anapewa kazi ya kufunga kidonda sio kazi yake, *orderly* anaachiwa kutia *drip* sio kazi yake, *orderly* anaachiwa kuzalisha sio kazi yake. Kazi ya *orderly* ni usafi wa hospitali, sasa usafi unapotea hapa *orderly* ukishampa kazi nyengine ambazo sio zake na wala haruhusiwi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe nenda kwenye hoja yako uliyokusudia.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Hoja yangu iko hapa. Katika huku kuajiri kampuni, na nilitoa angalizo jana hapa, tutakapoajiri hii kampuni ya usafi, naomba waziri anifahamishe usafi huo wataufanya ndani ya mawodi au nje ya mawodi hospitali na kama watafanya ndani ya wodi ya hospitali tunajipanga vipi kwanza kuwakinga na maradhi hawa wafanyakazi wa kampuni, lakini pili kuweza kujua *ethics* na *etiquettes* za wauguzi ili kuweza kutunza siri za wagonjwa wetu ndani ya mahospitali *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri naona ni jambo la kisera tu zaidi.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Naomba nimjibu Mhe. Gerei yeye ni mtaalamu bingwa wa masuala ya *nursing* na *mid wifery* au *mid husbandry*.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Gerei atenganishe kazi za *orderly* ndani ya wodi na kampuni itakayofanya usafi mazingira yote ya hospitali. Kampuni ya usafi itakuwa katika hospitali *premises, orderlies they will be like work attending the cleanness in the ward*. Nadhani amenielewa Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Mwenyekiti, nilivyofahamu katika michango ya malalamiko ya wawakilishi wengi huu usafi hasa hususan ni uchafu ndani ya mawodi, na narudia tena nje ya mawodi bado kuna wafanyakazi wengine *special gang*, hao ndio *special* kwa kusafisha nje ya mazingira ya mahospitali, ambao tayari serikali imewaajiri wapo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa narudia tena hawa ambao ni kampuni nakubaliana naye kwamba wafanyekazi nje ya mazingira ya mawodi, humu ndani ya mawodi je. Narudia kusema kwamba nampongeza waziri kwamba sasa wale wahusika, nasema tena kwamba tatizo kuna muhali wa kushindwa kusimamia, ambao nampongeza Mhe. Waziri amekubali kuwateremsha sasa wakubwa kuja chini.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili liendelee kusimamiwa, haiwezekani Hospitali ya Mnazi Mmoja ishindwe na Global Hospital kwa usafi hata siku moja. Namuomba Mhe. Waziri au namuunga mkono kwa hili kuwateremsha wafanyakazi wake chini. Lakini kubwa ni muhali uondoke, wafanyakazi wetu ma-*orderly* hawasimamiwi kufanyakazi zao ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana kwa ushauri wako, nafikiri serikali itautekeleza. Mhe. Doholo.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilichangia kwa maandishi. Mhe. Mwenyekiti, nilimuuliza Mhe. Waziri kwamba kwa nini hospitali za serikali tunapata mashaka kwa .....

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu gani unaongelea.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe. Mwenyekiti, hicho hicho alichosema Mhe. Gerei, na mimi nimesimama hicho hicho.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nikikutaja jina lako.....

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe**.** Mwenyekiti, nimesimama kwa kifungu....

Mhe. Mwenyekiti: Subiri Mheshimiwa nikikutaja jina lako wewe uanze kujiandaa na hicho kifungu, ili nitakapokupa sasa usimuoneshee kidole mtu kwamba kama alivyozungumza Mhe. Gerei.

Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo: Mhe. Mwenyekiti, kifungu HH01030106.

Mhe. Mwenyekiti: Haya endelea sasa.

Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo: Nilipokuwa nikichangia Mhe. Mwenyekiti, nilipeleka kwa maandishi nilimuuliza Mhe. Waziri kwa nini vituo vya afya vya serikali matumizi ya Bima ya Afya tunakuwa tunapata mashaka, tofauti na utumiaji wa Bima za Afya kwa sekta binafsi. Nilitaka majibu lakini hakunijibu, kwa hivyo naomba anijibu kwanza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kwa sababu unajua ninapokuambia ukinukuu hiki kifungu, wewe ukishamaliza kukitaja tu mimi nakwenda kwenye zile pesa, halafu sasa nakusikiliza, unachokitaka kwenye fedha hizi ni kitu gani ndio msingi wake, ndio maana nakusisitiza kitaje hicho kifungu halafu mimi nakwenda kwenye fedha. Wakati mwengine unakitaja pana sifuri, kama alivyokuja Mhe. Abdalla Maulidi Diwani kasema hapa kwamba kifungu kipo lakini pesa hakijatengewa kwa nini, ndio msingi wenyewe huu, ndio maana unakitaja.

Sasa wewe unakitaja pesa zipo lakini unazungumzia jawabu ya Bima ya Afya ambayo hakukujibu waziri. Sehemu hii ya Kamati ya Matumizi inahusika zaidi na mambo yanayohusu matumizi, kwa hivyo ni mambo yanayohusu fedha au sera. Nitakusaidia sasa hivi kwa kumruhusu Mhe. Waziri akujibu, lakini sitokupa nafasi nyengine, akujibu tu hapa Mhe. Waziri halafu baadae tuendelee na mtu mwengine. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kifungu hiki kina-*take care of,* yaani kitafanyia kazi hayo aliyoyaelezea na huku kwenye vifungu vidogo vidogo ambayo nayo *itemise*, nitaweza baadae kuwasilisha kwako wewe *itemise* ya kifungu hiki ili jambo hilo alilosema Mhe. Mjumbe pia linafanyiwa kazi ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Mhe. Omar Seif Abeid, Mhe. Jaku Hashim mwisho.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi. Mimi nasimamia fungu SH010303 Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kujua serikali ina mpango gani wa kulimalizia lile jengo la *Theatre* pale Micheweni katika *Cottage Hospital* ya Micheweni, kwa sababu nimeona kwenye bajeti ongezeko la fedha liliopo hapa ni kama milioni 25 tu kwa mwaka huu kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa napendekeza kwamba serikali au wizara iwaongezee watu wa Pemba fungu la fedha kutoka kwenye HH01030209 au

hilo la chini yake la 011, kwa sababu ile *theatre* ni kitu muhimu sana na imeshafikia asilimia 80 ya ujenzi wake ili kukamilika likaweza kutoa huduma na kuwapunguzia tatizo wananchi wa Wilaya ya Micheweni. Mhe. Mwenyekiti, naomba serikali kwa hapo ituhurumie iongeze fungu kwa wizara Pemba ili waweze kukamilisha lile jengo na liweze kutoa huduma.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe nimekuelewa lakini sasa huko ulikopendekeza zitolewe pesa, kwanza kifungu hicho cha 09 hamna kitu kitupu. Halafu hiki kifungu chengine cha 011 ni Uandaaji na Uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mjumbe amekwenda kwenye kifungu hiki, lakini hoja yake tayari tumeshapita iko kwenye zile hospitali za vijiji na wilaya. Kule ziko pesa za kumalizia hiyo *theatre* yake ambayo nimeitembelea na kuna mchango mkubwa wao pia kamati ya Jumuiya kwa hivyo zile ziko kule huko sio, huku Uratibu na utekelezaji wa hizi shughuli za Wizara nzima katika Idara hii ya Mipango.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikutoe wasiwasi kidogo hii bajeti kupita itapita…..

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Seif sijakuruhusu kuendelea kwa sababu tumeshapita huko na umehakikishiwa kwamba huko tulikopita hiyo fedha ipo ndio maana sikakupa tena tuendele Mhe.Jaku endelea tu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikutoe wasiwasi hii bajeti kupita itapita *challenge* wacha ziwepo kidogo…..

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwanye vifungu ulipata nafasi ya kuhutubia wakati huo tulikupa nafasi dakika 20 usituhutubie hapa *please*, njoo kwenye kifungu tufanye kazi tuondoke Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti unawalinda sana hawa…..

Mhe. Mwenyekiti: Siwalindi mimi mimi niko na nyinyi, Mheshimiwa siwalindi…..

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Unaona Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kafurahi anacheka pale anafurahi…….

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hebu fanya hiyo kazi nenda kwenye kifungu hicho kumbe huna tunaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ninayo Mheshimiwa hoja yangu utachagua nina mawili kifungu hichi hichi utakuja kunako HH01030102…….

Mhe. Mwenyekiti: Haya anza na hicho.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Halafu chengine utachagua moja katika hizo kuna SH100302 ….

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nisikuchagulie mimi wewe mwenyewe ndio mwenye hoja mimi sijui unataka kuongea nini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Basi nitakuwa katika Utaratibu, Mipango, Sera na tafiti za Wizara katika Sera na Utafiti, Mheshimiwa hapa nakuomba sana kwa unyenyekevu wa hali ya juu na huruma ya juu sana kwa lugha nyepesi kabisa mwezi huu, nataka busara zako na hekima zako, hili nimekusikiliza sana Mhe.Spika, hata nikazungumzia kwa lugha hii Mhe. Spika, nataka unifahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye hiyo hoja usinibembeleze.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kama kuna pahali paliponikosesha usingizi mimi lile banda la wagonjwa kafafanua waziri lakini kwa uzembe wa Wizara na nitakuthibitishia kuwa Wizara wazembe wala usijali, nitakuthibitisha nimeshaifanyia kamati hii huko nyuma mwalimu wangu yule pale Jidawi nilimuuliza kutoka Bohari kuu Maruhubi kuja Mnazi Mmoja unachukua siku ngapi, sikiliza vizuri Mhe. Spika, ninavyokuja na hoja hiyo maana hapa nataka nizungumze kwa ludhga sijawahi kuzungumza humu ndani……

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa usihutubie lakini nenda kwenye hoja yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Akaniuliza Mhe. Jidawi wakati huo ni Katibu Mkuu yule pale simsingizii na Ramadhani hii tuko katika kamati na Juma Duni ananiambia hoja yako, niambie siku ngapi unachukua toka Bohari Kuu Maruhubi mpaka Mnazi mmoja anambia nimwambie nikamwambia ata hadi nusu saa. Kuna dawa zili-*expire* kule wananchi wanazitaka Mnazi Mmoja si uzembe huo, hapatoshi hapa hili banda nimehangaika kwa muda mrefu mie leo kuja kunambia nimpe muda aaa wajumbe ninakuombeni sana nisaidieni sana sana kama tuko wakweli.

Mhe. Mwenyekit: Mheshimiwa hoja yako iko *valid* sana lakini sasa mimi najaribu…….

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa inaingia katika sera na utafiti waulize hao…..

Mhe. Mwenyekiti: Sawa lakini unachotaka sasa tufanye nini hizi pesa zilizopo sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ninachokiogopa huko Mhe. Mwenyekiti, hiyo hoja nisije nikaipata huko mbele na waswahili wanasema unapokuta maji yakoge kwanza hujui kama mbele kama utayakuta hoja inaingia hapa Mhe. Mwenyekiti, waulize wasaidizi wako sera na utafiti.

Mwenyekiti: Hatujakataa kama sera haingii Mheshimiwa nakubaliana na wewe ni sahihi unachokitaka kitu gani?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kama haiingii hapa tuje kwenye huduma za Rasilimali wa tu ndio nikasema nina hoja mbili hapo hapo sasa tutachagua ipi, hii huitaki.

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo moja hatujamaliza umeshachupia ya pili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa ipo katika hiyo huduma za rasilimali watu na hii ni huduma.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hiyo pesa unataka ifanyweje unataka kitu gani kwenye hii fedha?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Banda la Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hiyo ndio hoja yenyewe mheshimiwa unataka banda au vipi lijengwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hakuna kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti: Haya sasa nimeshakuelewa na Waziri ameshakuelewa mwache akujibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mwenyekiti, kuhusu banda pale nimejibu nimesema tunahitaji ndio unaona matatizo hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Hawakuwepo mimi nilikuwepo.

Mhe. Waziri wa Afya: Unaona matatizo hayo nimejibu kwamba tunahitaji miezi sita sasa yeye anasema pesa hizi mimi nimeshajibu kwamba banda sisi tutatekeleza, sasa wewe umemuuliza unahitaji nini ndani ya miezi sita ana wasiwasi wa nini.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa haya banda lako miezi sita tusikilizane mpeni Mhe. Jaku azungumze haya zungumza sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa unaona uwezo wa Mungu huu ulivyo kwa kuwa nazungumza ukweli ulivyo Mwenyezi Mungu anaonesha mfano wake, Mheshimiwa miezi sita ndio nikakwambia hawa watu utendaji wao hauridhishi, Wizara ya Afya ni Wazembe uzembe nimeshatoa mfano hili banda nimehangaika miaka saba ananambia miezi sita, anirejeshee ramani mimi ndio niliyehangaika na ataona hili jengo kama halitojengwa pengine isifike miezi sita hatua ataiona wajumbe nisaidieni nakuombeni jamani, nisaidieni kama tutapiga kura hili banda lirejeshwe wanaumia wale watu baada ya kuwa wazima wanapata magonjwa pale hospitali wanalala chini. Nakuomba Mhe. Spika, sijawahi kukuomba maisha yangu hili nakuomba unisaidie.

Mhe. Mwenyekiti: Nishakuelewa Mheshimiwa nishakuelewa..

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ramani mimi ndio niliyehangaika anirudishie tu nitajua njia za kwenda kujenga mimi nasaidia Zanzibar yangu mimi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina taarifa ya ramani kama kahangaika yeye mimi nilipoingia Wizarani katika makabidhiano nimeikuta ile ramani iko pale, sina taarifa hiyo wala hakuna pahala maandishi yameandikwa kwamba ile ramani ya Mhe. Jaku au alishughulikia Mhe. Jaku lakini ile ramani imefuata *process* zote za kwenda kwenye Mamlaka husika za Mji Mkongwe na kupata vibali vyote husika, nilichosema mimi kwamba kulikuwa hakuna *allocation* sasa hivi madam tupo na tunajua sisi njia zetu za kufanya atuachie miezi sita, baada ya miezi sita si tunarudi tena humu Barazani atatuuliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nakuomba tena na tena miaka saba na miezi sita yeye alikuwa hajui Mheshimiwa, naomba kidogo nisikilize najenga hoja hili wanaoumia ni wakulima na wavuvi, kwa nini anaumia kunipa mimi nikenda nikalijenga, kwani itakuwa aibu nimeshatoa laki 250,000 ndani ya Baraza humu kwa wananchi wa Jozani, Kitogani, Muungoni wanakosa maji wamechukua miezi miwili kwa laki mbili na nusu.

Sasa Wizara ina mambo mengi humu ndani limetokea kama kuna watu wanakumbuka nilitoa laki mbili nikampa Waziri hapa.

Mhe. Mwenyekit: Yaani Mheshimiwa unataka hili ulijenge wewe?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nitajua njia za kufanya watalikuta banda tu hulo kama sikujenga mimi nitaomba nitapitisha bakuli hata waheshimiwa watanichangia humu ndani, kwa hivyo asione aibu nimeshawahi kufanya Baraza lililopita mie laki 250,000 mimi nimempa Waziri hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tumeshakusikia Mheshimiwa Mhe. Waziri jibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali hauendi hivyo hata siku moja itolewe *Document* au litolewe Banda apewe Mhe. Jaku kesho atuwekee maduka pale ya kuuza kadi za simu na kadhalika haiwezekani, uamuzi wa Serikali ni huo baada ya miezi sita sisi tutawasilisha ripoti tumefikia wapi na naamini itakuwa tumeshamaliza. Lakini haiwezi Serikali ikatoa eneo tu au banda ikampa Mhe. Jaku mkononi haiwezekani Serikali haiwezi kwenda hivyo Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ni mara tatu umeshaongea na nafikiri tumeshafikia pahali wao wanaahidi watalijenga ndani ya miezi sita, tunajua kwamba miaka saba iliyopita hakuna kilichofanyika, lakini Mhe. Waziri aliyekuwepo ni mpya ameshaji-*commit* kwamba atafanya ka miezi sita.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa Miezi sita hebu niambie ndio ubinadamu watu wanateseka anayekwenda pale ni mkulima na mnyonge pana sakafu, tunahitaji kurudi kwa wananchi sisi..

Mhe. Mwenyekiti: Naomba ukae Mheshimiwa….

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti hili Baraza tunavyokwenda kiti kinayumba watu wanaumia Mheshimiwa watu wanatusikia huko.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku naomba ukae tunaendelea.

Kifungu PH 0103 Uendeshaji na Uratbu wa Wizara ya Afya	15,889,552,000
JUMLA KUU	**72,336,229,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi

bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU A02 HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Kifugu PA0201 Huduma za Uchanguzi na Matibabu

Mhe. Mwenyekiti: Nafasi ya mwanzo nitampa Mhe. Hassan Khamis Hafidh, nafasi ya pili Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) Mhe. Mwantatu, Mhe. Miraji watu wanne haya tuanze.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nasimama kwa SH 020101 *Diagnosis Service* Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru leo kwa kuonyesha ukakamavu wa kiti chako kwa kunikubalia hoja yangu halali ya kuunda kamati teule.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa huko usiende nenda kwenye hoja yako tu moja kwa moja.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mheshimiwa nakushukuru sana kwa sababu tunakuogopa siku hizi Mhe. Spika, unakipenda kimurimuri. Mhe. Spika, hoja yangu kuna mapesa mengi hapa tunapitisha Mhe. Spika, leo ambayo yanahusu *Diagnosis Service* lakini Mhe. Spika, tumezoea tunapokwenda Mnazi Mmoja wananchi weu wanapelekwa Al-rahma wakapime, wanapelekwa Kilimani, wanapelekwa Global na ushahidi wa hayo Mhe. Spika, leo asubuhi wakati tupo Mnazi Mmoja saa 12.16 hata zile dawa za kusafishia film za *X-ray* Mnazi Mmoja hakuna na mapesa haya tunapitisha.

Sasa nataka kauli ya Mhe. Waziri kwamba baada ya kupitisha pesa hizi leo kuanzia tarehe 1 Julai, hakuna mwananchi hata mmoja ataambiwa aende Al-rahma, hakuna mwananchi atakayeambiwa aende Global, au hakuna mananchi ataambiwa aende Kilimani, nataka leo niambiwe hapa ita-c*ommitment* ya Mhe. Waziri ambayo itakuwa ni ya Serikali wananchi wakwezi na wakulima kwenda Kilimani itakuwa basi, kwenda Global itakuwa basi, kwanda Al-rahma itakuwa basi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri *Commitment* kama ile hoja ya Mhe. Hamza ile imefanana sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilieleza pale nlipokuwa natoa maelezo na naomba nimkubalie Mhe. Hassan kwamba hizi huduma hata hivi sasa hivi wachilia mbali Julai, kwa sera yetu tuliyokuwa nayo na agizo la

Serikali huduma hizi zinatakiwa, mwanzo tulikuwa tuna-charge sisi *cityscan* na mambo mengine. *Cityscan* tulikuwa tuna-*charge* 150,000 Mhe. Rais alitoa tamko rasmi kwamba hiyo *charge* hiyo iondoshe. Kwa hivyo hivi sasa hivi kwa huduma za zinazonunuliwaa na huduma zote zinazotakiwa zitolewe Mnazi Mmoja zinatolewa, *only* zile *Extra* mfano nitatoa kama *Thyroid Function Test* wakati mwengine ile inabidi uende nje kwa sababu pale haipo huduma ile. Lakini huduma zote za *Basic Service* za *Laboratory* pamoja na uchunguzi, *MRI X-ray, MRI* yetu inafanya kazi sasa hivi zote zile hivi sasa hivi kabla ya hiyo mosi julai zinatolewa Mnazi Mmoja.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, unajua bluu iwe bluu na kijani iwe kijani Mhe. Mwenyekiti, si siri sote hapa tunafanya kazi moja ya kuitakia kheri sana Serikali ya Mapinduzi, nilisema na yeye alikiri kwamba katika Wizara inasemwa sana na wananchi ni Wizara ya Afya hasa hospitali ya Mnazi Mmoja. Sasa mimi nilichomuuliza hichi pesa ndio tunampitishia na Julai tarehe 1 zitaanza kutumika hizi pesa, sasa nataka aniambie tu pale pale nitagonga kwamba kuanzia Tarehe 1 Julai hakuna mwananchi atakayekwenda Mnazi Mmoja tena atapewa damu zake na vitu vyake aende Global, au Al-rahma au aende wapi hicho ndio ninachoktaka mie asizunguruke mbuyu. Ata Mhe. Rais anasema atakayejibu majibu yaliyokuwa yanaweza kutekelezeka yaliyo sahihi mapesa ndio haya hapa tunapitisha leo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa *commitment* ya Wizara kwamba pesa mkishakupata je, kuanzia tarehe 1 Julai, wananchi hamna tena ruhusa ya kwenda Global na kwengine kupata hivyo vipimo, ndio anayochataka yeye anataka *commitment* unajua ni ngumu sana kuipata, kwa sababu hizo kazi hazifanyi yeye kuna watendaji wengine nio wanaotenda lakini usimamizi muhimu sana hapa. Mhe. Waziri tafadhali.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru sana *We are committed and will Continue to be committed*, hivi sasa hivi tupo *committed* ndio maana watendaji wetu wako pale wote Serikali nzima iko hapa mbele yote *we are committed* kutoa *services* hizi na hilo ni tamko la Rais pia na Mhe. Rais wetu yuko *committed* ndio maana ametoka kwenye bilioni 4.3 mwaka jana amekuja kwenye bilioni 8 Mheshimiwa tutaendelea kutoa hizo *Services* na ukitaka hapa naweza nikasoma, kuna bilioni moja imetengwa kwa chanjo 4.5, 8 bilioni dawa muhimu na vifaa vya tiba pamoja na vitandalishi, kuna milioni 700 ambayo imeongezewa na milioni 300 nyengine kutimia bilioni moja dawa za saratani. kuna 1 bilioni nyengine kitendanishi vya maabara na huduma za uchunguzi wa mionzi ikiwemo *MRI, CityScan* na *X-ray* vyote viko kwa hivyo Mheshmiwa *we are committed*, sitaki kusema kwamba kuanzia 1 Julai, ndio

tutakuwa *committed* sasa hivi hatuko *committed* sasa hivi hatuko *committed*. Kwa hivyo tuwaache wananchi wetu tusiwahudumie ama wafe kuanzia sasa hivi mpaka 1 Julai, tuko *committed* sasa hivi na 1 Julai, tutaendelea kuwa *committed*.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, sitaki kukaa sana kwenye hili lakini sera ipo Mhe. Rais kashasema na hivi vitu havifanyiki Mnazi Mmoja, sasa sijui tunataka Rais aseme nini tena, sasa ina maana Rais kashasema havitekelezeki sasa hatutaki kusema mtu achukue *Political Responsibility* hatutaki kusema hivyo lakini tutatizama. Lakini tunataka kusema hivi ikibidi tutasema Mheshimiwa kwa sababu inatuuma wananchi wetu hawapati *Good Service* pale na Serikali inajitahidi na Rais keshasema. Leo tuna *reserve awards will not going to say the minister has Political Responsibility* leo tuna *Reserve but on near future* tutasema hilo, kwa sababu yeye ndie msimamizi mkuu nataka kumpa mfano. Walipita Mawaziri pale mfano Waziri yule jamaa yangu yule wa Ndijani alikuwa anasimamia Dkt. Sira alipita pale sasa tunamtaka akasimamie na pesa tunampitishia leo hatumwambii kuchukua *Political Responsibility* lakini on the near future tutamwambia kwa sababu kazi ya Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwa sababu tuna wasiwasi pesa hivi kasema mwenyewe hapa wasijekuwa wanazitumia kusafiria yeye na Mwanasheria kama alivyosema mwenyewe hapa, sasa tunataka zikafanye kazi yake Mhe. Spika.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. naona hili limekwisha tunakwenda kwa mtu mwengine Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa).

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana mimi nilikuwa na hoja moja (a) na (b) lakini ya kwanza niliona fedha hizi ambazo zimetajwa kifungu HH02100201 kutoa huduma kwa wagonjwa ambazo zimepangiwa milioni mia tatu na tano, nilikuwa nataka tuzizidishe na tuzitowe sasa kwenye kifungu PH 0202 ambazo zimepangiwa milioni kumi. Kwa nini niseme tuweze kuzizidisha hapa nina nia safi sana Hospitali ya Mnazi Mmoja imekosa *Urologist* nataka munisikilize vizuri *Urologist* mmoja tu aliyekuweko ni daktari wa kichina na nilipeleka mgonjwa ambaye alimtibu lakini alienda Malawi zaidi ya siku tatu au tano mgonjwa akakosa *Management* ya kutosha mpaka bleda likwa nje na hatimae mgonjwa alikufa.

Sasa nataka kuziongeza hapa aidha tuweze kuongeza Daktari yule aliyekuwa *Traning* tuweze tukampe mafunzo awe *Urologist* kamili ili tuweze kupata Madaktari bingwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hoja umeiona na umeisikia.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mheshimiwa tunamshukuru Mhe. Mohammed Said Mohammed ni kweli tuna *Urologist* moja amefanya *Reserch* yake vizuri naomba nimpongeze kwa hilo, mimi ningemuomba Mheshimiwa atukubalie kwa sababu kuna nafasi za masomo ambazo tumepokea kutoka Hokland University, kwa hivyo huyo tutajitahidi tumuingize huko kwa ajili ya kusoma tusiathiri bajeti hii. Kwa sababu tuna mashirikiano na Serikali ya Norway ambao wanatu-support sana kwenye suala la kutoa taaluma na ku-*up grade* madaktari wetu. Hivi sasa wapo Madaktari kadhaa ambao wako Norway na wengine wako *Egypt Alexandria Institute of Medical Siciences* ambao wanasoma huko. Kwa hivyo huyu tutamu-*up grade* kupitia ufadhili ambao tunapata moja kwa moja huko. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nimemfahamu sana Mhe. Waziri, lakini kitu ambacho kinauma unamtoa mgonjwa nyumbani anakuwa mzima anapata *treatment* lakini anakosa *management* Mheshimiwa inasikitisha sana, tuendelee lakini nina hoja (b) si unaniruhusu niendelee.

Mheshimiwa hii nazungumza habari ya sera kulikuwa na wafanyakazi kwenye hospitali ya Mental ambao wanatoa *Methadone*, wafanyakazi wale walikuwa wanalipwa, baadae wakawa wanalipwa dola 200 baadae zikakatwa zaidi ya miaka miwili hawalipwi tena lakini sasa wanaambiwa watalipwa elfu kumi ya *holiday* kati ya Jumamosi na Jumapili wanazofanyakazi pale. Nilikuwa nataka kujua hizi pesa nyengine ambazo walilipwa halafu zikakatwa zimekwenda wapi na lini watapewa pesa zao.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, pale pana miradi midogo midogo mbali mbali katika hii *Clinic* ya *mathodone*, sasa sina uhakika sitaki niseme kauli ambayo sio sahihi sina uhakika hizo mia mbili za mwanzo zilikuwa zinatoka wapi kwa sababu Kitengo kile tuna-*share* wako Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pale, wako kile Kitengo kile cha Madawa ya Kulevya na sisi pamoja. Wengine wako *pre* wengine *interim* wengine *post* kwa hivyo sina uhakika nitakwenda nitamtafutia mia 200 zile zilikuwa zinatokea wapi ili niweze kumletea kwa maandishi Mheshimiwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti nikushukuru na nimshukuru sana kwa majibu mazuri Mhe. Waziri lakini nataka anipe *commintment* kuwa sio yeye atokwenda tuende pamoja ili tuone haki ya wananchi wanyonge inapatikana.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nimekubali Mhe. Dimwa ni rafiki yangu sahibu wangu sana, kwa hivyo nimekubali nitakwenda naye pamoja na pale jimboni kwake pia.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: tuendelee.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia niligusia Kitengo cha *Physiotherapy* namshukuru Mhe. Waziri alipokuja kufanya majumuisho alijaribu kuelezea hoja yangu ilikuwa ni kwanini hakikujitokeza kitengo kile katika bajeti hii lakini Mhe. Waziri amenijibu kwamba vitengo anavyo vingi na hakuweza kuainisha kimoja kimoja lakini Mhe. Mwenyekiti hoja yangu hasa ilikuwa ni kwamba kitengo kile zaidi ya bajeti huu mwaka wa nne hawaingiziwi fedha na katika bajeti hapa tunapitisha lakini wakati wa utekelezaji kitengo kile hakipewi hata shilingi moja na nikajaribu kuelezea changamoto ambazo tunazipata sisi watu wenye ulemavu pale ndio kimbilio letu.

Sasa kutokana na bajeti hii Mhe. Waziri amesema kwamba watatenga watafanya watanunua lakini nataka anithibitishie kwamba ni kiasi gani hasa walichokitengea kitengo kile ili na mimi nijiridhishe kuona huduma zetu zinakwenda vizuri.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua hii ni bajeti ya Mnazi Mmoja kwa miaka hiyo minne iliyopita Kitengo kile wafanyakazi wake wanaendelea kulipa mshahara na Serikali wamo na wamo katika hizi 90.8 *billion*. Hakuna *individual allocation* ya kwamba kitengo hichi hichi hichi hiyo ni *internal information* ya wenyewe Mnazi Mmoja *management* naomba nimuhakikishie Kitengo hichi mwaka huu kitakuwemo katika kasma hii kuu tunayoipitisha ya Mnazi Mmoja la kwanza na la pili kuna wale *Club foot association* wa Uingereza ambayo wanachangia takriban milioni 200 hadi 300 tutaendelea kuwasiliana nao ili mchango wao ufike kwa kutoa ile programu ya kwenda *outreach* watoto kufanyia operesheni kwenda mashamba kuwatoa wale watoto ambao hawajatolewa kuja kufanya operesheni. Kwa sababu watu wengine wanawaficha watoto wenye kuja kufanya operesheni wanawaita miguu vifundo, kwa hivyo hilo naomba nimuhakikishie Mheshimiwa kwamba bajeti itakuwa *alocated* katika hii bajeti kuu ya Mnazi Mmoja na Kitengo hichi kama vitengo vyengine kisukari, presha vyote vinavyopata basi na hichi nacho kitakuwemo.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini tu Mhe. Mwenyekiti, *Club foot association* hii ipo *special* kwa kwa wale wa wototo wanye miguu rungu, lakini tukiangalia kitengo kile kinaangalia mahitaji mbali mbali nayo maradhi pamoja na ulemavu wa aina fotauti nafikiria mwaka mmoja kama walivyosema wenzangu si mbali naomba tuendelee tunaona utekelezaji ukoje.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi na nasimama kwenye kifungu HH02010201 Kutoa Huduma kwa wagonjwa.

Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu ya ufasaha na yanaonekana utekelezaji kuwa mzuri na hasa na pale atakaposhuka chini kama azma yeye na wenziwe watakavyokwenda kwa mujibu wa kauli yake. Naomba nende moja kwa moja kunako kifungu hichi.

Nimesema moja ya kadhia ambayo wanaipata wagonjwa wetu ni pale ambapo wanapewa ile huduma ya kuchunguzwa na kupelekwa katika wodi sasa wakitoka katika eneo lile la hospitali mpya, wakiandikiwa kulazwa katika hospitali kongwe katika jengo jipya kwenda katika jengo kongwe huingizwa katika *trolley* wakabururwa au wabururaji ni wale wanaokwenda na wagonjwa kitu ambacho, kuna utaratibu wake kuna watu tunawajiri na tunawapa fedha kuwa hawafanyi kazi ilie. Na kuna utaalamu pia wa kuwachukua hao wagonjwa wenyewe ili wasije wakaumia mara mbili zaidi ya kile walichokwenda nacho, sasa tulikuwa tunataka kabla hajashuka huko chini na timu yake kunako miundo mbinu kunako wale wafanyakazi ambao wanastahiki kufanya ile kazi nataka kauli ya Mhe. Waziri leo hatutawaona tena watu wetu kubebeshwa wale wagonjwa kinyume na misingi ya udaktari tunavyoelekezwa, Mheshimiwa naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. naomba nimshukuru Mhe. Miraji Khamis Mussa kuja na suala hilo ee ni kweli jamaa wa wagonjwa hao wanaosindikizwa hata miye mwenyewe nishawahi kusaidia kusukuma *trolley*, anayetakiwa kuongoza hasa ni mfanyakazi ambaye amepata mafunzo namna ya kum-*handle* mgonjwa, kwa sababu kuna *handling* kuna *course* hasa wamesomeshwa *handling of patient* na *care* yake, lakini lazima ndugu au jamaa wanakuwepo pale huwa wanasaidia kwa sababu ya uhaba wakati mwengine wa wafanyakazi. Sasa mimi ninachotaka kumuhakikishia kwamba tutahakikisha kama mfanyakazi wetu mmoja anakuwepo kama watatokezea mwengine kusaidia basi lakini lazima aweko ndani ya *care* na mfanyakazi wetu. Jana nilikwenda tena mimi kwa sababu aliuliza hili nilikwenda kutazama tena na nilipiga video na nililirusha katika mtandao wa wawakilishi kuona kwamba vipi inavyofanyika. Ni kweli

walikuwepo wawili jana wafanyakazi lakini ndugu jamaa watatu walikuwa pamoja. Wanamtoa huku wanampeleka kwenye jipya wanamtoa kwenye jengo lile kubwa wanamleta pale kwenye *emergency* na *drip* yake mmoja amekamata ile *drip* yake. Kwa hivyo Mheshimiwa nitahakikisha kwamba mfanyakazi wetu mmoja hatoki bila ya mfanyakazi wetu mmoja kuwepo ahsante.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti nimshukuru tena Mhe. Waziri na lile la miundo mbinu kaliacha kwa sababu pale pahala pabovu sana, lakini nataka nende tena kauli nzuri inaashiria utekelezaji mwema na Ishaallah Mwenyezi Mungu awawezeshe wawe na nia hiyo. Isipokuwa nataka kauli ya moja kwa moja sasa itakapotokea mgonjwa yule kenda kupata matibabu hakufatana na yule *nurse* ambae anawajibika au yule mtu ambaye anawajibika kisheria kwa mujibu wa taratibu wa taratibu za kidaktari nini kauli ya Waziri katika jambo hili itakapotokea maana tutakuja kuwapiga picha tumpelekee na daktari ambaye karuhusu kupita kwa mgonjwa tutamwambia nini kauli yake itakapotokea anachukuliwa mgonjwa kakabidhiwa wale wenyewe hao anaosema wanasaidia mpaka kwenye wodi anafika nini kauli ya Waziri litakapotokea jambo hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Kitanzi hicho haya.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kitanzi kikubwa sana Mheshimiwa hapa sitaki kutowa kauli yoyote kwa sababu hii ni kauli nzito sana ila nitatoa mfano halafu nitamuachia Mhe. Miraji aone mfano huo, kwa sababu mfano huo ushawahi kunitokezea. Hivi karibuni palitokezea ajali, ajali ya gari maeneo ya shamba na pale wanapoletwa wagonjwa na mimi nikawepo pale niliona jinsi gani wale manesi na madaktari waliovyohangaika wakawachukua wale wagonjwa wakenda nao *emergency* moja kwa moja. Sasa wale majeruhi wengine waliokuwa hawajaumia sana waliokuwa hawajapoteza fahamu ilibidi wasaidiwe na sisi tuliokuwepo pale na mimi mwenyewe, mmojawapo nikajitolea. Mimi Mheshimiwa sina *qualification* ya udaktari kwa hivyo na mimi nitaingia katika *category* hiyo hiyo kwamba siruhusiki kum-*handle* mgonjwa yule.

Sasa naomba Mhe. Miraji asitake tutowe kauli hapa kwa sababu ni suala zito linaweza kutokezea jambo lolote linaweza kutokezea ajali nchi hii tumeshapata ajali kadhaa za meli, maafa mengine inaweza kutokezea maradhi mengine ni kauli nzito kuitolewa washawahi kuja madaktari wewe Mhe. Mwenyekiti na Mhe. Spika wa Baraza hili ukiwepo pale unamuona mgonjwa huyu utashindwa kumsaidia anakata roho aa haiwezekani si ubinaadamu. Kwa hivyo *base on circumstrance* tusitowe *commintment* kwa sababu *circumstrance* zinabadilika

na inaweza kutokea jambo lolote tusije tukatoa *commintment* halafu tukashindwa kutimiza zile *commintment*.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri na kwa sababualiahiri yeye na timu yake watashuka chini basi najua watatusaidia wale ma-*nurse* wetu kufanya kazi nao nakushukuru tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tunaendelea.

PH0201	Huduma ya Uchunguzi na Matibabu	295,754,000
PH0202	Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja	

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi katika mchango wangu wa maandishi nilimuomba Mhe. Waziri kuhusu suala zima la maji katika hospitali ya Mnazi Mmoja huu ni mwaka wa saba sisi tuko katika Baraza hili na tunaeleza kuhusu shida ya wagonjwa wanayoipata kutokana na tatizo la maji.

Sasa mimi nikamuomba Mheshimiwa naye akanijibu akasema wako katika mipango wako katika kulifuatilia wako sio vibaya, lakini nia yangu ya kumuomba kwamba mimi nilitaka niwaombe kwa dhati waheshimiwa wajumbe wenzangu wa Baraza hili la Wawakilishi kwa moyo safi kabisa. Maana yake nimeongopa sana Mheshimiwa nasema katika majibu yake hapa nilikuwa nayasikia mengi yanasubiri wafadhili nikawa naogopa na hili tusijekuwa kuwa tunasubiri wafadhili. Ni suala zito kabisa, la kuwa lazima tuwe na maji pia ninaendelea kuharibu mazingira katika hospitali yetu maana vigeleni vya maji kila wodi utavikuta.

Sasa mimi nilikuwa nataka nimuombe Mheshimiwa kwamba suala hili, mimi nilitaka niombe wajumbe wenzangu kwa kuona uzito wa hili tatizo niwashawishi wajumbe wenzangu tuweze basi kusamehe posho yetu ya siku moja ili tukalishughulikie suala hili na hii ni kumuunga mkono Mhe. Rais wetu kwa jinsi ya juhudi kubwa kabisa anayoichukua katika kuona anataka kuhakikisha afya ya wananchi wa Zanzibar inapatikana wakati wowote. Sasa nilikuwa nataka niwashawishi wenzangu ili tuwachie posho yetu ya siku moja ili tukajitike katika kushughulikia hili suala la maji ambalo suala hili tukilishughulikia tutakuwa tumemsaidia Rais wetu katika zile juhudi zake anazozifanya lakini, pia litaweza kutujengea sisi katika hatma njema ya kuona tumetengeneza sadaka tu jaria yetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo mimi nilitaka kuwashawishi wenzangu juu ya hili ili tukasaidie huduma hii na nataka niumbe Mhe. Waziri ile alitwambia yeye kwamba tayari ana watu wanafatilia wana nini aweze kutushirikisha sisi wajumbe, tuone hiyo *concern* ya huko ikoje ili tuweze kulitatua suala hili kwa pamoja. Mheshimiwa nilikuwa naomba hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa, Mhe. Waziri kuna pendekezo hapa kwamba Waheshimiwa Wajumbe wachange posho lao la siku moja liende likasaidie ile huduma.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. kabla hawajawajibu,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. sitawahoji kwenye hili wala msiwe na wasiwasi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. hawajahojiwa bado, na sisi Mheshimiwa mimi naingia hofu kukubali kwa sababu tunaweza tukapewa posho la siku moja mfano ikawa shilingi milioni 10,000,000 mfano tu natoa na ile kazi ni ya milioni 200,000,000, 300,000,000 nitakuja kukapaswa na roho humu ndani kwa milioni 10,000,000 zile na wakati ule mradi ni milioni 200,000,000, 300,000,000 hapana. Naomba aiachie kazi hiyo Serikali ili Serikali ifanye *commintment* yake kwa wananchi kama ilivyochukua ahadi ya kufanya *commintment* yake kwa wananchi. Wapo wale wataalamu tutawashirikisha tutawaalika watakuja kututembelea kwa sababu kauli nyengine hizi zishaanza kutolewa hazina fiashiria vizuri.

Kwa hivyo naomba nimshukuru Mhe. Panya kwa *offer* yake hiyo niwashukuru wale wajumbe waliokubali kwa offer yao hiyo lakini naomba nitakae kuipokea kwa sababu itakuja kunitundika kama kamba baadae. Ahsante Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti mimi namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini sisi tulikuwa na lengo safi na ndio maana nikawa nataka tuende huko ili tukaone huo uzito wa tatizo na hawa mafundi na nini tutakavyoambiwa, ili sisi tuweze kuona tunatoa mchango wetu kwa kusaidia nguvu za Mhe. Rais. Kwa sababu Rais wetu kwa kweli amejitahidi katika mambo mengi kabisa juu ya afya. Sasa mimi imani yangu ikawa ni hiyo lakini kama Mhe. Waziri analeta hoja ya kuwa anaogopa basi mimi naomba tu atushirikishe sisi katika hao wataalamu wake wa maji ili na sisi tukajue hicho kilichoko huko, halafu sisi tutaweza kukaa kama wawakilishi nitakaa na wawakilishi wenzangu tutajua nini tufanye. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. nafikiri Wizara na Serikali walishalipokea hilo ni jambo zuri sana ulilolipendeka Mhe. lakini *timing* yake na sikukuu nafikiri ndio maana ikawa *reaction* kidogo kutoka kwa waheshimiwa iko tofauti tunaendelea. Mhe. Jaku hukuwepo nimewataja watu watakaochangia hapana Mheshimiwa naomba ukae *please* naokumba Mhe. Jaku naomba ukae *please* nakuomba ukae Mhe. Jaku na sisi tunataka kukimbilia huko Mheshimiwa naomba ukae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sijakasirika Mheshimiwa mtu mmoja hoja hii, ujue sijakasikirika mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. nakuomba nishakuomba basi imetosha. Naomba tuendelee.

PH0202	Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja	10,084,825
	Jumla kuu	**10,380,579**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara yetu ya Afya bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa.

Mhe. Spika: Naomba niwahoji hoja imeshatolewa na imeungwa mkono wale wote wanaokubaliana na hoja ya Wizara ya Afya wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda.*(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikikiwa)

M**he. Spika:** Waheshimiwa naomba kutoa shukrani zangu dhati sana kwenu nyinyi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwanza kwa michango ambayo mmeitoa na sote ni mashahidi kwamba mambo ya msingi na mazito sana ambavyo mlikuwa mmeyachangia, tumepata majibu lakini sasa tutakuwa tunasubiri zaidi utekelezaji upande wa Serikali. Lakini pia niishukuru Serikali kwa *commintment* ambazo wamezichukua baada ya kusikiliza

michango ya waheshimiwa Wajumbe na pia nishukuwe nafasi hii sasa kumpongeza Mhe. Waziri pia Mhe. Naibu Waziri pamoja na Watendaji wenu wote kwa kazi kubwa hii kazi ni ngumu sote tumeshaona hayo mazingira yeyewe nakupongezeni sana.

Baada ya hayo nimwite Katibu kwa shughuli inazoendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa Mwaka 2017/2018

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Bismilahi Rahmani Rahim. Mhe. Spika, kwanza ruhusa yako, naomba kuomba radhi Baraza lako kwa kuwa sauti yangu leo siyo nzuri sana kwa sababu kifua kinaniuma kwa hivyo naomba niombe radhi sana kwa hilo.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati, ili liweze kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W.) kwa kutujaalia afya njema na uzima na kwa kuniwezesha kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Naomba Mwenyezi Mungu anipe uwezo wa kuiwasilisha vyema hotuba hii.

Mhe. Spika, kwa furaha kubwa naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein kwa hekima na busara kubwa anazotumia katika kuiongoza nchi yetu. Hakika miongozo yake anayoitoa imeonesha nia, dhamira na malengo katika kukuza uchumi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ya kutumikia wananchi pamoja na mashirikiano mazuri anayotupa sisi Mawaziri wake.

Mhe. Spika, kwa namna ya kipekee napenda kukupongeza kwa dhati wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako kwa namna ya busara na hekima unayotumia kwa kuliongoza Baraza hili, namuomba Mwenyezi Mungu akupe moyo huo zaidi Inshaallah Mwenyezi Mungu akujaalie.

Mhe. Spika, naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano pamoja na Wajumbe wake kwa namna wanavyotoa mashirikiano ya pamoja katika kufanikisha kazi hii katika Wizara yangu.

Mhe. Spika, kwa namna ya kipekee naomba kuwapa pole Wananchi wote wa Zanzibar waliyokumbwa na maafa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha Unguja na Pemba. Tunawaomba waathirika wote wawe na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu. Aidha tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe mvua zenye neema na baraka kwa nchi yetu na ulimwengu kwa ujumla.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri samahani kidogo naomba nimpishe Mhe. Mwenyekiti.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuungana na Watanzania wenzangu wote katika msiba mkubwa uliotokea Arusha ambao umetuachia huzuni na simanzi kubwa kwa vifo vya watoto wetu wapendwa. Mwenyezi Mungu awape wafiwa moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu na awalaze Marehemu mahala pema Peponi –Amin.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu kuelezea utekelezaji wa wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na muelekeo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kama ifuatavyo:-

Mapato na Matumizi:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 6,100,000,000/= kutokana na vyanzo mbali mbali vya Taasisi zake. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2017 jumla ya Tsh 3,709,148,965 /= zimekusanywa. Kiwango hichi ni sawa na asilimia 61% ya makadirio.

(Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia kiambatanisho “A”).

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara yangu ilipangiwa kutumia jumla ya Tsh 57,456,186,000. Kati ya Fedha hizo Tsh 9,555,400,000 ni kwa kazi za kawaida na Tsh 47,900,786,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2017 Wizara yangu ilikwishapatiwa Tsh 34,416,767,325 kwa kazi za Maendeleo sawa na asilimia 72% na Tsh 4,577,921,367 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 48% ya makadirio, hivyo kufanya jumla ya fedha zote tulizozipata kuwa ni Tsh 38,994,118,688 sawa na asilimia 72% ya makisio yote.

(Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho“B1 na B2) ”

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa shughuli za Wizara, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu ilifanikiwa kutekeleza majukumu yake kupitia programu kuu nne zifuatazo:

Programu PN0101: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi.
Programu PN0102: Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi.
Programu PN0105 : Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati.
Programu PN0106: Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Programu PN0101: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina jukumu la uratibu katika utekelezaji wa kazi za Wizara na inajumuisha programu ndogo tatu ambazo zinatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, na Afisi Kuu Pemba ambapo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/ 2017 utekelezaji wa huduma za program hii ulikuwa kama ifuatavyo:-

Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 utekelezaji wa Programu hii ndogo ulilenga kutekeleza shughuli za kuratibu, kuandaa mipango na miongozo ya kisera ya utekelezaji wa kazi za Wizara, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu na miradi ya Wizara pamoja na kuendeleza tafiti kwa ajili ya kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma katika sekta za Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2017 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:

Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini kwa miradi ya maendeleo

Idara imesimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa kufanya kazi za Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji *(Monitoring and Evaluation)* kwa lengo la kuhakikisha kwamba miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi kama ilivyopangwa. Miradi iliyosimamiwa na Idara hii ni kama ifuatavyo :-

i) Usambazaji Umeme Vijijini.
ii) Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme na Kulijengea Uwezo Shirika la umeme.
iii) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na kuijengea uwezo kifedha Mamlaka (ADF 12)
iv) Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji Awamu ya Pili.
v) Mradi wa uchimbaji visima wa Ras al- Khaimah
vi) Uchimbaji wa Visima na usambazaji maji (CHINA).
vii) Utekelezaji wa Sera ya Nishati.
viii) Utafiti wa Nishati Mbadala.
ix) Mradi wa Mashirikiano ya Sekta za Ardhi baina ya Zanzibar na Finland (ICI).
x) Mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya ukanda wa Pwani (LDCF),

Kusimamia maandalizi na utekelezaji wa Sera za Wizara na kuratibu mapitio ya Sheria mbalimbali za Wizara

Mhe. Mwenyekiti, Rasimu ya Sera ya Ardhi imeandaliwa na ipo katika hatua za mwisho za kuwasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Mapinduzi. Sera ya Mafuta na Gesi Asilia pamoja na Sheria yake zimekamilika na mapitio ya Sera ya Nishati tayari yameanza kufanywa kupitia mradi wa kuisaidia sekta ya Nishati *(Energy Sector Support Project).* Aidha kutokana na kukamilika kwa Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) imeanzishwa rasmi tarehe 18/03/2017 baada ya kutangazwa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji (MD) wa Taasisi hiyo.

Kuimarisha Mazingira ya Uendelezaji wa Tafiti pamoja na kuratibu shughuli za uendelezaji wa tafiti ndani ya sekta za Wizara

Mhe. Mwenyekiti, Idara imeandaa maandiko ya awali matatu *(research concept)* kwa ajili ya kuendeleza tafiti, maandiko hayo yamewasilishwa Tume ya Mipango kwa kutafutiwa ufadhili ili tafiti hizo ziweze kufanywa. Kati ya maandiko hayo, mawili (2) yanahusiana na Masuala ya mazingira na moja (1) linahusiana na usambazaji wa umeme.

Kuimarisha mahusiano na Washirika wa Maendeleo

Idara imeshiriki kikamilifu katika majadiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika katika juhudi za kuendeleza ufadhili kwa ajili ya Mradi wa ‘’ *Enhancing National Capacity for Mainstreaming Climate Resilience in Zanzibar*’’, ambapo hadi hivi sasa mradi huo wa miezi kumi na nane (18) upo tayari kwa hatua za utekelezaji.

Aidha, jumla ya vikao tisa (9) vya mashirikiano baina ya Wizara yetu na Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vimefanywa kati ya hivyo vikao viwili (2) Kwa Wizara ya Maji na saba (7) Wizara ya Nishati na Madini**.**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Katika kutekeleza programu ndogo ya uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti, jumla ya **Tsh** 173,067,000/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2017, fedha zilizoingizwa ni Tsh 129,030,100/= sawa na asilimia 75**%** ya makadirio

Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji

Mhe. Mwenyekiti, program hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji na inajukumu la kusimamia rasilimali watu na uendeshaji wa kazi za kila siku za Wizara, ambapo hadi mwezi wa Machi 2017 Idara iliweza kutekeleza yafuatayo:-

i) Kuandaa na kuratibu mpango wa Rasilimali watu wa Wizara kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwaka 2017 hadi mwaka 2022, ili kujua mahitaji ya wafanyakazi wenye taaluma mbalimbali watakaohitajika katika sekta zote za Wizara.

ii) Kuandaa mafunzo ya ndani kwa watendaji na maafisa utumishi wa Wizara juu ya kuandaa Mpango wa Rasilimali watu kwa muda wa miaka mitano.

iii) Kulipa stahiki mbalimbali za wafanyakazi ikiwemo malipo baada ya saa za kazi na posho za likizo kwa wafanyakazi 17.

iv) Kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Wizara kwa kulipia gharama za ununuzi wa vifaa mbalimbali, malipo ya huduma pamoja na matengenezo ya vipando.

v) Kuratibu shughuli za kustaafisha Wafanyakazi tisa (9) kwa sababu mbalimbali na kuwatayarishia mafao yao ambapo wafanyakazi watano (5) waliostaafu waliratibiwa mafao yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Katika kutekeleza programu ndogo ya Utawala na Maendeleo ya Rasilimali watu jumla ya Tsh 808,112,000/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2017, fedha zilizoingizwa ni Tsh 625,506,359/= sawa na asilimia 77 % ya makadirio.

Programu Ndogo ya Uratibu na Uendeshaji wa Shughuli za Wizara Pemba

Mhe. Mwenyekiti, Program hii ndogo inatekelezwa na Afisi Kuu Pemba na ina jukumu la uratibu na usimamizi wa kazi za Wizara ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo kwa Pemba ambapo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 iliweza kutekeleza yafuatayo:-

i) Kukagua jumla ya Miradi tisa (9) ya Maendeleo, kati ya hiyo, miradi sita (6) ni ya Maji, mmoja (1) wa Umeme, na miwili (2) ya minara ya ukusanyaji wa taarifa za upepo na jua kwa ajili ya nishati mbadala.

ii) Kupima viwanja 271 kwa ajili ya shughuli mbali mbali kama vile makaazi, biashara, taasisi, vitega uchumi, mashamba na huduma za kijamii (miskiti na shule).

iii) Kuziingiza katika mfumo wa database taarifa 1,416 za viwanja vilivyopimwa.

iv) Kutayarisha mikataba minne (4) kwa ajili ya ukodishwaji wa Ardhi, mikataba hiyo ni katika eneo No.77 Makangale, eneo la African Muslim Agency lililopo Mabaoni, shamba la kilimo Makangale na kituo cha mafuta ya petrol Mchangamdogo.

v) Kufanya ukaguzi wa maeneo 32 kwa ajili ya kutayarishiwa hati na mikataba, kati ya hayo 29 ni kwa ajili ya hati na 3 kwa ajili ya Mikataba ya ukodishaji Ardhi *(Lease).*

vi) Kufanya utambuzi wa maeneo *(parcels)* 657 katika shehia ya Limbani Wete, Wara na Mkoroshoni Chakechake.

vii) Kusajili jumla ya maeneo *(parsels)* 282 yaliyofanyiwa utambuzi katika shehia ya Wara Chakechake na Limbani Wete.

viii) Kufanya ziara za ukaguzi wa maeneo ya uwekezaji Micheweni na maeneo ya utalii Makangale, Kiweni Muwambe na Vitongoji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Katika kutekeleza programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ardhi Pemba jumla ya Tsh 1,361,267,000 /= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2017, fedha zilizoingizwa ni Tsh 617,457,750/= sawa na asilimia 45.4% ya makadirio.

Programu Kuu PN0102: Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyofahamika kwamba Kamisheni ya Ardhi ni chombo kikuu kinachosimamia Programu ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi nchini. Hivyo suala la kuimarisha Kamisheni ni hatua muhimu katika kutekeleza majukumu yake. Sekta hii inahitaji kuwa na Sera na Sheria makini ambazo zitatumika kwa mujibu wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Aidha, katika kutekeleza majukumu yake Kamisheni inalenga kuwa na usimamizi mzuri wa pamoja unaozingatia sheria na utawala bora wa ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la programu hii ni kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi *(security of tenure)* kwa maendeleo ya nchi pamoja na kujenga matarajio ya kuwa na matumizi ya ardhi yaliyo bora na yenye ufanisi. Jukumu hili lilipangiwa kutekelezwa kupitia programu ndogo tatu ambazo ni programu ndogo ya utawala wa ardhi, programu ndogo ya upangaji wa miji kwa matumizi ya ardhi na programu ndogo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Taaasisi husika zinazohusiana na utekelezaji wake ni Idara ya Ardhi, Afisi ya Usajili wa Ardhi, Idara ya Upimaji na Ramani na Idara ya Mipango Miji na Vijiji pamoja na Mahakama ya Ardhi.

Programu Ndogo ya Utawala wa Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inatekelezwa na Idara ya Ardhi, Idara ya Upimaji na Ramani na Afisi ya Msajili wa Ardhi ambapo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 programu hii ndogo iliweza kutekeleza Huduma za Ugawaji na Usimamizi wa Ardhi, Uthamini wa Ardhi na Usajili kwa kutekeleza shughuli za msingi zinazohusiana na majukumu hayo.

IDARA YA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu katika utekelezaji wa programu ndogo ya Utawala wa Ardhi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia mwezi wa Machi 2017, kupitia Idara ya Ardhi imetekeleza yafuatayo:

Utayarishaji wa Hati za Umiliki wa Haki ya Matumizi ya Ardhi:

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya hati 450 ziliandaliwa kati ya hizo Hati 316 ni za kudumu na Hati 134 ni za muda. Utayarishwaji huo ni sawa na asilimia 42 ya shabaha iliyowekwa ya utayarishwaji wa Hati 1,350. Aidha, vitambulisho 70 kwa ajili ya kupatiwa wananchi waliopatiwa ardhi za Eka tatu vilitayarishwa na kukabidhiwa wenyewe kati ya vitambulisho 60 vilivyopangwa kutayarishwa. Hiyo ni sawa na asilimia 116 ya shabaha iliyopangwa.

Utayarishaji wa Mikataba ya Ukodishwaji Ardhi:

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya mikataba 73 kwa ajili ya wawekezaji na wageni waliokodishwa ardhi kwa ujenzi wa nyumba za mapumziko ilitayarishwa kati ya 130 iliyopangwa kutayarishwa. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 57 ya mikataba yote katika kipindi hicho. Aidha, katika kuimarisha usalama na umakini wa Mikataba hiyo, hivi sasa Mikataba yote inayotayarishwa hupitiwa na kukaguliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Uingizaji wa Taarifa za Ardhi katika mfumo wa Kompyuta:

Mhe. Mwenyekiti, Idara imeweza kuingiza taarifa za msingi za umiliki wa Haki za Matumizi ya Ardhi kutokana na utayarishwaji wa Hati za Ardhi, Mikataba ya Ukodishwaji Ardhi na Vitambulisho vya Eka Tatu katika mfumo wa kompyuta.

Ukaguzi wa Maeneo yaliyohitaji kutayarishiwa Mikataba ya Uwekezaji na Maeneo ya Kilimo (Eka Tatu):

Mhe. Mwenyekiti, maeneo yote 73 yaliyotayarishiwa mikataba ya ukodishwaji ardhi yalikaguliwa kwa lengo la kuyaelewa, kujua hali yake ya umiliki, uendelezwaji wake na kujua kama hayana madai yanayoweza kuleta migogoro baada ya kutolewa kwa mikataba ya ukodishwaji. Zoezi kama hilo lilifanyika kwa maeneo yaliyotolewa kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo na hasa eka tatu. Pamoja na ukaguzi huo, ukaguzi mwengine wa maeneo 108 ulifanyika katika maeneo ya eka tatu kwa ajili ya kufuatilia na kutatua migogoro ya ardhi iliyokuwepo na pia kufuatilia utekelezaji wa masharti yanayotolewa katika upewaji wa ardhi hizo.

Ufanyaji wa Kazi za Uthamini Ardhi:

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa kazi za uthamini wa ardhi, jumla ya kazi 199 za utiaji thamani wa mali zisizohamishika zilitekelezwa kati ya 300 zilizolengwa. Hii ni sawa na asilimia 63.3% ya shabaha ya mwaka. Utekelezaji wa shughuli hii hutegemea uhalisia wa maombi yanayowasilishwa.

Uendelezaji wa Zoezi la Utambuzi:

Mhe. Mwenyekiti, zoezi hili la kuwabaini na kuwatambua wenye haki ya matumizi ya ardhi lilisita kwa kipindi kirefu tokea kumalizika kwa mradi wa SMOLE II kutokana na kukosa fedha za kugharamia shughuli zake. Hata hivyo, kutokana na fungu maalum la serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Urasimishaji Mali na Biashara (MKURABITA), zoezi hilo limeweza kuanza tena kwa hapa Unguja na kuweza kufanikisha utambuzi wa maeneo (*parcels*) 450 hadi mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2017 katika Shehia ya Matarumbeta.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu wa fedha kazi ya utambuzi inatarajiwa pia kufanyika katika Shehia ya Mpendae na kuweza kufikia utambuzi wa jumla ya maeneo 1,000 hadi kukamilika kwake. Shabaha ya awali ya zoezi hili ilikuwa ni kutambua maeneo 500 tu lakini kupatikana kwa fedha za ziada kumewezesha mafanikio zaidi.

AFISI YA MRAJIS WA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mrajis wa Ardhi ni Taasisi yenye jukumu la kusajili ardhi yote ya Zanzibar kwa kuweka taarifa za wamiliki wa haki ya matumizi ya ardhi. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Afisi imeweza kutekeleza program ndogo ya Utawala wa Ardhi kwa kutoa huduma za utambuzi, kusajili ardhi na utoaji wa kadi za usajili, kama ifuatavyo:

i) Jumla ya Shehia 3 za Mpendae, Matarumbeta na Chukwani zimo katika hatua za utambuzi kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba Shehia ya Limbani imesajiliwa na Shehia 5 za Uweleni, Msingini, Chokocho, Ngomeni na Kipangani zimo katika hatua za mwisho za utambuzi.

ii) Jumla ya kadi 679 za usajili zimetengenezwa na kugaiwa kwa wananchi ambao tayari wamekwisha kusajiliwa kwa maeneo ya Mjini na Ng'ambo.

iii) Jumla ya marejista ya ardhi kwa Shehia 5 za Kikwajuni Bondeni, Miembeni, Muembetanga, Mchangani na Rahaleo tayari yameshatayarishwa.

iv) Kwa kuendelea na zoezi la kutoa elimu ya usajili wa ardhi, Afisi imefanya mkutano mmoja ambao uliwashirikisha masheha pamoja na wasaidizi wao.

v) Kwa kushirikiana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Afisi imefanikisha suala la mirathi kwa maeneo 35 ambapo wamiliki wa maeneo hayo tayari wameshasajiliwa na kutengenezewa kadi zao za usajili wa ardhi. Katika kuleta mafanikio zaidi Afisi imeanzisha utaratibu wa kukutana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ili kurahisisha taratibu za usajili kwa mali za mirathi ambapo vikao viwili (2) vimeshafanyika.

vi) Katika jitihada za kuongeza uwelewa kwa wafanyakazi wa Afisi ya Mrajis wa Ardhi, Afisi imetoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wa Afisi ya Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, katika kutekeleza programu ndogo ya Utawala wa Ardhi jumla ya Tsh 1,065,460,000 ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2017, fedha zilizoingizwa ni Tsh. 592,735,321 sawa na asilimia 56% ya makadirio

IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza programu ndogo ya Utawala wa Ardhi**,** Idara ya Upimaji na Ramani kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

Usimamizi wa Shughuli za Upimaji wa Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/17, Idara ya Upimaji na Ramani imefanikiwa kupima jumla ya viwanja 259 kwa matumizi mbali mbali ikiwa ni pamoja na miradi mikubwa ya Kitaifa na uwekezaji. Aidha, Idara imefanikiwa kufanya vipimo vya mtandao wa alama msingi za upimaji kwa ajili ya matayarisho ya kuelekea utaratibu mpya wa vyanzo vya upimaji msingi (kutoka Arc 1960 kwenda WGS84).

Jaduweli Namba 1: Maeneo yaliyopimwa

Nam	**Matumizi**	**Idadi ya Viwanja**
1	Makaazi	102
2	Huduma mbalimbali	54
3	Vitega Uchumi	28
4	Taasisi	9
5	Mashamba ya Kilimo (Watu binafsi)	66
JUMLA		259

Chanzo: Kamisheni ya Ardhi 2017

Utayarishaji na Utoaji wa Ramani za Ardhi pamoja na Utoaji Taarifa za Kupwa na Kujaa kwa Maji

Idara imefanikiwa kuchapisha ramani *(detail maps)* 273 kwa matumizi mbali mbali pamoja na kupitia taarifa kwa ajili ya kuimarisha ramani msingi 41. Aidha, Idara imeendelea na utaratibu wake wa kukusanya taarifa za vipimo vya mwenendo wa kupwa na kujaa kwa maji ya bahari ambavyo vinaonesha kuwa maji hayo yanakupwa na kujaa kwa mtiririko wake wa kawaida. Aidha, kwa ujumla vipimo hivyo hutumika kwa kazi mbali mbali za utafiti pamoja na kutabiri mwenendo mzima wa bahari.

Ukusanyaji na Uwekaji wa Taarifa za Upimaji

Katika ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za upimaji (*cadastral maps and coordinates)*, Idara imefikia asilimia 25% ya malengo iliyojipangia, pia kupitia mtandao wa taarifa za Ardhi *(Zanzibar Land Information System -ZALIS)* kwa kushirikiana na Idara za sekta ya Ardhi zilizopo, Idara imekuza uelewa kwa watendaji kwa asilimia 5 kati ya asilimia 20 ilizojipangia,

Programu Ndogo ya Upangaji wa Miji kwa Matumizi ya Ardhi

Mhe. Mwnyekiti, Idara ya Mipango Miji na Vijiji ni taasisi yenye dhamana ya usimamizi wa shughuli zote za mipango ya matumizi bora ya ardhi na maendeleo yake nchini. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Idara kupitia program ndogo ya Upangaji kwa Matumizi ya Ardhi, imeweza kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

Kupanga matumizi bora na endelevu ya miji yote midogo 14 ya Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha lengo hili, Idara ilitekeleza kazi mbili (2) zifuatazo:

i) Baada ya kukusanya taarifa muhimu na kukutana na wadau, Idara tayari imekamilisha rasimu ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo ya Mji wa Makunduchi.

ii) Hii ni baada ya kukamilika kwa utayarishaji wa mipango ya maendeleo ya miji ya Chwaka na Nungwi, Idara sasa inaanza kazi za utekelezaji wa maendeleo ya miji hiyo kwa kushirikiana na Wilaya na Halmashauri za Wilaya husika.

Kusimamia maendeleo ya ardhi Mijini, Kikanda na maeneo ya fukwe

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2017 katika kufanikisha lengo hili, Idara ilitekeleza kazi nne (4) zifuatazo:

i) Kwanza katika hatua za kuondosha migogoro ya ardhi, Idara inafanya jitihada zote kuhakikisha kuwa ujenzi wowote unaofanywa katika miji yetu unapewa miongozo.

ii) Katika kukabiliana na ujenzi holela suala la utoaji wa vibali vya ujenzi ni muhimu. Idara kwa kushirikiana na Kamati ya Usimamizi na Udhibiti Ujenzi (DCU).

iii) Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ya Mji wa Zanzibar *(Master Plan)*, unaelekeza kupanga maeneo mapya ya makaazi ya mji. Katika hatua za kutekeleza *"Master Plan"* hiyo, Idara tayari imeshaanza kulipanga eneo la Kisauni. Kazi iliyofanywa ni kukusanya taarifa pamoja na kukutana na wananchi wa eneo husika.

iv) Katika utekelezaji wa mradi wa Mashirikiano ya Sekta za Ardhi baina ya Zanzibar na Finland *(ICI)*, Idara ilipitia mpango wa maendeleo wa eneo la utalii Chwaka mpaka Matemwe.

Kuimarisha Miji ili kukuza uchumi na kuleta Maisha bora

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha lengo hili, Idara ilitekeleza kazi zifuatazo kama zinavyosomeka katika taarifa yangu namba 1 mpaka namba 7.

i) Kwa madhumuni ya kuongeza haiba ya eneo la Mkunazini ambalo ni maarufu kwa biashara na utalii katika Mji Mkongwe. Idara imefanikiwa kulipanga upya eneo hilo ili kuongeza maeneo ya biashara na vivutio baada ya kuondoshwa gereji zote katika mtaa huu na Mji mkongwe kwa ujumla.

ii) Idara imelipanga upya eneo la Saateni ili kuwawezesha wafanyabiashara wa eneo la Michenzani kuhamia eneo hilo, ili kuliwezesha eneo la Michenzani liendelezwe kuwa eneo la biashara.

iii) Kufuatia hatua ya Serikali ya kuondosha kituo cha mabasi katika eneo la Darajani ili litumike kwa shughuli za biashara, Serikali imefanya maamuzi ya kujenga kituo kipya cha mabasi katika eneo la Kijangwani. Hivyo, Idara kwa kushirikiana na Baraza la Manispaa Mjini imeshalipanga eneo la kituo kipya cha usafiri katika eneo la Kijangwani.

iv) Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi unaelekeza kuifanya Tunguu kuwa ni eneo la makaazi, biashara na huduma ikiwemo gereji, magari ya mawe, yadi za magari na nyenginezo. Kwa kufanikisha lengo hilo Idara imelipanga upya eneo hilo ili kutimiza malengo hayo.

v) Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi wa Mji wa Zanzibar umependekeza kurudisha tena haiba ya kitovu cha mji wa Zanzibar katika eneo la Ng'ambo kama ilivyokuwa azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Kwanza. Kwa kuanza utekelezaji wa azma hiyo, Kamisheni kwa kushirikiana na mradi wa Huduma za Miji (ZUSP) zimefanikiwa kusimamia zabuni ya kumpata mshauri elekezi wa kutengeneza mpango wa uendelezaji wa eneo jipya la biashara, usafiri na bustani katika barabara ya Karume. Miongoni mwa makampuni arubaini (40) yaliyoomba, sita (6) yamechaguliwa kuingia katika awamu ya pili ya mchakato wa zabuni.

vi) Idara imetoa taaluma kwa wafanyakazi wake watano katika fani za Mipango Miji. Wafanyakazi hao wamepata mafunzo nchini Japan, Korea ya Kusini, Holland, China na Italia. Kwa upande mwengine Idara imetoa taaluma kwa Mabaraza ya Manispaa na Halmashauri za Wilaya na wananchi ili kuwapa elimu na maelekezo ya kazi zake.

vii) Katika Utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi, Idara imefanya jumla ya vikao Tisa (9) na Wananchi katika Wilaya tatu za Mkoa wa Mjini Magharibi kwa ajili ya kuwaelimisha kuhusu Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi na kutoa maoni yao kabla ya Mpango huo kupelekwa Serikalini kwa kuthibitishwa. Katika vikao hivyo takriban wakaazi Elfu tatu (3,000) walihudhuria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Katika kutekeleza programu ndogo upangaji wa Miji kwa Matumizi ya Ardhi jumla ya Tsh. 1,021,398,000 ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2017, fedha zilizoingizwa ni Tsh. 659,094,559 sawa na asilimia 65% ya makadirio.

Programu ndogo ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi ina jukumu la kupokea, kusikiliza na kuamua kesi za migogoro ya ardhi zinazowasilishwa na wananchi pamoja na taasisi mbali mbali. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Mahakama ya Ardhi kupitia program hii ndogo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi imetekeleza shughuli zifuatazo:

Kutatua migogoro ya ardhi

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Mahakama ya Ardhi imejiwekea malengo ya kuzitolea maamuzi kesi 260. Kwa kipindi hicho Mahakama imepokea kesi mpya 121 ambazo zimefunguliwa Unguja na Pemba, Mahakama imeendelea kuendesha kesi mbali mbali zilizopo Mahakamani ambapo jumla ya kesi 241 zimetolewa maamuzi sawa na asilimia 93 ya lengo la mwaka kwa mchanganuo ufuatao kama inavyoonekana katika taarifa hii:

Unguja: Kesi mpya 86 zimepokelewa na kesi 140 zimetolewa maamuzi.

Pemba: Kesi mpya 35 zimepokelewa na kesi 101 zimetolewa maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2017, Mahakama ya Ardhi ina jumla ya kesi 473 zilizopo Mahakamani, Unguja kesi 357 na Pemba kesi 116.

Ufuatiliaji wa hali ya majengo ya Mahakama ya Ardhi:

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi imeomba kufanyiwa tathmini halisi ya gharama za matengenezo ya jengo lake la Afisi Kuu Majestic na lile la

Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja lililopo Gamba. Tathmini hizo za gharama za matengenezo tayari zimeshafanywa kwa hatua za kuandaa utaratibu wa kuyafanyia matengenezo majengo hayo.

Kutoa elimu kwa jamii

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kufuata Sheria mbali mbali za ardhi kwa kushiriki kwenye maonesho ya maadhimisho ya siku ya Sheria Duniani *(Law day).*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, katika kutekeleza programu ndogo ya utatuzi wa migogoro ya Ardhi jumla ya Tsh 188,214,000 ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2017, fedha zilizoingizwa ni Tsh 149,945,700 sawa na asilimia 80% ya makadirio.

Programu Kuu PN0105: Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii inatekelezwa na Taasisi zifuatazo; Mamlaka ya Maji (ZAWA), Shirika la Umeme (ZECO), Mamlaka ya Kudhibiti na Kusimamia Ubora wa Viwango vya Huduma za Maji na Nishati Nchini (ZURA), Idara ya Nishati na Madini na Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA). Programu hii inajukumu la kusimamia Uzalishaji na Usambazaji Endelevu wa Huduma za Maji na Nishati.

MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Maji ni rasilimali muhimu sana kwa maisha ya viumbe na Jamii zote, maendeleo yote duniani yamechangiwa na upatikanaji wa huduma ya maji. Aidha upatikanaji wa huduma ya maji kwa kila siku hupelekea kukua kwa kipato cha familia na uchumi wa Nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea kutekeleza majukumu yake, kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Sera ya Maji ya mwaka 2004, na Sheria ya Maji ya mwaka 2006, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar awamu ya tatu (MKUZA III), Dira ya Maendeleo ya 2020 na Malengo ya Milenia.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ilitekeleza kazi mbalimbali kupitia miradi na kazi za kawaida kama ifuatavyo:

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Kifedha Mamlaka (ADF 12).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imefanikiwa kulipa fidia katika maeneo yalioathiriwa na Mradi huu uliofadhiliwa na Benki ya maendeleo ambayo hayakuwahi kulipwa hapo awali. Maeneo hayo ni kama inavyosomeka katika taarifa yangu.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji kupitia mradi wa ADF12 imefanikiwa kuchimba Visima 9 katika maeneo ya Bumbwisudi (6), Kinumoshi (2) na Machui (1) na kuvifanyia matengenezo makubwa visima 23 katika maeneo ya Welezo, Mbweni, Mombasa, Kaburi Kikombe, Kianga, Machui, Mwembe Mchomeke na Chumbuni.

Aidha, ujenzi wa vyoo katika Skuli za Msingi Kisiwandui, Kajificheni, Mkunazini na Skuli za Sekondari za Hurumzi, Ben Bella na Haile Selassie umekamilika. Kazi bado inaendelea kwa Skuli za Msingi za Makadara, Mwembe Makumbi, Magogoni, Maungani, Kidongo Chekundu, Muungano, Jang'ombe, na Skuli za Sekondari za Mwembeladu, Nyerere, Lumumba, Chumbuni, Kidongo Chekundu na Kiembe Samaki.

Mhe. Mwenyekiti, Fedha zilizopangwa kwa mwaka katika utekelezaji wa mradi huu ni Tzs 1,060,000,000/-na Fedha zilizopatikana kwa mwaka ni Tzs 1,031,501,788/-sawa na asilimia 97%.

Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu tayari umekamilika na ulikua unafadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada la (*JICA*). Kwa upande wa Mradi huu kazi ya ulazaji wa mabomba katika maeneo ya Gulioni na Makadara imekamilika. Mamlaka ya Maji ilipanga kujenga Chemba za mita na valvu *(Manifold 70 na valve 85).* Hadi kufukia Machi 2017 jumla ya Chemba 26 na Valvu 36 zimejengwa na tayari zinatumika.

Mhe. Mwenyekiti, Fedha zilizopangwa kwa mwaka katika utekelezaji wa mradi huu ni Tzs 150,000,000/-na Fedha zilizopatikana kwa mwaka ni Tzs 125,000,000/-sawa na asilimia 83% ya makadirio.

Mradi wa uchimbaji visima wa Ras al- Khaimah

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu wa uchimbaji visima 50 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 tayari umekamilika na umefadhiliwa na Mtawala wa Ras – al-Khaimah.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imefanikiwa kulipa fidia katika maeneo ya Upenja, Bandamaji, Jendele, Kwarara, Kinyasini, Moga, Dole, Ubago na Shakani Unguja. Aidha Mamlaka imefanikiwa kuviendeleza visima 24 ambavyo tayari vinatoa huduma, Unguja visima 10 na Pemba visima 14. Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho "C"

Mhe. Mwenyekiti, Fedha zilizopangwa kwa mwaka katika utekelezaji wa mradi huu ni Tsh 200,000,000/- na Fedha zilizopatikana kwa mwaka ni Tsh 200,000,000/- sawa na 100%.

Uchimbaji wa Visima na usambazaji maji (CHINA)

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China umefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Matangi 2 katika maeneo ya Chaani na Donge na unaendelea na ujenzi wa Tangi la Kisongoni;

Vile vile Mradi umekamilisha ulazaji wa mabomba katika eneo la Chaani yenye urefu wa kilomita 7.2 (7.2km) na Donge yenye urefu wa kilomita 7 (7km). Aidha ulazaji wa mabomba katika eneo la Kisongoni unaendelea vizuri na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2017 ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 3.8 (3.8km) umeshakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imefanikiwa kulipa fidia katika maeneo ya ujenzi wa matangi na uchimbaji wa misingi kwa ulazaji wa mabomba katika maeneo ya Chaani Masingini, Gamba na Donge na kazi ya uvutaji wa umeme inaendelea katika eneo la Kisongoni, Donge na Chaani.

Mhe. Mwenyekiti, fedha zilizotengwa kwa mwaka ni Tsh 200,000,000/- na Fedha zilizopapatikana kwa mwaka in Tsh 199,168,241/- ambazo ni sawa na asilimia 99.5%.

KAZI ZA KAWAIDA

Matengenezo Ya Mabomba

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji imefanikiwa kufanya matengenezo ya mabomba katika maeneo mbali mbali kama yanavyosomeka katika taarifa hii.

Marekebisho Ya Umeme

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji Zanzibar katika mwaka wa fedha 2016/2017 ilifanikiwa kufanya marekebisho ya umeme katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba kama inavyoonekana kwenye jaduweli namba 2:

Jaduweli Namba 2: Maeneo yaliyofanyiwa marekebisho ya Umeme

Unguja	**Pemba**
Welezo, Dimani, Mombasa, Mbweni, Kiashange No. 2, Magogoni, Kandwi, Kisongoni, Chaani TASAF, Kaburi kikombe, Mgeni haji ADB, Kibele, Kitogani, Jambiani, M/mchomeke, Chunga No. 9, Uroa – Pongwe, Makunduchi, Ukokongoroni, Tumbatu, Dunga, Bumbwisudi, Bambi, Sebleni, Kinumoshi, Masumbani No 4, Fuoni, Kizimkazi, Kilombero, Bweleo, Mkorogo BH15, Umbuji, Kigongoni, Msikiti mzuri N10, Bwejuu, Mtopepo na Chwaka	Ng'ambwa-2 na Kwapweza, Mtambwe Kaskazini, Bungumi, W B, Jojo, Kwapopo, Mazrui, K Makangale

Matengenezo ya Pampu na Mota Zilizoungua

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji imefanikiwa kufanya matengenezo ya Pampu na Mota zilizoungua katika vituo mbalimbali Unguja na Pemba kama inavyoonekana katika jaduweli namba 3:

Jaduweli Namba 3: Vituo vilivyofanyiwa matengenezo ya Pampu na Mota

Unguja	**Pemba**
Kibele, Msikiti Mzuri, Kizimkazi, Masumbani (Chukwani), Mbweni (Rais), M/Mchomeke No1, Binti Amrani No1, Kiashange ADB 4, Kisongoni, Tazari, Kaburi Kikombe, Kiembesamaki, Bambi TASAF, Mfenesini, Ukongoroni, Uroa/Pongwe, Bweleo, Mbweni BLW, Kwarara, Welezo, Chumbuni, SEMUSO na Mgambo	Mahuduthi, Chambani, Mtambi Mbuzini, Mfikiwa, Mkanyage Saninga, Wingwi Njuguni, Mtam Bimtumwa, Shumba Viamboni

Chanzo: ZAWA

Kutoa Elimu kwa Watumiaji wa Maji

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji katika mwaka wa fedha 2016/2017 imefanya kazi kubwa ya uhamasishaji wa Jamii juu ya umuhimu wa kuchangia huduma ya maji na kutunza miundombinu ya maji. Maeneo yaliyohamasishwa kwa Unguja na Pemba ni kama yanavyoonekana katika jaduweli namba 4:

Jaduweli Namba 4:Maeneo yaliyofanyiwa uhamasishwaji

Unguja	**Pemba**
Paje, Bwejuu, Nungwi, Mkokotoni, Tumbatu, Donge - Kipange, Mahonda, Gamba, Jumbi, Dole, Kianga, Magogoni, Kilimaji, Kihinani, Migombani, Pangawe, Kizimkazi Mkunguni, Kizimkazi Dimbani, Mtende na Kibuteni	Shumba Viamboni, Tumbe, Mbu Limbani, Kizimbani, Mgagadu, Wawi, Gombani, Ole, Kilindi Mtambile, Micheweni

Chanzo: ZAWA

Kujenga na Matengenezo ya *"Well – Head"*

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji imefanikiwa kujenga na kufanya matengenezo ya "Well – head" katika maeneo ya Mwanakwerekwe C, Uwanja wa Mao Tse Tung, Chaani Masingini, Magogoni, Welezo (RH), Jambiani Kivuli, Kigongoni, Kijitoupele, Kilindi No.2 na Ukongoroni kwa Unguja na Tumbe Saninga, Shumbavyamboni, Mbuzini, Changuo, Kwa Bimtumwa, Junguni, Finya kwa Pemba.

Ufungaji wa Mita za Usajili wa Wateja Wapya wa Maji

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Mamlaka imefanikiwa kusajili wateja wapya 2,659 Unguja na Pemba. Aidha, Mamlaka imefanikiwa kufunga mita 1,582.

Kuvilinda, Kuvitunza na Kuviwekea Uzio Vianzio vya Maji

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ya Maji ni usimamizi, utunzaji na uhifadhi wa rasilimali maji katika kutekeleza hayo

Mamlaka ya Maji imeendeleza kazi ya upandaji miti katika maeneo ya Mwanyanya na Kiashange ambapo jumla ya miti 300 imefanikiwa kupandwa.

Ukusanyanyaji wa Mapato

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji Zanzibar katika bajeti ya mwaka 2016/2017ilijipangia kukusanya jumla ya TShs bilioni 5.1 kutokana na mauzo ya maji na mauzo mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2017, jumla ya TShs bilioni 2.045 zimekusanywa sawa na asilimia 40 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka haikuweza kufikia lengo iliojipangia kutokana baadhi ya maeneo kuwa na upungufu wa maji na hata yale maeneo ambayo huduma hii inapatikana vizuri wananchi walio wengi bado hawajaitikia vizuri wito wa kuchangia huduma hii.

IDARA YA NISHATI NA MADINI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nishati na Madini ni taasisi yenye jukumu la kusimamia Sekta ya Nishati na Madini hapa Zanzibar kwa lengo la kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa nishati bora, gharama nafuu inayozingatia uendelevu wa mazingira yaliyo salama na rafiki kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 Idara ya Nishati na Madini ilisimamia na kutekeleza mambo yafuatayo:-

Mradi wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati

Mhe. Mwenyekiti, itakumbukuwa kuwa, katika utekelezaji wa Mradi wa Kujenga uwezo Sekta ya Nishati awamu ya pili, Idara ya Nishati kwa kushirikiana na Ubalozi wa Sweden, ilitiliana saini na Kampuni ya *"Multiconsult ASA*" ya nchini Norway kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Katika mradi huu mambo yafuatayo yamepangwa kutekelezwa:-

i. Utafiti wa Awali wa taarifa za Nishati Nchini, - "*Energy base-line study"*
ii. Kuandaa Mfumo Mkuu wa kuhifadhi takwimu za Nishati, -*"Energy statistics database"*
iii. Kutunga Sheria ya Nishati ya Zanzibar, -*"Zanzibar Energy Act"*

iv. Mpango Mkuu wa matumizi bora ya Nishati,- "*Energy Efficiency Master Plan"*

v. Kuijengea Uwezo Idara ya Nishati na Madini, -"*Strengthening Department of Energy and Minerals"*

vi. Kuijengea Uwezo Idara ya Mipango Sera na Utafiti, -*"Strengthening Department of Planning, Policy and Research"*

vii. Kutoa uelewa wa masuala ya Nishati, -*"Awareness Campaign"*

viii. Mpango wa Utekelezaji wa matumizi bora ya Nishati, -*"Energy Efficiency Implementation Plan"*

ix. Kufanya mapitio ya Sera ya Nishati ya mwaka 2009.

Mhe. Mwenyekiti, Mshauri elekezi ameshaanza kutekeleza mambo yafuatayo kama yanavyoonekana katika taarifa hii namba i mpaka iv :

i. Utafiti wa Awali wa taarifa za Nishati Nchini, - "*Energy base-line study"*
Kazi ya ukusanyaji wa takwimu za nishati kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita kwa madhumuni ya kuandaa mfumo mkuu wa takwimu za Nishati. Kazi hii inaendelea.

ii. Kuandaa Mfumo Mkuu wa kuhifadhi takwimu za Nishati, -"Energy statistics *database*.

Wizara ipo katika hatua ya kumtafuta mkandarasi wa kutengeneza na kuongoza kazi hiyo kwa kusaidiana na Mshauri elekezi wa Mradi huo.

iii. Kufanya mapitio ya Sera ya Nishati ya mwaka 2009 na utungaji wa Sheria ya Nishati ya Zanzibar*"Zanzibar Energy Act".* Mashauriano ya wadau yamefanyika na Rasimu ya awali ya Sera ikotayari na kazi hii inaendelea.

iv. Kuijengea Uwezo Idara ya Nishati na Madini na Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Kazi hizi zimeanza kwa kuwajengea uwezo watendaji wa taasisi husika kwa ziara za kimafunzo nchini Kenya na mafunzo hayo yatakua endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi Idara imeweza kufanya ukaguzi katika maeneo yaliyofungwa mifumo ya umeme wa jua kwa kutathmini ufanisi wa utendaji kazi wake katika ukaguzi huo, imegundulika kuwa mifumo hiyo imetoa mchango mkubwa kwa wananchi katika maendeleo ya jamii, hata hivyo jitihada za ziada zinahitajika katika kuwajengea uelewa

wananchi katika masuala ya umiliki, matumizi na matengenezo ya mifumo hiyo. Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini imeazimia kuchukua hatua za ziada ili kupunguza dosari hizo.

Kuwapatia elimu wananchi katika masuala ya nishati (Mafuta, Gesi Asilia na Nishati Mbadala)

Wizara kupitia Idara ya Nishati imetekeleza lengo hilo kwa kuandaa vipindi vitano (5) vya Redio na Televisheni kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) na vituo binafsi ili kuwapa wananchi uelewa wa masuala ya Mafuta, Gesi Asilia na Nishati Mbadala. Aidha, Semina tatu (3) za kujenga uelewa wa masuala ya Mafuta na Gesi Asilia zilizowashirikisha wadau mbali mbali zilifanyika.

Utekelezaji wa Mradi wa Nishati Mbadala unaofadhiliwa na Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaendelea na azma yake ya kukamilisha Mradi wa Utafiti wa Nishati Mbadala ili kujua uwezekano wa Zanzibar kupata umeme kwa njia mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, Katika utekelezaji wa mradi huu, takwimu za kuangalia mwenendo wa upepo na upatikanaji wa jua zinaendelea kukusanywa tokea mwezi wa Agosti 2015 hadi hii leo. Takwimu zinazoendelea kukusanywa zinaashiria uwezekano mzuri wa matumizi ya nishati mbadala kwa Zanzibar, hata hivyo takwimu hizo zinaendelea kukusanywa na kufanyiwa uchambuzi kwa lengo la kuhakikisha ubora wa takwimu hizo. Takwimu hizo zinafanyiwa uchambuzi (analysis) na Kampuni ya GOPA-INTEC kutoka Ujerumani na hatimae kuandaliwa Ripoti Kamili ya Utafiti itakayojumuisha mipango ya usafirishaji wa vifaa, Uchambuzi wa Kimazingira, Mipango ya kifedha itakayokimu miradi ya Nishati mbadala na uwezo wa Miundombinu ya umeme iliopo ili kuelewa umadhubuti wake wa kuhimili na kusafirisha umeme utakaozalishwa kutokana na nishati mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na utafiti wa taarifa za kiufundi, uwekezaji wa miradi ya nishati mbadala unahitaji usimamizi makini ili kufikia lengo lililokusudiwa. Kampuni ya MWH kutoka Ubelgiji inaendelea na kazi ya kuandaa mazingira ya kisheria na leseni na uchambuzi wa kina wa gharama na faida ya Miradi kwa ajili ya uwekezaji.

Aidha pamoja na kazi hizo, Kampuni ya MWH itahusika na kujenga mazingira shirikishi ya kisekta kwa upande wa Serikali na sekta binafsi na kujenga uelewa kwa wananchi juu ya Nishati Mbadala na matumizi bora ya nishati. Kampuni hii inatarajiwa kukamilisha kazi zake ifikapo mwezi wa Juni 2018. Baada ya kukamilika kwa kazi hizo, Zanzibar itakuwa katika mazingira bora ya uwekezaji katika Miradi ya Nishati mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi na viongozi wote kwa mashirikiano yao katika kufanikisha mradi huu na waendelee kudumisha mashirikiano na usalama katika maeneo na miundombinu inayotumika katika mradi huu.

Kazi za Kawaida

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa kazi za kawaida katika mwaka wa fedha 2016/17 Idara ilitekeleza mambo yafuatayo:-

Kushiriki katika masuala yote ya nishati ya Kitaifa, Kikanda, na Kimataifa

Katika utekelezaji wa hili, Idara imeweza kushiriki katika mikutano ishirini na nane (28) iliyofanyika ndani na nje ya nchi ikiwemo vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika masuala ya Nishati.

Kuendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuimarisha na kutekeleza mipango ya mafunzo ya Mafuta na Gesi Asilia

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada za kushirikiana na washirika mbali mbali wa maendeleo, Idara imefanikiwa kuendesha semina nne (4) kwa mwaka wa fedha 2016/17 zinazohusiana na masuala ya Mafuta na Gesi Asilia ambazo zinawashirikisha wafanyakazi wa Wizara na Idara ya Nishati na Madini ikiwa ni sehemu ya kuwajengea uwezo Kitaaluma.

Mhe. Mwenyekiti, mnamo tarehe 15 Novemba 2016, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein alitia saini Sheria nambari 6 ya mwaka 2016 inayohusiana na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar baada ya kupitishwa kwa mswaada wa Sheria hiyo na Baraza lako tukufu hili.

Aidha, katika utekelezaji wa Sheria hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na

Gesi Asilia (*ZPRA*) na ipo katika mchakato wa kuanzisha Kampuni ya Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (*ZPDC*). Halikadhalika, rasimu ya mkataba wa mafuta na gesi asilia (*MPSA*) ambao utatumika katika uwekezaji wa masuala ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia Zanzibar ni sehemu ya mafanikio yaliyotokana katika kipindi hiki.

SHIRIKA LA UMEME

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Umeme lina jukumu la usambazaji, uimarishaji na upatikanaji wa huduma bora ya umeme. Katika kutekeleza jukumu hilo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, shirika limetekeleza yafuatayo:-

Ukusanyaji wa Mapato

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016-2017, shirika lilikadiria kukusanya Tsh. 108,114,620,732 kutokana na biashara ya kuuza umeme na huduma nyenginezo zinazotolewa kwa wananchi. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2017 shirika limekusanya jumla ya Tsh. 76,527,009,443 sawa na asilimia 71% ya makadirio.

Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi shirika lilikadiria kutumia Tsh. 107,840,528,872 hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2017 shirika limetumia Tsh. 73,976,971,910 sawa na asilimia 69% ya makadirio kama inavyoonekana katika Jaduweli Nam. 5.

Jaduweli Namba 5: Matumizi ya Shirika la Umeme 2016/2017

MAELEZO	**MAKADIRIO YA MWAKA 2016-2017**	**MAT Julai,201**
Ununuzi wa Umeme TANESCO	62,756,171,561	
Kazi za Kawaida	33,366,602,806	
Kazi za Maendeleo	11,717,754,505	
Jumla	**107,840,528,872**	

Chanzo: ZECO

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA

Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme

Mhe. Mwenyekiti, uimarishaji wa miundombinu ya njia kubwa na ndogo inayosambaza umeme ni jambo muhimu sana kwa shirika, kwani unasaidia kuimarika kwa upatikanaji wa huduma ya umeme na kupunguza upotevu kwenye maeneo. Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2017 shirika limebadilisha waya chakavu zenye urefu wa kilomita 18.3, nguzo mbovu 3,003 na kupima *transformer* 450 kwenye maeneo ya Mijini na Vijijini pamoja na kuzifanyia marekebisho *transformer* zilizokuwa na matatizo, ili kuhakikisha kwamba hali ya upatikanaji wa huduma bora ya umeme inapatikana wakati wote.

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Usambazajiwa Umeme Vijijini

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, shirika lilikadiria kutumia Tsh. 5,558,993,025 kwa kusambaza umeme vijijini. Kati ya fedha hizo, Tsh. 3,558,993,025 ni za mfuko wa shirika na Tsh. 2,000,000,000 ni mchango kutoka mfuko wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya Tsh. 2,776,000,000 zilitumika kwa ununuzi wa vifaa vya umeme, waya, nguzo, transfoma pamoja na kulipa fidia ya mali na mazao ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kazi za upelekaji umeme katika kisiwa cha Fundo zinaendelea ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi, 2017 kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:-

i. Ujenzi wa laini kubwa ya umeme yenye urefu wa kilomita 7.29 umekamilika.
ii. Ujenzi wa laini ndogo ya umeme yenye urefu wa kilomita 8 tayari umekamilika.
iii. Ufungaji wa *transformer* 4 kwa ajili ya Vijiji vya Ndooni, Chumbuni, Ngagu, Kunguni, Mabaoni, Kimeleani na Nafasitele tayari umekamilika.

Aidha, katika kipindi hicho, shirika pia limejenga kilomita 22.4 ya umeme mkubwa na kilomita 83.7 za laini ndogo ya Umeme pamoja na uwekaji wa *transformer* 19 za kusambaza umeme katika Vijiji 47 kwa Unguja na Pemba. Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho (D).

Mradi wa Ufungaji wa Mita za TUKUZA

Mhe. Mwenyekiti, lengo la mradi huu ni kukuza ukusanyaji wa mapato ya shirika na kupunguza malimbikizo ya madeni. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, shirika limenunua mita 20,208 za TUKUZA kwa gharama ya Tshs. 1,778,304,000 kati ya hizo, mita 10,268 zimefungwa kwa wateja wapya na mita 9,940 zimefungwa kwa ubadilishaji wa mita za kawaida na mbovu.

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR - (*ZURA*)

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (*ZURA*) imeanzishwa kwa lengo la kudhibiti na kusimamia masuala yote yanayohusiana na huduma za maji na nishati Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Mhe. Mwenyekiti, *ZURA* imeweza kuleta uimara wa soko la bidhaa za mafuta ya petroli hapa Zanzibar. Kabla ya uanzishwaji wake, soko la bidhaa za mafuta ya petroli halikuwa la uhakika sana na kulikuwa na ukosefu wa mafuta wa mara kwa mara. Wananchi walipata shida ya kuadimika kwa mafuta ya petroli na diseli na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi, hususan wafanyakazi na wafanyabiashara wanaofanikisha kazi zao kwa kuwepo kwa usafiri wa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuwahakikishia wafanya biashara wa bidhaa za mafuta ya petroli wanapata faida na wananchi hawatozwi bei ya petroli isiyostahiki, *ZURA* imeweza kuweka utaratibu wa fomula ambayo inamuhakikishia mfanyabiashara na wateja wote wanapata bei inayostahiki kwa mujibu wa bei halisi za bidhaa hizo katika Soko la Dunia, na hivyo kuondoa utata wa wafanyabiashara kuligomea soko la mafuta ama kuficha bidhaa hizo.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha *ZURA* kuwa mdhibiti bora wa viwango vya kimataifa, Mamlaka imeandaa kanuni ambazo zitasimamia udhibiti wa huduma na upatikanaji bora wa huduma hizo kwa viwango vinavyotakiwa.

i. Kanuni za Usimamizi wa Vituo vya Mafuta *(The Petroleum Filling Stations Regulations).*

ii. Kanuni za Usimamizi ya Biashara ya Mafuta *(Petroleum Supply Regulations).*

iii. Kanuni za Uagizaji Mafuta wa Pamoja *(Petroleum Bulk Procurement Reulations).*

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ambazo zimeshatengenezwa ambazo zinasubiri kuwasilishwa katika Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka na hatimae kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mwishowe kusainiwa na Mhe. Waziri zinaonekana katika taarifa yangu kanuni moja mpaka sita:

i. Kanuni ya Huduma za Uzalishaji Umeme *(The Electricity Generation Services Regulations).*

ii. Kanuni ya Huduma za Usafirishaji Umeme *(The Electricity Transmission Services Regulations).*

iii. Kanuni ya Huduma za Usambazaji Umeme *(The Electricity Distribution Services Regulations).*

iv. Kanuni ya Huduma za Uunganishaji Umeme *(The Electricity Supply Services Regulations).*

v. Kanuni ya Usambazaji wa Huduma za Maji *(The Water Supply Licensing Regulations).*

vi. Kanuni ya kutatua migogoro kwa wateja *(Customer Complaints Handling Procedures).*

Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (*ZURA*), inaendelea na uandishi wa kanuni zifuatazo:

i. Kanuni ya maji (*Water Regulation*)
ii. Kanuni ya Gesi (*Gas Regulation*)
iii. Kanuni ya Vilainishi vya vyombo vya moto (*Petroleum Based lubricants Regulation*)

Mhe. Mwenyekiti, *ZURA* imefanikiwa kuleta mfumo wa kutoa leseni kwa vituo vya mafuta. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2017 Mamlaka imeshatoa leseni 56 kwa vituo vya mafuta, 44 vya Unguja na 12 vya Pemba.Vituo vyote vya mafuta vya Zanzibar vinavyotambulika na Mamlaka vinakaguliwa alau mara moja kwa vipindi vya miezi mitatu mitatu. Hii ni kwa ajili ya kuhakikisha kuwa vituo vinakidhi viwango ambavyo vimewekwa na Mamlaka. Viwango hivyo

ambavyo vimewekwa na wataalamu wa mafuta vina lengo la kuhakikisha usalama wa vituo hivyo vya mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa kuijengea uwezo taasisi, hadi sasa *ZURA* imefanikiwa kupata wafanyakazi ishirini na tisa, 25 kwa ajili ya Ofisi za Unguja na wanne 4 kwa ofisi za Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka imeweza kujitangangaza kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa vya kujitangaza kama fulana, vitabu vya kumbukumbu, kalenda, kalamu na maji. Mamlaka pia imejishajihisha katika huduma za kijamii kwa kutoa misaada mbalimbali ikiwemo nyumba za wazee, watoto yatima pamoja na kushiriki maadhimisho ya shughuli za kitaifa ikiwa pamoja na sherehe za elimu bila ya malipo na maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi.

Aidha, Mamlaka imeweza kutayarisha miongozo kwa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kanuni ya Utumishi (*Staff Regulation*) na miongozo ya taratibu na nidhamu za kazi (*Staff Code of Conduct*), ambayo itakua miongozo kwa wafanyakazi wote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa utoaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi, mafunzo yanaendelea kufanyika ndani na nje ya nchi. Kutokana na ugeni walionao wafanyakazi wa Mamlaka katika fani ya Udhibiti, na kwa kufahamu haja iliyopo ya kuwapatia mafunzo zaidi ya vitendo wafanyakazi wake, Mamlaka imeweza kutembelea taasisi nyengine za udhibiti na Mamlaka zinazosimamia nishati na maji zilizomo nchini Rwanda, Kigali, Namibia, Mombasa na Nairobi, Kenya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, katika kutekeleza programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati jumla ya Tshs. 48,978,195,000 ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2017, fedha zilizoingizwa ni Tshs. 35,832,062,368 sawa na asilimia 73% ya makadirio.

Programu PN0106: Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

Mhe. Mwenyekiti, lengo la programu hii ni kuimarisha uhifadhi na utunzaji wa mazingira pamoja na kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi Zanzibar. Programu hii inatekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (*ZEMA*) pamoja na Idara ya Mazingira kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko Tabianchi ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ilifanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:

Programu ndogo ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ndogo inatekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na Idara ya Mazingira ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

Kuandaa Kanuni juu ya sheria mpya ya Mazingira ya mwaka 2015

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya Kanuni 5 za Mazingira zimetayarishwa kwa ajili ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ya mwaka 2015. Kanuni hizo ni Maliasili Zisizorejesheka; Uangamizaji wa vitu visivyofaa kwa matumizi; Kampuni za kufanya Tathmini za Kimazingira Zanzibar; Gharama za malipo ya tozo na ada za kimazingira; na Mkakati wa Tathmini za Kimazingira (*Strategic Environmental Assessment – SEA*).

Kufanya operesheni za kusimamia marufuku ya mifuko ya plastiki

Mhe. Mwenyekiti, Jumla ya operesheni 87 za mifuko ya plastiki zimefanyika ambapo jumla ya watu 140 wamekamatwa na jumla ya tani 2.4 za mifuko ya plastiki zimekamatwa na kuangamizwa. Faini ya Tsh. 14,034,000 zimetozwa kwenye mahakama husika. Kwa jumla mifuko ya plastiki imepungua kuzagaa mitaani kama ilivyokuwa imezoeleka.

Kufanya Operesheni za kusimamia maliasili zisizorejesheka

Mhe. Mwenyekiti, mikutano ya wadau mitatu (3) imefanyika, kikosi kazi maalum kinachosimamiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mjini Magharibi kimeundwa na kimeanza kufanya kazi zake. Jumla ya operesheni 41 za kudhibiti uchukuaji holela wa maliasili zisizorejesheka zimefanyika ambapo jumla ya magari 18 ya ng'ombe na 1 ya punda, gari 13 za mchanga zimekamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kufanya ziara za ufuatiliaji wa kimazingira

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa lengo hili jumla ya viwanda 27 vya matofali vimekaguliwa katika maeneo mbalimbali ya Unguja. Maeneo mawili (2) ya majaa ya Kiwengwa na Sebleni na eneo moja (1) la uchimbaji wa kifusi la Tunguu yamekaguliwa na amri ya kusimamisha utupaji wa taka na uchimbaji wa kifusi katika maeneo hayo (*stop order*) imetolewa. Aidha, majaa makuu

katika Wilaya zote za Unguja na Pemba yamekaguliwa na kutolewa ushauri wa kimazingira.

Kusimamia Tathmini za Kimazingira kwa Miradi

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya miradi 41 imefanyiwa tathmini za mazingira na kupewa vyeti vya kimazingira kwa ajili ya kuendelea na hatua nyengine za miradi hiyo. Aidha, masharti ya kimazingira yameambatanishwa na vyeti hivyo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa miradi hiyo inaendeshwa bila ya kuwa na uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira.

Kufanya ufuatiliaji wa miradi ya kiuchumi na kimaendeleo

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya miradi 130 imefanyiwa ufuatiliaji wa kimazingira, miradi mingi imeonekana kuanza kutekeleza masharti ya mazingira, hata hivyo juhudi zaidi zinahitaji kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa miradi yote inatekeleza masharti ya kimazingira.

Kukuza uelewa na ushiriki wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya vipindi saba (7) vya redio na 3 vya TV vimeandaliwa na kurushwa kupitia *ZBC redio* na *TV*. Vipindi vya redio vilikuwa vinahusu maliasili zisizorejesheka (2), Athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya Kilimo (2), Tathmini za Athari za Kimazingira (2) na umuhimu wa hifadhi ya kasa (1). Aidha, vipindi vya TV vilikuwa vinahusiana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira namba 3 ya mwaka 2015 (1), usafi wa Mazingira na usimamizi wa taka (2).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, katika kutekeleza Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi jumla ya Tshs. 678,298,000/= ziliidhinishwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2017, fedha zilizoingizwa ni Tsh 388,356,531/= sawa na asilimia 57% ya makadirio.

Utekelezaji wa Kazi za Maendeleo

Mhe. Mwenyekiti, programu hii vilevile ilipangwa kutekeleza kazi za maendeleo kupitia mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya ukanda wa Pwani (*LDCF*), mradi huu ulitekeleza shughuli za upandaji wa mikoko katika maeneo ya Kilimani, Kisakasaka, Tovuni, Ukele, Kisiwa Panza na Tumbe. Mafunzo kwa ajili ya

upandaji wa mikoko kwa wananchi 379 wa maeneo hayo yameshatolewa na Jumla ya hekta 254.3 na mikoko zinategemewa kupandwa kwenye maeneo hayo.

MUELEKEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa bajeti ya wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2016/2017, sasa naomba kuwasilisha muelekeo wa bajeti yenye kuzingatia programu ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ina jumla ya Programu Kuu nne ambazo ni;

a. Programu PN0101: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi.
b. Programu PN0102: Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi
c. Programu PN0105: Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati.
d. Programu PN0106: Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya Tshs. bilioni 47,508,574,000 zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wa programu hizi nne.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu kutoa maelezo kuhusu Programu na Programu ndogo zinazohusiana na wizara yangu kama ifuatavyo:-

Programu PN0101: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inajukumu la kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa Kazi za Wizara ambapo matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kukuza ufanisi katika utawala wa rasilimali ardhi pamoja na utoaji huduma za kijamii. Programu itasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji, na Afisi Kuu Pemba ambapo jumla ya Tsh. 1,959,901,000 zinatarajiwa kutumika kwa utekelezaji wake. Programu hii imegawanyika katika Programu ndogondogo kama ifuatavyo:-

Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni Uratibu wa Shughuli na Kazi za Wizara kwa Ufanisi. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga Kuratibu na Kuandaa Mipango na Miongozo ya Kisera ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara, kuratibu uandaaji wa Sheria zilizochini ya Taasisi za Wizara, Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa Programu, Miradi ya Wizara na Kuandaa Tafiti kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma bora katika sekta za wizara.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Tsh 202,643,000/=.

Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji

Mhe. Mwenyekiti, lengo la kuwepo kwa programu hii ni kusimamia uendeshaji wa wizara na Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali watu. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kuendeleza kutoa huduma za uendeshaji, kuendeleza kuifanyia matengenezo afisi, kuimarisha mawasiliano na utunzaji wa kumbukumbu mbalimbali za afisi, kuwapatia fursa na stahiki wafanyakazi wa wizara na kukuza soko la ajira kwa sekta za ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha program hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh. 892,933,000/=

Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba, ambapo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kuratibu shughuli za Wizara kwa Pemba, kuimarisha kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa programu na miradi ya Maendeleo ya Wizara Pemba na Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tshs. 864,325,000/=.

Programu PN0102: Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inajukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi (*security of land tenure*) kwa maendeleo ya nchi. Matokeo

ya muda mrefu yanayotarajiwa ni kuwa na matumizi ya ardhi yaliyo bora na yenye ufanisi. Programu hii inasimamiwa na Kamisheni ya Ardhi na Mahakama ya Ardhi ambapo jumla ya Tsh. 2,515,001,000/= zinatarajiwa kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, programu hii imegawanyika katika programu ndogondogo kama ifuatavyo:

Programu ndogo ya Utawala wa Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la Programu ndogo hii ni kuhakikisha usalama wa umiliki wa ardhi kwa wananchi ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu hii ni ugawaji na usimamizi wa ardhi kwa matumizi mbalimbali, uthamini wa ardhi na usimamiaji wa shughuli za upimaji na ramani pamoja na usajili wa ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia Kamisheni ya Ardhi katika programu ndogo ya Utawala wa Ardhi imepanga kutekeleza kazi zake kama inavyosomeka katika taarifa yangu kifungu kidogo 1 mpaka 10.

i. Kutayarisha hati za umiliki wa haki ya matumizi ya Ardhi 1,400 na mikataba ya ukodishaji Ardhi 140.
ii. Kutayarisha Vitambulisho vya umiliki wa matumizi ya Ardhi za Eka tatu 60.
iii. Kuingiza taarifa za Ardhi katika mfumo wa kompyuta.
iv. Kukagua maeneo 140 yatakayohitajika kutayarishiwa mikataba ya uwekezaji na maeneo ya 65 ya Eka tatu.
v. Kufanya kazi 350 za uthamini ardhi kwa madhumuni mbalimbali.
vi. Kuendeleza kazi za utambuzi wa kumjua mwenye haki ya matumizi ya ardhi kwa maeneo 1,000 Unguja na Pemba.
vii. Kuendeleza shughuli zote za upimaji wa viwanja 600, upimaji wa mipaka, upimaji wa alama msing na utayarishaji wa ramani .
viii. Kuendeleza wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo pamoja na kuimarisha uwezo wa utendaji kwa kuwapatia vitendea kazi vinavyohitajika.
ix. Kuendelea na usajili kwa maeneo ya Matarumbeta na Jang'ombe Urusi kwa Unguja na maeneo ya Limbani, Wara na Chokocho kwa Pemba.
x. Kutoa kadi 800 za usajili kwa wanachi waliokwisha kusajiliwa

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh 1,142,576,000 /=.

Programu ndogo ya Upangaji wa Miji na Matumizi ya Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni Kuhakiksha Uwiano wa matumizi ya Ardhi kati ya Matumizi ya Uchumi na Kijamii. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamisheni ya Ardhi kupitia Idara ya Mipango Miji na Vijiji inakusudia kuongeza bidii zaidi ili kuhakikisha haiba ya mji wa Zanzibar inabadilika na kuwa bora zaidi. Kufikia azma hii, Idara ya Mipango Miji kupitia programu hii imekusudia kutekeleza malengo makuu matatu kama ifuatavyo:

i. Kuhimiza matumizi bora na endelevu ya ardhi kwa faida za kiuchumi na ustawi wa jamii Unguja na Pemba.

ii. Kuipa nguvu mifumo ya kisheria ya maendeleo ya ardhi kwa kuandaa Kanuni na miongozo ya ujenzi.

iii. Kuongeza uwezo wa wafanyakazi na washirika wake wote kwa kuwapatia mafunzo pamoja na kuimarisha kitengo cha utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Tshs. 1,052,657,000/=.

Programu ndogo ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni kuhakikisha kuwepo kwa utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa haraka zaidi kadri inavyojitokeza, ambapo matokeo ya muda mfupi (*output*) yanayotarajiwa katika utekelezaji wake ni pamoja na kupungua kwa migogoro ya ardhi. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuongeza ufanisi katika utoaji wa maamuzi ya kesi zinazohusiana na migogoro ya ardhi kwa lengo la kuzitolea maamuzi kesi 260 kwa mwaka kwa Unguja na Pemba.
ii. Kufanya matengenezo ya jengo la Mahakama ya Ardhi la Mkoa wa Kaskazini Pemba (Wete).

iii. Kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na shughuli za Mahakama ya ardhi na utatuzi wa migogoro ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Tshs. 319,768,000.

Programu PN0103: Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la programu hii ni kuhakikisha upatikanaji wa Huduma za Maji na Nishati zinazotosheleza mahitaji ya jamii. Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa ni upatikanaji wa huduma bora na endelevu za Maji na Nishati pamoja na kusimamia zoezi zima la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na Gesi Asilia.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii itasimamiwa na Mamlaka ya Maji, Idara ya Nishati na Madini, Mamlaka ya Kudhibiti Huduma za Maji na Nishati, Shirika la Umeme na Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mamlaka ya Maji kupitia program hii ya Usimamizi wa huduma za Maji na Nishati imepanga kutekeleza kazi kama zivyosema katika taarifa hii namba moja mpaka tano.

i. Kuendeleza Programu ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini kwa kutekeleza mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka kifedha (ADF 12) na Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya maji Mjini (JICA), na Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Mjini (INDIA)
ii. Kuendeleza Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini kwa kutekeleza Mradi wa uchimbaji wa visima unaofadhiliwa na Serikali ya China na Mradi wa kuviendeleza Visima visima vilivyochimbwa na Ras Al khaimah.
iii. Kuendeleza kazi za kawaida za kufanya matengenezo ya Miundombinu ya Maji ili kupunguza upotevu wa maji..
iv. Kuendeleza kazi za Kulinda na kuhifadhi vianzio vya maji kwa kuimarisha ulinzi, upandaji wa miti na ujenzi wa uzio.
v. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuvilinda vianzio vya maji na miundombinu yake, kuchangia huduma ya maji na matumizi bora ya maji kwa maeneo mbalimbali Mijini na Vijijini Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ukusanyaji wa Mapato Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 inatarajia kukusanya jumla ya Tsh bilioni 5.908 kutokana na mauzo ya maji na mapato mengineyo. Aidha ili kuongeza makusanyo ya fedha Mamlaka imejipanga kuongeza vituo vya mauzo ya maji na huduma kwa wateja Mijini na Vijijini, kuimarisha miundombinu ya maji ili wananchi wanufaike na huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Baraza lako Tukufu ninawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuwa karibu na Wananchi katika kulinda, kuhifadhi, kuenzi na kutunza, miundombinu na vyanzo vya maji pamoja na kuitikia wito wa uchangiaji wa huduma ili kuiwezesha Mamlaka kutoa huduma endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Idara ya Nishati na Madini, kupitia program hii ya Usimamizi wa huduma za Maji na Nishati imepanga kutekeleza malengo kama inavyosomeka kuanzia namba moja mpaka saba.

i. Kushiriki katika masuala ya nishati ya kitaifa, kikanda, na kimataifa.
ii. Kushirikiana na taasisi ya ZURA katika kuendelea kusimamia upatikanaji wa bidhaa za mafuta na gesi ya majumbani Zanzibar.
iii. Kushirikiana na ZPRA katika kuhakikisha masuala ya utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia yanafanyika kwa ufanisi mkubwa kwa maslahi ya Wazanzibari.
iv. Kuendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuimarisha na kutekeleza mipango ya mafunzo ya Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kutoa elimu kwa wananchi.
v. Kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa mafuta na gesi asilia Zanzibar.
vi. Kuendeleza kazi za Mradi wa Nishati Mbadala pamoja na juhudi za kuwapatia wananchi wa Zanzíbar elimu juu ya matumizi bora ya Nishati Sanifu na Nishati Mbadala (*Energy efficiency and Renewable energy).*
vii. Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa kuijengea uwezo sekta ya Nishati Zanzibar *(Zanzibar Energy Sector Support Project).*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Shirika la Umeme, kupitia program hii ya Usimamizi wa huduma za Maji na Nishati imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuendeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Mijini na Vijijini.
ii. Kuendeleza ufungaji wa Mita 16,105 za TUKUZA.

iii. Kutekeleza Mradi wa uimarishaji wa miundombinu ya umeme "*Capacity Building on Maintanances"* unaofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo kutoka Serikaliya Norway.

iv. Utekelezaji Mradi wa Uimarishaji wa Sekta ya Nishati awamu ya pili unaofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo kutoka Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la SIDA.

Mapato na Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mapato Shirika kwa mwaka wa fedha 2017/2018 linakadiria kukusanya Mapato ya jumla ya Tshs 128,222,588,849.00 kutokana na mauzo ya umeme na huduma nyenginezo. Aidha, Shirika linatarajia kutumia jumla ya Tsh 126,682,331,636.00 kwa kazi za Kawaida na za Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati kupitia program hii ya Usimamizi wa huduma za Maji na Nishati imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuandaa kanuni za Mamlaka zitakazosimamia udhibiti wa utoaji wa huduma za maji, umeme na Nishati

ii. Ujenzi wa majengo ya ofisi za Mamlaka pamoja na ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri kwa Unguja na Pemba

iii. Kufanya shughuli za uhamasishaji kwa jamii juu ya uwepo wa ZURA, kazi zake na dira yake.

iv. Kuandaa nyenzo na kutatua migogoro itakayowasilishwa Mamlaka kutoka kwa wadau wake, *ZAWA, ZECO*, kampuni za mafuta, wauzaji wa gesi baina yao na watumiaji(*Customer Complaint Regulation*).

v. Mafunzo na ziara za ndani na nje kwa wafanyakazi wa Mamlaka kwa utaratibu uliopangwa.

vi. Kuandaa mfumo wa pamoja wa uleteji wa mafuta (*Bulk Procurement System*) pamoja na Kutayarisha mfumo wa kuweka alama za mafuta (*Petroleum inspection and Marking System*)

vii. Kufanya utafiti wa maeneo yanohitaji miundombinu mipya au kuimarisha kwa ajili ya usambazaji wa huduma.

viii. Kufanya upembuzi yakinifu (Feasibility Study) kwa eneo la uwekezaji wa bohari ya mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukamilisha shughuli zilizopangwa, Mamlaka imepanga Bajeti ya Tsh. 6,530,436,000/= kwa ajili ya shughuli za maendeleo

na kazi za kawaida ambazo zitatokana na makusanyo ya mapato ya Mamlaka kupitia vyanzo vikuu vikiwemo:-

i) Tozo ya Udhibiti wa huduma inazozisimamia
ii) Maombi ya Leseni na Usajili
iii) Ada na penalti

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kupitia program hii ya Usimamizi wa huduma za Maji na Nishati imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kufanya ukarabati wa jengo la ofisi ya Mamlaka na kuipatia vitendea kazi.
ii. Kujenga uelewa kwa wananchi juu ya masuala ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.
iii. Kuandaa kanuni na miongozo ya kitaalamu kwa ajili ya kudhibiti shughuli za utafutaji wa mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.
iv. Kudhibiti shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na Gesi Asilia kwa kampuni zitakazopewa vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii ya Usimamizi wa Huduma za Maji na Nishati kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Tsh. 41,438, 242,000**.**

Programu PN0106: Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

Mhe. Mwenyekiti, proramu hii itatekelezwa kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi na utekelezaji wake utaimarisha usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu hii ni kuhakikisha usimamizi endelevu wa masuala ya kimazingira, ambapo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Programu hii imepanga kutekeleza kazi kama zinavyosomeka kifungu kidogo moja mpaka nane.

i. Kutayarisha Kanuni 6 za usimamizi wa mazingira.
ii. Kufanya operesheni 96 za kusimamia marufuku ya mifuko ya plastiki
iii. Kufanya operesheni 96 za kusimamia maliasili zisizorejesheka
iv. Kufanya ziara 84 za ufuatiliaji wa kimazingira
v. Kusimamia Tathmini za Kimazingira kwa miradi 58

vi. Kufanya ziara za ufuatiliaji wa miradi 84 ya kiuchumi na kimaendeleo
vii. Kukuza uelewa na ushiriki wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa Mazingira kupitia vipindi 20 vya Radio (14) na TV (6).
viii. Kufuatilia vilabu 48 vya Mazingira vya Maskuli.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa Programu hii ndogo vile vile itatekelezwa kupitia mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya ukanda wa Pwani (*LDCF*), mradi wa kuimarisha usimamizi wa mazingira, maliasili na mabadiliko ya Tabianchi Zanzibar (*UNDP*) na mradi wa kukuza uwezo wa kitaifa wa kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (*ADB-ACCF*) ambapo utekelezaji wake utahitaji mashirikiano makubwa kutoka kwa wadau mbali mbali kuhusiana na Mabadiliko ya Tabianchi. Miongoni mwa kazi zitakazotekelezwa kupitia miradi hiyo ni pamoja na Upandaji wa mikoko kwa maeneo mbali mbali yaliyoathirika, Ujenzi wa ukingo wa bahari kisiwa Panza, ujenzi wa kuta za kuelekea baharini Kilimani, kuwajengea uwezo watendaji juu ya masuala ya mabadiliko ya Tabianchi na kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa (*LGAs*) na makundi tofauti katika jamii juu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Tshs. 1,595,431,000.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwatumikia Wananchi wenzangu kupitia Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Nchi marafiki, Mashirika ya Kimataifa na yasiyo ya Kimataifa, Sekta binafsi, NGOs, CBOs na wananchi kwa jumla kwa mashirikiano makubwa waliyoyaonesha kwa Wizara yangu kwa misaada yao ya hali na mali waliyoitoa na wanayoendelea kutoa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara hii. Washirika hao ni JAPAN, NORWAY, SWEDEN, CHINA, FINLAND, HOLLAND, INDIA, EU, UNICEF, UNDP, JICA, Sida, OfD, UN HABITAT, AfDB, TASAF, NORAD, BENKI YA DUNIA, RAK GAS TANZANIA, STATOIL, SHELL, lakini sisahau wananchi wa Zanzibar, pamoja na wale wote ambao kwa bahati mbaya hatukuweza kuwataja. Tumepata faraja kubwa sana kwa michango yao

kwa maendeleo ya nchi yetu, tunaahidi kuienzi na kuiendeleza na kuithamini michango hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani maalumu nazitoa kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Ndugu Juma Makungu Juma kwa mashirikiano yake makubwa anayoendelea kunipa katika kuongoza Wizara hii. Vile Vile shukurani kwa Katibu Mkuu Ndugu Ali Khalil Mirza, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Tahir Mohammed Khamis, Katibu Mtendaji Kamisheni ya Ardhi, Wakurugenzi, Mameneja, Afisa Mdhamini, Wenyeviti wa Bodi, Mahakimu na Maafisa wa ngazi zote pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ambao wamenipa mashirikiano yao ya hali ya juu kwa wakati wote na kutuwezesha kutekeleza malengo na majukumu yetu kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho napenda kuishukuru sana Jumuiya ya Wanawake Tanzania kwa uamuzi wao wa kunipendekeza kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuamini kuwa nitaendelea kuwatumikia ipasavyo. Aidha, nawashukuru wananchi wote ambao wamefuatilia na kusikiliza hotuba yangu hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu wayapokee, wayajadili kwa kina, watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe makadirio haya. Tuna imani kubwa kuwa michango ya waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako hili itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza programu kuu na programu ndogo nilizozieleza, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya Tsh Bilioni 47,508,574,000 na pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya Tsh Bilioni 10,035,127,000 kutokana na vianzio mbali mbali vilivyomo ndani ya Wizara yangu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Kwa ufafanuzi zaidi ninaomba muangalie kiambatanisho “E1, E2 na E3”

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

KIAMBATISHO “C”:Visima Vilivyochimbwa na Mradi wa Ras Al Khaimah ambavyo tayari vimeendelezwa na vimeshaanza kutoa huduma.

S/N	Shehia	Mahala	
Mkoa wa Mjini Magharibi			
1	Welezo Waterworks	Welezo Jeshini	
2	Chumbuni	Chumbuni Wireless Station	
3	Mwanakwerekwe “C”	Mwanakwerekwe “C” School	
4	Shakani	Buyu (Faculty of Marine Science of UDSM)	
	Jumla		
Mkoa wa Kusini Unguja			
1	Makunduchi	Tangini	
		Kilimo/Usalama	
2	Uzini	Uzini	
	Jumla		
	Mkoa wa Kaskazini Unguja		
1	Kiombamvua	Michungwa Miwili /Majimekundu	
2	Kinduni	Kinduni	
3	Pangeni	Boma	
	Jumla		
Jumla Unguja			
Mkoa wa Kusini Pemba			
1`	Mkungu	Mkoroshoni (Mahuduthi)	
2	Chambani	Bonde la Kwapopo	
3	Mtambile	Skuli ya Mtambile	
4	Kwa Changawe	Kwa Changawe	
5	Mbuzini	Mbuzini	
6	Mfikiwa	Mfikiwa	
7	Mkanyageni	Kwa mabata	

8	Mahuduthi	Mahuduthi	
9	Mgogoni	Wawi -Kwa Bimtumwa	
	Jumla		
Mkoa wa Kaskazini Pemba			
1	Finya	Field Force	
2	Tumbe Kusini	Saninga	
3	Wingwi Njuguni	Makundani (Mlindo)	
4	Mtambwe Kaskazini	Uondwe	
5	Shumba Viamboni	Mikinduni	
	Jumla		
Jumla Pemba			
JUMLA KUU ZANZIBAR			

Kiambatanisho “D”

Vijiji vilivyobahatika kusambaziwa Umeme:

UNGUJA	**PEMBA**
Bumbwini Pangatupu	Ole Hozi la ng’ombe
Tunguu Mji mpya	Makangale
Ndunduke	Wawi Mavapacha
Donge Chechele	Kangagani
Upenja Uwandani	Ole Markaz
Fuoni Kitongani	Gombani ya Kati
Kiwengwa Pongwe	Madungu Kosovo
Tunguu njia ya Kibele	Kinyasini Selemu
Mfenesini Selem	Mkungu Mahudhuthi
Mwera Gudini	Mbuzini
Mangapwani	Vitongoji Darajani
Kwarara Madina	Sizini msikiti wa Ijumaa
Mitondooni	Masjala Kiungoni
Paje Mji mpya	Quweit

Kilindi	Muhogoni Mahuduthi
Mgambo	Magogoni Ngwachani
Mahonda Bangalow	Makoongeni Mtambwe
Chuini asumini	Masota Msikitini
Myamanzi	Kigope Mtambile
Selemu	Kinazini Wingwi
	Jemele Kangani
	Chamanangwe kilimo
	Wingwi Dodeani
	Tumbi
	Matuleni
	Junguni kisima cha maji
	Ngomeni

Chanzo: ZECO,2017

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Ardhi, Ujenzi, Nishati na Mazingira kwa uwasilishaji wa hotuba yako na hoja imeungwa mkono.

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi nakushukuru sana kuweza kunipa nafasi hii kusimama katika hadhara hii mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kusoma Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe**.** Mwenyekiti, sote hatuna budi kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima tukaweza kukutana tena katika Mkutano huu wetu wa Sita wa Baraza hili la Wawakilishi kwa kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako ili kuweza kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano hapa mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe**.** Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, Mhe. Salama Aboud Talib, Naibu Waziri, Mheshimiwa Juma Makungu Juma, Katibu Mkuu ndugu Al-halil Mirza, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyatoa katika kipindi choto tulipokuwa kwenye shughuli zetu za kawaida za Kamati.

Mhe**.** Mwenyekiti, aidha, napenda kuipongeza tena Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa huu 2017/2018 kwa umahiri na ufanisi mkubwa wa hali ya juu kabisa katika mfumo mpya wa bajeti unaozingatia programu yaani "*PBB*".

Mhe**.** Mwenyekiti, sitakuwa nimewatendea haki ikiwa nitaendelea kutoa hotuba hii bila ya kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe na Katibu wa kamati yangu ambao tumeshirikiana kwa pamoja kuyapitia na kuyachambua makadirio haya ya Bajeti ya Wizara hii na hatimaye leo kunipa nafasi kuweza kuyawasilisha.

Mhe**.** Mwenyekiti, Kwa kuheshimu, kuthamini na kutambuwa mchango wao mkubwa kwenye Kamati hii hadi kufanikisha kazi hii iliyokusudiwa, naomba hivi sasa unipe ruhusa niweze kuwataja Wajumbe wa Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi. Kamati hii ilikuwa imeongozwa na Mheshimiwa:-

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Suleiman Sarahan Said	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Khadija Omar Kibano	Mjumbe
4.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
5.	Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohammedali	Mjumbe
6.	Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
7.	Mhe. Said Omar Said	Mjumbe
8.	Ndg. Fatma Omar Ali	Katibu

Mhe**.** Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Baraza la Wawakilishi liliidhinishiwa na Wizara ya Fedha Matumizi ya jumla ya Tshs. 9.555 bilioni kwa ajili ya Fungu N01 kwa Matumizi ya kazi za Kawaida. Aidha, Baraza pia liliidhinishia Wizara ya Fedha kutumia jumla ya bilioni 47.900 bilioni kwa ajili ya Matumizi ya kazi za Maendeleo. Vile vile, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya Tshs. 6.100 bilioni kama ni mapato yatokanayo na vyanzo mbali mbali kama alivyosema Mhe. Wizara.

Mhe**.** Mwenyekiti, katika hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 Wizara ya Fedha imepangiwa Tshs. 10.664 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tshs. 36.943 bilioni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, inakadiriwa kutumiaTshs. 47.608 bilioni kwa ajili ya kutekeleza adhma ya Fungu N01.

Aidha, katika utaratibu mpya wa bajeti inayozingatia programu ya '*PBB'*, Wizara hii imepangiwa kutekeleza Programu Kuu Nne (4) kama alivyoeleza Mhe. Waziri.

Mhe**.** Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kwa idhini yako Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze uchambuzi wa Programu hizo kama zilivyokwishakutangulia kuelezwa na Mhe. Waziri.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi

Mhe**.** Mwenyekiti, kama inavyofahamika kuwa jukumu kubwa la Programu hii ni kuimarisha shughuli za uratibu katika suala zima la utekelezaji wa kazi za wizara pamoja na kukuza ufanisi katika utawala wa rasilimali ardhi pamoja na utoaji wa huduma kwa jamii. Aidha, Programu hii inajumuisha Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Afisi Kuu Pemba ambapo jumla yabilioni. 2,040,551,000 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii. Vilevile, programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo zake tatu (3).

Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara

Mhe**.** Mwenyekiti, Kupitia Programu Ndogo hii, Kamati yangu inamuomba sana Mhe. Waziri kushauriana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Tume ya Kurekebisha Sheria kuweza kuharakikisha ufanyaji wa marekebisho ya baadhi ya Sheria mbali mbali za ardhi zinazohusiana na maswali mtambuka ya ardhi katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwani vimekuwa vikileta mtafaruku mkubwa juu ya ongezeko la migogoro ya ardhi hadi kufika mwezi Machi, 2017, zaidi ya kesi 473 zimepokelewa na kutolea maamuzi. Kesi 241 kwa upande wa Unguja kamati yangu inaamini wizara ikikaa na Tume ya Kurekebisha Sheria basi tutaweza kuja kupata sheria nzuri zinazozingatia muda wa sasa na mahitaji mapya na vile vile kufuta baadhi ya zile sheria za zamani ambazo zimesababisha migogoro mimhi ya hapa kwetu Zanzibar ambayo inahusiana na ardhi.

Mhe**.** Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo na changamoto kwa upande wa utoaji wa ardhi kupelekea kuongezeka kwa migogoro sugu na kamati itaendelea kuisisitiza Wizara kwa Bajeti hii tunayoipitisha ya 2017/2018 kuhakikisha kwamba wanaandaa sera mpya ya ardhi na hatimaye kuweza kuzifanyia marekebisho baadhi ya hizo sheria kama nilivyosema hapo mwanzo.

Mhe**.** Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu makuu ya Programu kuu hii ni

kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi kwa maendeleo ya pamoja kwa matumizi yaliyo bora na fanisi. Aidha, Programu hii kawaida hutekelezwa na taasisi mbali mbali kama vile Idara ya Usajili wa Ardhi, Idra ya Upimaji na Ramani, Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Hata hivyo, vile vile kuna na Mahakama ya Ardhi.

Mhe**.** Mwenyekiti, hivi sasa kumekuwa na miradi mingi mikubwa ya uwekezaji hasa katika Mji wa Fumba, pamoja na Mbweni. Kamati yangu haijaridhika na mfumo wa ujenzi unaoendelea hivi sasa wa nyumba za kisasa bila ya kuangalia ukubwa wa ardhi yetu ya Zanzibar ni ndogo na lakini kitu ambacho wawekezaji wa ujenzi wa miradi hiyo wameanza kujenga majengo madogo wenye ukubwa wa ghorofa moja na na mengine ghorofa mbili. Kamati yangu ingepenedelea kuona ujenzi wa ghorofa kuanzia ghorofa saba na kuendelea ili kuweza kulinda ardhi ndogo tuliyokuwa nayo.

Kamati yangu imaishauri kuwa ile miradi ya Fumba basi iwekewe utaratibu maalum wa ujenzi kuanzia ghorofa saba na kuendelea ili kuweza kubadilisha mandhari ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Lakini vile vile kuweza kubana matumizi kwa ardhi yetu ndogo tuliyokuwa nayo.

Programu ndogo ya Utawala wa Ardhi

Mhe**.** Mwenyekiti, naomba nieleze wazi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kuwa moja kati ya Programu muhimu katika Wizara hii ni programu ndogo hii ya Utawala wa Ardhi programu hii ambayo kwa mfumo wa hivi sasa moja kwa moja husimamiwa na Kamisheni ya Ardhi kwa kushirikiana na baadhi ya Idara kama nilivyozielezea hapo juu. Hata hivyo, kamati yangu hairidhishwi na utendaji kazi wa Kamisheni hii ya Ardhi hususan katika masuala mazima yanayohusiana na uombaji wa ardhi, utoaji wa ardhi, upimaji pamoja na usimamiaji wa ardhi, kwani changamoto sungu iliyosababisha migogoro ya ardhi huko nyuma na mpaka sasa hivi migogoro hiyo inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nitatoa mifano michache kati ya mingi ambayo imekuwa ni donda ndugu lisilopoa, ambapo Baraza lako tukufu litatakiwa kufanya maamuzi magumu ili wananchi waweze kupata haki zao na katika maeneo yao yaliyochukuliwa kwa nguvu na baadhi ya viongozi bila ya ridhaa yao. Naamini ripoti ya kamati yangu itachambua tu baadhi ya kadhia hizo lakini kamati itazitaja kwenye ripoti hii. Lakini tunaamini wajumbe wenzetu waliokuwemo humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, wao wanayajua mengi zaidi kuliko inavyoyajua kamati, mengi ya kadhia hii na

wao katika migogoro hii ya ardhi ambayo imo katika maeneo mbali mbali katika majimbo yao, nao wataweza kuzitaja kero nyengine kama hivi tunavyoanza sisi kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kadhia hiyo, kamati yangu ilihitaji kuomba maelezo ya kina wakati wa kupitia bajeti kwa upande wa wizara iliomba kupatiwa maelezo ya kina wakati wa kupitia bajeti ya wizara hii ili kuweza kujua ni kitu gani kinachopelekea utendaji au na sheria zikakiukwa na taratibu zilizowekwa na sheria husika. Mfano wa baadhi ya kadhia hizo ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Uwekezaji wa "*Spice Islander"* uliopo katika eneo la Nungwi lenye hekari 7.8 ambapo muwekezaji huyo alipewa '*lease'* halali na Serikali ya Mapinduzi ya Zanizbar, eneo hilo baadaye kufutwa bila ya taarifa na kinyume cha utaratibu wa Sheria na hatimaye kugaiwa ardhi hiyo kwa watu wengine wanne tofauti kinyume cha Sheria ambapo kitu cha kushangaza ardhi hiyo aliyonyang'anywa muwekezaji huyo wakapewa watu ambao hawana hata miradi wa kufanya, matokeo yake maeneo hayo wakawa wanatafuta wateja ili kuweza kuyauza na kujipatia pesa kinyume cha Sheria, ambapo jambo hilo ni utapeli na pia ni utakatifu wa fedha haramu (yaani '*Money Loundry'*) jambo ambalo ni uvunjifu wa Sheria za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kadhia hiyo, tunamshukuru sana Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi baada ya kugundua dhulma hiyo imefanyika, akamuagiza Mhe. Waziri wakati huo aliyehusika na wizara hii kwa wakati huo, eneo hilo arejeshewe muwekezaji wa '*Spice Islander',* lakini cha kushangaza eneo hilo halijarejeshwa kwa mwenyewe hadi leo hii tumepata taarifa eti watendaji wa wizara wanakusudia kumrejeshea eneo hilo mwekezaji huyo robo tatu, robo moja hawataki kumrejeshea eti kwa sababu amepewa mtu mmoja mkubwa sana. Suala hili ndio kamati yangu inajiuliza hawa watendaji wetu wanafuata maelekezo ya nani, ikiwa kama Makamu wa Pili wa Rais ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanizbar. Kamati yangu inamtaka Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira aliyekuwepo hivi sasa, alitekeleze agizo lile halali la Mhe. Makamu wa Pili Rais, ili kumrejeshea muwekezaji yule wa *Spice Islander* ili kulinda heshima ya serikali, na huyo 'mtu mkubwa' kama yupo basi aweze kutafutiwa eneo jingine kama iko haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambapo kamati yangu haikuridhika ni kitendo alichofanyiwa muwekezaji kutoka Kampuni ya '*Pakachi Beach Resort'* ambapo alipewa '*invoice'* na Idara hii ili afanye malipo ya kupatiwa

‘*lease’* lakini kitu cha kushagaza baada ya mwekezaji huyo kulipa ‘*lease’* hiyo, imetolewa kwa jina la mtu mwengine, ambaye ni ndugu Mohamed Othman Abdalla ambapo kamati yangu inahisi huo ni utapeli aliofanyiwa muwekezaji huyo wa kigeni, kwani alifuata utaratibu wa kuweza kufanya maombi na akapatiwa *bill* na akaweza kulipa, lakini lease hiyo akapewa mtu mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu iliwaita wahusika katika kadhia hiyo, akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Diwani, Sheha, Mwenyekiti wa Halmashauri, pamoja na huyo mmiliki alieuza eneo hilo mbele ya waziri pamoja na watendaji wa Kamisheni ya Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, kitu cha kushangaza katika kikao hicho tulikubaliana na Mhe. Waziri alitoa agizo kwamba hati ile ifanyiwe marekebisho ili aweze kutoa *lease* nyengine. Lakini hadi tunafika kusoma ripoti hii na Mhe. Waziri amefika kusoma bajeti hii ‘*lease’* ile bado haijafutwa na haijarejeshwa kwa yule aliyehusika. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa *lease* ile ilitoka *Invoice* kwa yule ambaye aliyelipa *bill* tunaomba serikali kwa kupitia Mhe. Waziri *lease* ile ipatiwe mtu yule ambaye aliyeomba na aliyepewa *bill* na akalipa serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia haikuridhika na tabia ya kamisheni hii ya kuwanyima kuwapatia ‘*lease’* baadhi ya wawekezaji hasa wazalendo bila ya kuwa na sababu madhubuti na kupelekea kuwarejesha nyuma katika kushiriki kwao katika uwekezaji. Mmoja wa mfano huo ni uwekezaji mkubwa uliopo huko Mangapwani ambapo muwekezaji huyo ndugu Khamis Kipara ambaye anamiliki Kampuni ya *Ocean Petroleum*, amekusudia kujenga chelezo cha kutengenezea meli huko Mangapwani, lakini kitu cha kushangaza hadi leo kamisheni hawajampatia *lease*, ambapo majirani zake karibu wote waliokuwepo pale ambao wamemkuta tayari wameshapatiwa ‘*lease’*. Huu ni ubaguzi usio na sababu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inamshauri Mhe. Waziri kumpatia ‘*lease’* muwekezaji huyo mzalendo, kwani kamati yangu ilipotembelea Mombasa (Kenya) iliukuta mradi wa aina kama hiyo ambapo umetoa ajira nyingi kwa vijana na pia utaiongezea mapago serikali ya fedha za kigeni, kwani kwa kawaida malipo kwa vyombo vya baharini hulipiwa kwa fedha za kigeni, na hapo utakapoanza kazi utaweza kuisaidia sana kuongeza mapato ya serikali hasa fedha za kigeni, kwani hivi sasa wanakuja wabia mbali mbali ili washirikiane naye katika kuendeleza mradi huu, lakini anashindwa kwa sababu hajaweza kupata hiyo ‘*lease’.*

Mhe. Mwenyekiti, suala hili hapa Barazani sio jipya, kwani kamati iliyopita

iliwahi kulisemea suala hili na hadi sasa hatuelewi ni kitu gani kilichosababisha mradi huu umekwama mpaka hivi sasa, wakati tayari umeshafanyiwa *EIA* na kuonekana kwamba hakuna tatizo la kufanyika mradi huo katika eneo hilo. Hapa Waziri aje atuambie sababu za msingi vinginevyo ampatie '*lease'* mwekezaji huyo, ili aweze kuendeleza mradi wake huo, tena kukazi hoja yetu kwa mradi huo kwa hapa Zanzibar au hapa Unguja, hauwezi kufanyika katika eneo jengine lolote, isipokuwa katika eneo hilo kwani eneo hilo ndio pekee lenye kina kirefu kikubwa cha maji ambapo meli ya aina yoyote inaweza kuelea kukaa eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kadhia nyingine ambayo kamati yangu haijaridhika na vitendo vilivyofanywa na aliyekuwa waziri wa wizara hii kuwanyang'anya watu wa Nungwi eneo lao na kumpatia mwananchi mwengine wa familia yake bila ya ridhaa ya wananchi hao. Vile vile wananchi hao wamefika kulalamika katika ngazi zote serikalini hadi kufikia kwetu Baraza la Wawakilishi, ili kuweza kuwasimamia katika kupata haki yao hiyo. Hivi sasa suala hilo tumepata taarifa limeshafikishwa mpaka kwa Katibu Mkuu Kiongozi, lakini bado halijaweza kupatiwa ufumbuzi. Kamati yangu inamtaka Mhe. Waziri kufuatilia suala hili kwa karibu na hatimaye hiyo hati iliyotolewa kimakosa kwa mwananchi wa familia ya waziri aliyepita kinyume cha taratibu, hati hiyo warejeshewe wananchi ili waweze kulitumia eneo hilo kwa shughuli zao walizokusudia.

Mhe. Mwenyekiti, tabia hii iliyokuwepo hapo nyuma kwa viongozi kuwadhulumu wananchi haki zao kwa matumizi ya ardhi na kupewa watu fulani kwa manufaa yao binafsi, wakati tunapopewa dhamana hizi na wananchi ili kuwaongoza wananchi ni jambo baya sana, jambo ambalo hupelekea wananchi kukosa imani na serikali yao kwa vitendo vya watu wachache kwa maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imeona ni dhahiri kuwa kuna uporaji wa ardhi ya wananchi hao na Mhe. Waziri kuweza kumpatia mtu mwengine wa familia yake kinyume cha sheria inayosimamia maadili ya viongozi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, hali kadhalika kwa upande wa Pemba, kuna eneo la Wingwi (Micheweni) nako pia wananchi wamenyan'ganywa eneo lao walikokuwa wakilima kilimo cha ushirika na kupewa tena mtu binafsi ambaye ni mtu wa karibu na aliyekuwa karibu na Mhe. Waziri wakati huo kinyume cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa kutumia madaraka aliyopewa kwa kujinufaisha yeye mwenyewe au familia yake. Mhe.

Mwenyekiti, ardhi hiyo tangu siku hiyo ambapo wananchi walikuwa wakilima mpaka leo haitumiki kwa shughuli yoyote, kwa sababu hata huyo aliyepewa na yeye hana shughuli nyengine yoyote ya kufanya, kwa hivyo ardhi imekaa bure.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika eneo la Muyuni Matemwe kuna mwananchi wa kijiji hicho maarufu ndugu Choroko, nae pia wizara ilimtaka eneo lake ampatie mwekezaji kwa makubaliano kwamba mwekezaji huyo angemlipa fidia mwananchi huyo Tshs. 120 milioni, ili aweze kuliacha kulitumia eneo hilo na amruhusu mwekezaji mwengine ndugu Yakub. Lakini jambo la kushangaza kabla ya kulipwa fidia hiyo mwananchi huyo, waziri aliyekuwepo kwa wakati huo aliweza kumpatia '*lease'* mwekezaji huyo bila kumlipa fidia ndugu Choroko haki yake ambayo kwa makubaliano ambayo yalisimamiwa na wizara kwa wakati huo, lakini hadi leo tunawasilisha ripoti yetu hii mwananchi huyo hajalipwa hata senti moja.

Lakini cha kushangaza zaidi Mhe. Mwenyekiti, mwananchi huyo aliitwa wizarani na watendaji wa ardhi na akapewa shilingi milioni 12 eti mwekezaji anamtafutia pesa zake, zikiwa tayari atakuja kummalizia. Lakini hadi leo kitu ambacho cha kushangaza, hadi leo Mhe. Mwenyekiti, wananchi huyo hajaweza kulipa pesa zake. Kwa hivyo, kitu cha kushangaza leo inakuwaje mwekezaji aliyepewa eneo ni mtu mwengine, lakini watendaji wa serikali ndio wanakwenda kumuita mwananchi yule na kumpa hizo pesa milioni 12, jambo ambalo ni kinyume cha taratibu za kisheria. Eneo lile alilopewa huyo ndugu Yakob mpaka leo ameshindwa kuliendeleza na kwa sababu na yeye sio mwekezaji, isipokuwa anatafuta mteja na yeye aweze kuliuza eneo hilo. Kamati yangu Mhe. Mwenyekiti, inamshauri Mhe. Waziri eneo hilo kumrejeshea mwananchi huyo ili aweze kuliendeleza kwa shughuli zake.

Mhe. Mwenyekiti, pia, Kamati yangu imepata malalamiko ya mradi wa "*Wave Resort*" ambao uliokuwepo huko Bwejuu. Mhe. Mwenyekiti, hata waziri umeshamfikia mgogoro huu katika meza yake. Lakini hadi leo ameweza kuwasilisha ripoti yake hapa Barazani, kamati yangu bado Mhe. Waziri suala hili hajalifanyia kazi na bado yuko mbioni kuweza kulifanyia kazi. Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Waziri eneo hili aweze kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, najaribu kwenda kwa ufupisho kwa sababu hotuba yangu ni refu. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kuokoa muda naomba nimalizie jambo moja ambalo ni ukiukwaji mkubwa wa sheria za nchi pamoja na Maadili ya Viongozi wa Umma. Kamati yangu imegundua kuwa waziri

aliyepita aliwagaia maeneo mengi watu wa karibu yake na maeneo hayo yalikuwa yakimilikiwa na wananchi wengine na maeneo hayo serikali haifaidiki chochote, isipokuwa yamekaa bure na kuikosesha serikali mapato makubwa ambayo yangeliweza kuongeza mapato kwa serikali. Kwa kuwa maeneo hayo ni mengi nadhani itachukua muda mrefu sana kuyataja lakini tutayaambatanisha maeneo hayo kwenye hii ripoti yetu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo, pia kamati yangu imegundua serikali inakosa mapato mengi kwa watu ambao wamepewa "*lease*" kwa muda mrefu, lakini wameshindwa kuyaendeleza maeneo hayo na kuikosesha serikali mapato, ambayo ndio nguzo ya uchumi wa nchi zote duniani, na pia miongoni mwao wako ambao hata hizo "*lease*" zenyewe hawazilipii kodi kama sheria serikali inavyosema.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kadhia hiyo tunamuomba sana Mhe. Waziri aweze kuchukua hatua za haraka, lakini kwa inavyoonekana migogoro hiyo kwa kuwa imekaa muda mrefu, nadhani Baraza lako iko haja ya kuweza kuchukua hatua za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa huduma zilizopangwa kutekelezwa kupitia programu hii ni huduma ya kusimamia matumizi bora ya nishati iliyo salama na rafiki kwa mazingira, kusimamia tafiti na kuendeleza matumizi ya nishati mbadala, kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii, kusimamia na kuanzisha mpango wa utafititi wa uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, uimarishaji wa miundombinu wa maji mijini na vijijini, umarishaji na kuijengea uwezo *ZAWA* kujiendesha kibiashara, usambazaji wa umeme vijijini, uimarishaji na uendelezaji wa miundombinu ya umeme, kuanzisha na kusimamia miongozo ya kitaalamu kwa maendeleo ya mafuta na gesi asilia, pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za mafuta na gesi.

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyofahamika hii ni miongoni mwa Programu muhimu kwa manufaa na maendeleo ya nchi yetu programu ambayo inaingiza mapato makubwa kwa serikali yetu, ila bado utekelezaji wake unasuasua kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Shein, kwa kutuletea Sheria ya kuweza kusimamia masuala ya Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar, na hivi sasa serikali imeshaanza kuunda vyombo na mamlaka ambazo zinatakiwa kuanza shughuli zake na kutengeneza sheria, pamoja na kanuni za kuwavutia wawekezaji katika sekta hii mpya ya Mafuta na Gesi Asilia. Kamati yangu

inaitaka serikali kuweza kuzipatia pesa za kutosha taasisi hizo ambazo zimeundwa, kwani kazi zao ni za kitaalamu zinahitaji vitendea kazi vya kisasa, wataalam waliopo hawatoshi. Pia wanatakiwa wawe wazoefu katika masuala mbali mbali yanayohusu mafuta na Gesi Asilia, kwani kwa mafungu tuliyoyatenga katika bajeti ya mwaka huu, kwa kweli hatujawatendea haki, kwani taasisi zinapokuwa mpya zinahitaji nyenzo za kutosha ili kuweza kujiandaa na utekelezaji wa majukumu yao waliopangiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili la nishati ya mafuta na Gesi Asilia, serikali inatakiwa kuwekeza zaidi katika kuwasomesha vijana wetu wenye umri mdogo waliotoka vyuoni, ili wawe na muda mrefu wa kuja kufanya kazi katika sekta hii, na kupunguza kutegemea wataalamu kutoka nchi za nje ambao watakuja kuigharimu serikali pesa nyingi. Sasa kwa kuwa hivi sasa kuna vijana wengi zaidi ya sitini ambao tayari wameshamaliza masomo yao katika fani hii ya mafuta na Gesi Asilia, basi tunaiomba serikali kuweza kuwaajiri vijana wetu hawa, ili kuanza kupata uzoefu, lakini pia kuwatafutia mafunzo nje ya nchi ili kuja kulitumikia taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili labda Mhe. Waziri akija aje atueleze, hadi hivi sasa kuna shughuli gani ambayo imeshaanza katika masuala mazima ya utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia, na vipi uitikiaji wa wawekezaji katika utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, lakini pia je kuna kampuni gani yoyote ambayo serikali imeshampa kibali cha uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa visiwani kwetu?

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia Mhe. Waziri aje kutueleza kuhusu utafiti uliokwisha kufanywa na ile ndege iliyokuja kufanya utafiti wa mafuta. Je, ripoti yake imeshakabidhiwa serikalini, na je, imeonyesha kwamba hapa Zanzibar Mafuta na Gesi Asilia yapo ya kutosha au ndio hivyo tena hapa, kwani wananchi wetu wana hamu kubwa ya kusikia kuwa Zanzibar yamegundulikana Mafuta na Gesi Asilia, ili kuweza kuondokana na umaskini. Pia Mhe. Waziri aje kutuambia mamlaka imejiandaa vipi kuhusu utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya Mafuta na Gesi Asilia na changamoto zake, ili na wao washiriki kikamilifu katika kunufaika na rasilimali zao hizo, lakini zaidi katika uhifadhi wa mazingira katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza sana *ZURA* kwa utendaji wao wa kazi zaidi katika kusimamia ubora wa huduma za maji na mafuta hapa Zanzibar. Kwani kwa kipindi kirefu tangu kuanzishwa kwa taasisi hii ya *ZURA*, hatujasikia kuadimika kwa mafuta wala kusikia kuna mafuta machafu ambapo vyombo vya moto huwa vinaharibika mara kwa mara. Wakati huko nyuma

ilikuwa ni jambo la kawaida kusikia maharibiko ya vyombo vya moto au kuadimika kwa mafuta. Lakini kamati yangu inaishauri sana *ZURA* bado kuna tatizo la matumizi ya mashine za kupimia mafuta kwenye sheli zetu au kwenye vituo vyetu vya petroli, kwani inaonekana kuna baadhi ya vituo vipimo vyao sio vizuri na huwa vinawadhulumu wananchi wanaotumia mafuta. Kwa hivyo tunaiomba *ZURA*, kuwaiga wenzao wa "*EWURA*" kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika vituo vya mafuta, hasa vya mashamba, kwani inaonekana mchezo mchafu unafanyika, ili kuondoa kuwabinya wateja na watumiaji wa mafuta kupitia katika vyombo vya moto.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza *ZURA* kwa mpango waliokuja nao wa kuliendeleza eneo la Mangapwani, kwa nia ya kujenga Bandari ambayo itakayotumika kwa ajili ya kupakia na kupakulia mafuta kutoka kwenye Meli. Mradi ambao tunategemea utaweza kuleta tija sana serikalini. Kwa hivyo, kamati inawatia moyo sana na wala msirudi nyuma katika mradi wenu huu. Hivyo, Mhe. Waziri akija basi aje atuambie mradi huu umefikia hatua gani. Lakini pia tunaipongeza *ZURA* kwa kuja na wazo la kujenga jengo lao jipya la taasisi yao, ambalo litaweza kusaidia sana kuondoa tatizo la ufinyu wa nafasi katika taasisi mbali mbali zilizokuwemo katika wizara yao ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika eneo hili la huo ujenzi unaotarajiwa aje atueleze wamefikia hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Mjini kutoka kwa wafadhili wetu hasa huu mradi kutoka India unatekelezwa kwa wakati uliowekwa ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wetu. Pamoja na hayo, Kamati yangu inaitaka Mamlaka hii katika bajeti hii kuweka utaratibu maalum wa kuvipa kipaumbele visima vyote ambavyo vilichimbwa kupitia mradi wa Ras Al khaimah viweze kufanya kazi iliyokusudiwa kwani visima hivyo vikiungwa umeme na kuekewa miundombinu ya mabomba basi tunaamini maeneo mengi ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba vitapata maji ya kutosha na kupunguza tatizo la maji kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tuwe wawazi kwani tatizo la maji bado ni kubwa hasa katika Mji wetu wa Zanzibar hususan katika Mkoa wa Mjini Magharibi na tukizingatia bado makaazi ya watu yanaongezeka siku hadi siku katika Mkoa wetu huu. Hivyo basi, ni vyema kwa Mamlaka ya Maji kwa kushirikiana na Serikali za mitaa kuhakikisha vianzio vya maji vinalindwa kwani Kamati yangu ilipotembelea baadhi ya vianzio hivyo iligundua kuwa

baadhi yake vimeshavamiwa na makaazi ya watu jambo ambalo linapelekea kina cha maji kupungua kila siku na kusababisha upungufu wa maji kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia imegundua kuwa msitu wa Masingini pamoja na ule wa Mwanyanya kwa taarifa za wataalamu ndio msitu unaohifadhi kiasi kikubwa cha maji ardhini na ndicho kinachosaidia kupatikana kwa maji katika vivima vyatu. Kwa taarifa msitu huo umeanza kuvamiwa kwa ujenzi wa nyumba na makaazi, jambo ambalo linaweza kusababisha uhaba wa maji ardhini. Hivyo, Kamati yangu inaitaka *ZAWA* kwa kushirikiana na Halmashauri husika kuzuia ujenzi wa aina yoyote karibu na msitu hiyo ili kuweza kuzuia kupatikana kwa tatizo la maji hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Kamati yangu inaitaka *ZAWA* kuweza kununua *Pump* za maji zenye viwango bora ili kuepusha kuharibika mara kwa mara kwa pump kwani wananchi wetu wanasumbuka sana kutokana kuungua kwa *pump* hizo. Kamati yangu pia inaitaka *ZAWA* kuharakisha mradi wa ubadilishaji mabomba ya kupitishia maji kwani mengi yaliopo yameshakuwa machakavu ikiwemo kuziba kwa *calcium* ndani ya mabomba na kusababisha kupasuka na kuzuia kasi ya upitikanaji wa maji kwenda kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya maji kujitahidi kutumia vizuri pesa za wafadhili, kwani pesa nyingi sana za wahisani zimeingia kwenye miradi ya maji lakini bado tatizo la maji inaonekana bado kutatuka, watu wengi hawapati maji majumbani mwao na hata hao wanaopata hupata kwa mgao tena usio na ratiba ya uhakika na unaweza kukaa wiki nzima maji hayajatoka katika majumba yetu, hiyo imekuwa ni shida kubwa kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka upande huo naomba sasa niingia katika Shirika la Umeme Zanzibar ambalo ndio tegemeo kubwa kwa wananchi wetu na Serikali kwa ajili ya kutoa huduma za usambazaji wa umeme mjini na vijijini. Aidha, licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana, bado Shirika hilo linaendeshwa hasara hali ambayo inaisababishia Serikali kukosa kufikia makusanyo yaliyojiwekea. Vile vile, Kamati inaendelea kuishauri Wizara kukaa pamoja na Shirika la Umeme na Idara ya Nishati kutafuta mbinu mbadala ya kuweza kuzalisha umeme wa jua, upepo pamoja na mawimbi ya bahari jambo ambalo litaisaidia Serikali kuwa na chanzo chengine cha umeme kuliko ilivyo hivi sasa ambapo tunategemea chanzo kimoja tu. Ambapo Shirika limekuwa likibambikiziwa gharama nyingine ambazo wala hazina msingi na kulibebesha

Shirika madeni yasiyolipika.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo, Kamati yangu pia inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza tena Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa busara zao na hekima zakuanza kulipa deni la Zanzibar kwenda *TANESCO* Tshs. 11.8 bilioni kati Tshs. 61.8 ya deni halisi. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hii iliyoanza kuchukuliwa ya kulipa deni hilo. Pamoja na pongezi hizo kwa Serikali, Kamati yangu inaitaka Wizara ya Fedha ili kuiokoa *ZECO* na kubeba mzigo mkubwa wa madeni basi ni vyema kwa upande wa taasisi za Serikali, Wizara ya Fedha ikaweza kulipa moja kwa moja *ZECO* vile vifungu vya huduma za umeme kwa zile taasisi ambazo hazijaungiwa mita za tukuza ili kulipa nguvu Shirika kuweza kutoa huduma bora kwa wakati na pia kuweza kulipa madeni ya *TANESCO*.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inaipongeza *ZECO* kwa kuweka mkakati wa kulipa *'current Bill'* na pia malipo ya ziada kwa *TANESCO* ili kuweza kulimaliza deni hilo kwa muda waliojipangia. Kwa hiyo na sisi wananchi tuisaidie *ZECO* kwa kulipa bili zetu kwa wakati ili kuliwezesha Shirika kulipa madeni yake kwa wakati. Pia bila ya kusahau, Kamati yangu inapenda kumpongeza Mhe. Professor Muhongo, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini kwa jinsi akivyoweza kushirikiana na Mhe. Waziri wa Maji, Nishati wa Zanzibar Mhe. Salama Aboud katika kulisimamia suala la deni halisi iliyokuwa inadaiwa *ZECO* kutoka *TANESCO* na lengo hilo Mhe. Waziri tunashukuru limeweza kufanikiwa. Kwa hiyo tunamtakia kila la kheri Mhe. Professor Muhongo, lakini vile vile tunampa pole kwa uwajibikaji ambao aliwajibika kisiasa na hayo ndio majukumu yetu sisi kama wanasiasa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pamoja na pongezi kwa *ZECO* lakini pia inautaka uongozi…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti, una dakika kumi katika kuwasilisha kwako.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano) Haina tatizo Mheshimiwa. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo kwa *ZECO*, lakini pia inautaka uongozi wa *ZECO*, *Management* pamoja na Bodi kuangalia kwa karibu utendaji wa Shirika hasa katika kufuatilia masuala ya *Tender* na manunuzi ya Shirika kwani inaonekana matumizi yanazidi kuwa makubwa ambapo kwa upande mwengine kuna mkakati wa kulipa Deni la *TANESCO*. Pamoja na hayo,

pongezi zetu kwa *ZECO* kwa kuweza kusambaza umeme karibu asilimia 80 katika vijiji vya Unguja na Pemba.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni kuu la Programu hii ni kuhakikisha usimamizi ulio bora na imara juu ya mambo yote yanayohusiana na mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuweka usimamizi endelevu wa masuala hayo. Ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2106/2017, programu hii imetengewa Tshs. 1,598,298,000 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya fedha hizo kutengwa kwa Mamlaka hiyo pamoja na Idara yake, bado changamoto zinaendelea kuwepo na wala hazipungui. Miongoni mwa Changamoto hizo ni wakurungezi wawili kutumia ofisi moja, jambo ambalo limewakosesha faragha ya utendaji kwa wakuu hao jambo ambalo Kamati yangu hailipendelei hata kidogo. Kwani limekuwa ni suala la muda mrefu lakini Wizara inashindwa kulichukulia hatua kwa kulitafutia ufumbuzi. Kamati yangu inaishauri Wizara kuchukua hatua za haraka ili kuwatenganisha wakurugenzi hao kila mmoja awe na ofisi yake aweze kufanya kazi yake kwa utulivu.

Changamoto nyingine ni uchimbaji wa mchanga kiholela kwa baadhi ya maeneo mbali mbali hasa Kinuni na kusababisha mashimo ambayo ni hatari kwa wakaazi wa maeneo hayo wakati wa mvua, pia utupaji wataka ovyo katika maeneo ya mjini na vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na Changamoto hizo Kamati yangu inamuomba Mhe. Waziri kuweza kuwatafutia jengo jengine litakalokuwa na nafasi kubwa ya kuhimili idadi kubwa ya watendaji. Aidha, Kamati haitosita kuishauri Mamlaka kwa kushirikiana na Idara kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi, kwani miongoni mwa changamoto kubwa Duniani kwa hivi sasa ni suala la mabadiliko ya tabianchi ambapo katika Mkutano uliofanyika nchini Mexico mwezi uliopita moja katika moto uliyotoka pale ni jamii kushirikishwa jamii ikiwemo watu binafsi na taasisi binafsi kuweza kushiriki kikamilifu katika kusimamia mazingira na kupunguza athari za maafa pale yatakapotokea.

Mhe. Mwenyekiti, pia Kamati yangu imefanya utafiti mdogo katika maeneo mengi ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kwenye maeneo ya fukwe za bahari zinaendelea kula nchi miaka kila ikienda kwa kiasi kikubwa

yamechangiwa na ujenzi usiofuata Sheria za mazingira hasa katika pembezoni mwa fukwe za bahari, ambapo miradi inatakiwa ijengwe katika fukwe za kawaida si chini ya mita 30, lakini katika maeneo ya fukwe ijengwe si chini ya mita 10. Lakini katika eneo hili wawekezaji wengi wameshindwa kufuata Sheria ya ujenzi katika maeneo ya fukwe ambapo wamekuwa wakijenga nje ya mita hizo zilizotajwa na kufuata utaratibu. Matokeo yake matokeo yake inasababisha bahari kupanda juu kila siku zikienda na kuvamia mashamba ya watu na kuwakosesha wananchi kulima mashamba yao.

Mhe. Mwenyekiti, kadhia nyengine ya uharibifu wa mazingira ni kuwa kumeanza kujitokeza tatizo kwa wananchi wa Jimbo la Mtoni hivi sasa zaidi ya nyumba 80 zimekuwa zikiingia maji bahari kutokana na mradi mkubwa unaoendelea hapo katika Mtoni Marinena kusababisha nyumba hizo sasa kuvamiwa na maji ya bahari.

Mhe. Mwenyekiti, Jambo hili ni kubwa na limeleta taharuki kubwa kwa wananchi wanaoishi katika nyumba hizo. Kwa hivyo, Kamati yangu inamtaka Mhe. Waziri wa Ardhi, Mhe. Waziri wa Utalii, Mhe. Waziri wa Mawasiliano pamoja na Wizara ya Fedha kuiundia Tume maalum na kuleta taarifa hapa Barazani kuona na kuona ni kiwango gani cha athari ya mazingira na hatua gani za haraka zitachukuliwa kwa athari ile iliyojitokeza na ni hatua gani za haraka zitaweza kuchukuliwa ili kuweza kuwaokoa wananchi wale wasije kuzama ndani ya bahari na nyumba zao.

Mhe. Mwenyekiti, pia kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuja na mipango mipya ya kupanga miji yetu ili iwe ya kisasa na yenye ubora ingawa kumekuwa na baadhi ya changamoto hasa katika kuhamisha makazi ya watu, ikiwemo wafanya biashara inaonekana ushirikishwaji unakuwa mdogo na kuleta malalamiko makubwa kwa wananchi wetu pamoja na kuwa hawapingani na kile kinachotakwa kufanywa na Serikali. Lakini pia kamati yangu inaitaka Serikali kuwa kitu kimoja hasa katika matumizi ya mipango ya kuendeleza maeneo yaliyogusa hifadhi ya Mji Mkongwe, kwani kuna baadhi ya Wizara hufanya maamuzi ya matumizi katika maeneo ya Mji Mkongwe bila ya kushirikisha mamlaka za Mji Mkongwe na suala hili linachelewesha miradi hiyo, wakati mwengine kuwavunja moyo wawekezaji na pia kuwatia hasara katika kucherewesha kufanya miradi yao.

Kwa mfano mradi wa Hoteli ya Bwawani, Jumba la Treni, pamoja na mradi wa Darajani Coridoo. Kamati yangu inaishauri Serikali katika kupanga matumizi bora ya ardhi basi ni vyema Serikali kushirikiana na Shirika la

Nyumba la Zanzibar kuhakikisha na wa wao wanatafuta wafanya biashara au fedha kwa kuana kujenga majengo ya kisasa katika maeneo yetu ya Ng'ambo na kuwauzia wananchi au kuwakodisha wananchi ili tuweze kuwa na makazi bora yanayoendana na karne hii ya Sayansi na Technolojia, ambapo yapo mashirika na taasisi za kifedha nyingi ambao wako tayari kushirikiana na taasisi hizo.

Serikali kwa kuanza kufanya uteuzi wa baadhi ya wasimamizi wa Mamlaka za kusimamia masuala ya Mafuta na Gesi hapa Zanzibar, lakini kasi ya ukamilisha wa vyombo hivyo ni ndogo kwani bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwa jamii na Taifa kwa jumla. Lakini pia inaonekana bado Serikali haijalipa umuhimu mkubwa suala hilo kwani mafungu ya fedha waliyotengewa ni madogo hasa ukizingatia taasisi hizo ni mpya kwa hiyo zinahitaji miundombinu ya kisasa ili kuweza kufanya shughuli zake kwa ufanisi mkubwa, kuanzia wataalamu, vifaa vya kisasa pamoja na usafiri wa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuja na mipango mipya ya kuipanga miji yetu ili iwe ya kisasa na yenye huduma bora, ingawa kumekua na baadhi ya changamoto hasa katika kuhamisha makaazi ya watu ikiwemo wafanya biashara inaonekana ushirikishwaji unakuwa mdogo na kuleta malalamiko makubwa kwa wananchi wetu pamoja ya kuwa hawapingani kile kinachotaka kufanywa na Serikali. Lakini pia Kamati yangu inaitaka Serikali kuwa kitu kimoja hasa katika matumizi na mipango ya kuendeleza maeneo yanayogusa hifadhi ya Mji Mkongwe kwani kuna baadhi ya Wizara hufanya maamuzi ya matumizi ya Mji Mkongwe bila ya kuwashirikisha Mamlaka, jambo ambalo linachelewesha miradi hiyo na wakati mwengine kupelekea kuwavunja moyo wawekezaji na pia kuwatia hasara kwa kucheleweshwa kufanya miradi yao mfano Hoteli ya Bwawani, Jumba la Treni Darajani na mradi wa ujenzi Darajani Corridor.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inaishauri Serikali katika kupanga matumizi bora ya ardhi basi ni vyema Serikali kushirikiana na Shirika la Nyumba la Zanzibar kuharakisha mpango wao wa kutafuta wafanyabiashara au fedha na kuanza kujenga majengo ya kisasa katika maeneo yetu ya nga'mbo na kuwauzia au kuwakodisha wananchi ili tuweze kuwa na makaazi bora yanayoendana na karne hii ya sayansi na technologia, ambapo yapo mashirika na taasisi za kifedha ambayo yapo tayari kushirikiana kuifanya kazi hiyo. Kwa hivyo ni vyema kuwepo mashauri ya pamoja na ya karibu baina ya Idara ya Mipango Miji na Shirika la Nyumba la Zanzibar ili

kufanikisha mpango huo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa Bajeti basi wale Wazee wa Mahakama ya Ardhi waweze kuwalipa mafao yao yote ili kuwapunguzia makali ya maisha hasa ukizingatia kuwa wanalitumikia Taifa letu kwa muda mrefu lakini pia kazi wanayoifanyia ni kubwa. Pamoja na hayo, tunaipongeza Wizara hii kupitia Katibu Mkuu baada ya kuona wazee wetu hawa wanasumbuka katika kuwalipwa mafao yao kwa kuwaekea fungu maalum kwa mwaka huu wa bajeti ya 2017/2018 ambapo mwanzo hazikuwemo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu ya Ardhi na Mawasiliano imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Lakini Kamati hii imeyapitisha Mapendekeo haya kwa masharti maalum Mhe. Mwenyekiti katika lile eneo la migogoro ya ardhi kamati yangu imeripoti kwamba kitumike kifungu cha 111 ili kuweza kuundwa Kamati teule ya kwenda kuchnguza migogoro ile ya ardhi pamoja na mengine ambayo nilisema Waheshimiwa wananchi wataitaja ili kuweza kujiridhisha. Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri atakubali kuniridhia na hilo basi mimi na wajumbe wangu tutaishawishi bajet hii tuipitishe kwa masharti yale Kamati ambayo iliyioishauri. Baada ya hayo machache mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo lakini nitaomba tu Mheshimiwa unipe dakika tatu ili niweze kuzungumzia kadhia ya jimbo langu husika.

Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu la Shaurimoyo kuna shule kubwa ya Sekondari ya Kwamtipura ambayo Wizara ya Elimu iliweza kuibadilisha jina na kuita jina la skuli ya faraja, naiomba sana Idara ya Mazingira namuomba sana Mkurugenzi wa Mazingira, Serikali imetumia pesa nyingi karibu biloni 1 milioni 300 kuijenga Skuli ya Faraja lakini kitu ambacho kinaana kunitia wasi wasi skuli ile kama haijafanyiwa marekebisho sio marekebisho ya jengo, lakini marekebisho ya lile eneo lenyewe ilipo skuli yenyewe skuli ile tunaweza tukaja tukaikuta imekatika ukuta na kuanguka chini. Kwa hivyo kitu ambacho nakiomba Idara ya Mazingira tutafutane ili twende katika skuli ile kuna eneo ambalo Maji ya mvua yanapita tuangalie katika miradi yao kuweza kutengeneza mradi maalum wa kuweza kujaza kifusi na kuweza kuokoa eneo lile ili skuli ile isije ikaanguka.

Baada ya hayo machache naamini Mkurugenzi amenisikia lakini Mhe. Waziri yeye amenisikia zaidi naamini tutaweza kushirikiana ili kuokoa fedha za Serikali, baada ya kusema hayo machache nitaiiunga mkono hotuba hii baada

ya Mhe. Waziri kuja kukubali yale maoni yote ya kamati. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana kwa ustahamilivu wenu na utulivu wenu na kuweza kusikiliza hotuba zote hizi mbili ambazo zimewasilishwa mbele yetu. Na hapa ni mwisho wa kikao chetu cha leo na naliahirisha Baraza hadi kesho Saa 3.00 asubuhi.

(Saa 8.51 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 6/6/2017
Saa 3.00 asubuhi)